

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**BUNGE LA KUMI NA MOJA**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 6 Mei, 2019**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya  
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto  
kwa mwaka wa fedha, 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Swali letu la kwanza leo linaulizwa na Mheshimiwa Ruth Mollel, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 166

**Athari za Mtambo wa Kuchoma Takataka za Hospitali na Dawa Zilizokwisha Muda – Mkuranga**

**MHE. RUTH H. MOLLEL** aliuliza:-

Mtambo wa kuchoma takataka za hospitali na dawa zilizokwisha muda wake upo katika Kijiji cha Dundani Wilayani Mkuranga. Uchomaji unapofanyika moshi mzito huingia kwenye nyumba na maeneo ya wananchi wanaoishi karibu na mtambo huo na kuhatarisha afya zao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru afya na maisha ya wananchi wanaoishi karibu na mtambo huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba upo mtambo wa kuchomea taka na dawa zilizokwisha muda wake uliojengwa na mwekezaji katika Kijiji cha Dundani, Wilaya ya Mkuranga. Hapo awali mtambo huo ulikuwa na kasoro za ujenzi ambapo Serikali ilimwagiza mwekezaji kuzirekebisha kwa ilani ya tarehe 18, Oktoba, 2017 yenye kumbu. Na. *NEMC/HQ/EA/05/0702/VOL1/7* sambamba na

kusimamisha shughuli za mtambo mpaka kasoro zitakapokuwa zimerekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho hayo yamefanyika na baada ya mamlaka zote, ikiwemo Serikali ya Kijiji cha Dundani kujiridhisha kwamba hakuna tena moshi unaoathiri mazingira, mtambo huo umeruhusiwa kuendelea na kazi na mpaka sasa hakuna taarifa yoyote iliyofika katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Wilaya ya Mkuranga kulalamikia shughuli za mtambo huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na marekebisho ambayo yamefanyika, ni kwamba sasa ule moshi zamani ulikuwa unafika mbali, baada ya marekebisho ule moshi bado unatoka na bado unaathiri wananchi waliokuwa jirani, unasababisha watu kukohoa na harufu chafu kwa wananchi wanaozunguka lile eneo. Swali langu: Je, Serikali ilishafanya utafiti kwa sababu watu wanakohoa, tumejua ni madhara gani ya kiafya yanayosababishwa na moshi huo?

Swali langu la pili; ni kwa nini sasa *NEMC* wasirudi tena kule Dundani na kuhakikisha kwamba ule moshi unatafutiwa namna ambayo itaudhibiti usiendeleo kuchafua mazingira?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri kwamba Mheshimiwa Ruth Mollel ni Diwani wa kata husika, kwa hiyo, yeye ni mdau katika eneo hilo. Kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, kwamba mpaka sasa hivi hakuna taarifa ambayo imekuja Ofisi ya Mkurugenzi ikionesha kwamba kuna kasoro ambazo

Serikali inatakiwa irekebishe, naomba Mheshimiwa Mbunge kwa kutumia vikao vyake alipeleke hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sababu sisi tunajali afya ya mwananchi kuliko jambo lingine lolote, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na swali lake la pili kwamba angetaka *NEMC* waende kwa mara ya pili kutazama; kwa sababu mtaji wetu kwa mwananchi ni kuhakikisha kwamba ana afya bora, basi naomba nimhakikishie kwamba Serikali kwa kupitia *NEMC* tutakwenda kuchunguza na tujiridhishe pasi na mashaka kwamba hakuna madhara ambayo yanatokana na kichomea taka hiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa madawa yaliyokwisha muda wake (*expired drugs*) ni hatari sana katika maisha ya binadamu; na kwa kuwa baadhi ya maduka hayakaguliwi vizuri kuhakikisha kwamba madawa yaliyokwisha muda hayapo.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu ukaguzi wa maduka yote ambayo yana madawa hayo yaliyokwisha muda wake?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu zetu za afya, dawa zilizoisha muda au matumizi hazipaswi kutumika kwa matumizi ya binadamu. Mahospitali pamoja na wauzaji wa maduka binafsi wanatakiwa wazitenge tofauti na dawa ambazo zinaendelea kutumika ndani ya vituo vyetu vya kutolea huduma za afya lakini vilevile katika matumizi ya dawa za kuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu maalum ambao umewekwa ambapo dawa na vifaa vya hospitali havichomwi tu kama takataka nyingine, vina utaratibu wake na utaratibu huu upo. Nitoe rai tu kuhakikisha kwamba mamlaka ambazo zinasimamia ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya *TFDA* na Baraza la Famasia, basi wapite kuhakikisha kwamba wanatoa elimu hiyo na kuweka utaratibu mzuri wa uteketezaji wa hizi dawa ili zisije zikaingia katika mikono isiyo salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuta linaulizwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini na linaelekezwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora)

Na. 167

### **Zoezi la Kuwaondoa Watumishi Wenye Vyeti Fake**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Serikali katika kuhakikisha inapata watumishi bora na wenye sifa iliamua kuwaondoa watumishi wasio na sifa pamoja na wenye vyeti feki, lakini zoezi hilo lilikumbwa na changamoto mbalimbali ambapo Afisa Utumishi aliwaondoa watumishi kwenye *payroll* bila sababu maalum na walipofuatilia Wizarani walirudishwa kazini:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiunde timu maalum ili ipite kila Halmashauri kupitia taarifa juu ya zoezi hili ili haki itendeke hasa kwa wale ambao hawana uwezo wa kwenda Wizarani?

(b) Wapo watumishi ambao baada ya kuajiriwa kwa kutumia vyeti feki walijiendeleza kielimu zaidi ya Darasa la Saba na wameondolewa kwa kosa la udanganyifu wa vyeti: Je, Serikali haioni kuwa hao ni bora kuliko wale ambao hawakujiendeleza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na waajiri na Baraza la Mitihani la Taifa, Serikali iliendesha zoezi maalum la kuhakiki vyeti vya ufaulu mtihani wa Kidato cha Nne, Kidato cha Sita na Ualimu. Kupitia zoezi hilo, watumishi 15,189 walibainika kuwa na vyeti vya kugushi na kuondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara (*payroll*).

Hata hivyo, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa watumishi na vyanzo vingine kuhusu watumishi kuondolewa kimakosa au kwa uonevu katika orodha ya malipo ya mishahara, Serikali imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa karibu ikiwa ni pamoja na kuunda timu za ufuatiliaji wa utekelezaji wa zoezi hili. Jumla ya watumishi 4,160 waliobainika kuondolewa kimakosa au kwa uonevu wamerejeshwa kazini. Kati ya watumishi waliorejeshwa kazini 3,057 ni Watendaji wa Vijiji/Mtaa na Kata.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wanaojiendeleza zaidi ya Darasa la Saba wanafanya vizuri na Serikali inahimiza watumishi kujiendeleza kielimu. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ile ya D.12 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009, ni makosa kwa mtumishi kujipatia ajira kwa njia ya udanganyifu.

Hivyo Serikali ilielekeza waajiri kuwaondoa kwenye orodha ya malipo ya mishahara Watumishi wa Umma wote walioajiriwa kabla ya tarehe 20, Mei, 2004 ambao katika kumbukumbu zao rasmi za kiutumishi walijaza taarifa za udanganyifu kwamba walifaulu mitihani ya Kidato cha Nne, lakini hawakuthibitisha taarifa zao kwa kuwasilisha vielelezo vya sifa hizo kama vile taarifa binafsi (*personal records*).

Hivyo, pamoja na watumishi hao kujiendeleza kielimu, uamuzi wao wa kutoa taarifa za udanganyifu unawaondolea

sifa ya uaminifu na uadilifu kwa Serikali na hivyo wanakosa sifa za kuendelea kuwa Watumishi wa Umma. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, mkwe wangu, kwa majibu mazuri aliyoweza kunipatia, lakini (a) kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kati ya watumishi 15,000 walioondolewa waligundua kwamba watumishi 4,160 waliondolewa kimakosa. Hawa ni wale waliopata nafasi ya kuja Dodoma, Utumishi na kwenda Dar es Salaam kwenye Tume. Wale ambao hawakuwa na uwezo, tafsiri yake ni kwamba wamebaki huko. *(Makofi)*

Sasa swali; ni lini sasa Serikali itaunda tume ambayo angalau itakwenda kila Halmashauri au Mkoani pale iwaite wale wote waliokumbwa na mkasa huu wa kupoteza ajira waje ili vyeti vyao viweze kuhakikiwa ili wale ambao hawakupata nafasi ya kuja waweze kurudi kazini? *(Makofi)*

Swali la pili; tunatambua kwamba wako watumishi ambao wamekaa au wametumikia nchi hii katika kipindi kirefu na wengine walibakiza tu mwaka mmoja wastaafu na kwa bahati mbaya wamekumbwa na huo mkasa; Serikali ina mpango gani angalau hata kuwapa kifuta machozi ili waende wakaanze maisha yao huko waliko kuliko kuwaacha kama ilivyowaacha?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa

kufuatilia sana suala la watumishi wa Umma, hususan wale ambao walikuwa wameandika taarifa zisizokuwa na ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kujibu swali lake la kwanza; kwanza kabisa naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge na kwa faida ya Watanzania wengine na Watumishi wa Umma wote kwamba Serikali ilishafanya zoezi la ufuatiliaji kwa zaidi ya asilimia 95 na hilo zoezi limeshakamilika. Wale watumishi wote ambao waliandika taarifa zao siyo sahihi katika *personal records* au kwenye *OPRAS*, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba kama walidanganya watakosa stahiki zao zote kwa sababu Kanuni ya Utumishi wa Umma, kile kifungu D.12 kinasema mtumishi yeyote ambaye anaandika taarifa za uongo hataruhusiwa kuwa Mtumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali pia ilitoa msamaha hadi tarehe 31 Desemba, 2017, kwamba wale wote ambao walikuwa wamejiendeleza, basi waleta taarifa zao kwenye Ofisi yetu ya Utumishi maana ilishatoa msamaha ili taarifa zao ziweze kuingia na waweze kurudi kazini. Kwa hiyo, zaidi ya watumishi 500 wamesharejeshwa na wale ambao walijiendeleza baada ya muda huo basi waweze kutuletea vyetu vyao tuweze kuhakiki na waweze kurudi kazini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Naomba kuuliza kuhusu watumishi waliochishwa kazi kwenye hili zoezi wenye vyeti vya Darasa la Saba wakaenda chuo; kwa mfano kuna waliokwenda Chuo cha Simanjiro cha Mifugo wakapata vyeti, waka-*perform* vizuri wakaenda kusoma Diploma ya Udaktari wa Mifugo katika chuo cha Serikali kule Tengeru, lakini baada ya zoezi kupita walipogundulika tu kwamba hawana cheti cha *form four* –lakini hawajadanganya – wakaachishwa kazi.

Je, Serikali inaweza kutoa tamko gani kuhusu hawa ambao wanaona kwamba wameonewa?



**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lazima tukumbuke kwamba tarehe 20 Mei, 2004, baada ya hapo wale wote ambao walikuwa wametoa taarifa zisizo sahihi tulitoa msamaha hadi tarehe 31 Desemba, 2017 kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi na wale wote waliojiendeleza, kwa mfano katika masuala ya *recategorization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, Serikali tunasisitiza, tunathamini, tunaheshimu *recategorization* kwa wale wote wanaojiendeleza kimasomo. Nimesema kwamba hadi hiyo tarehe 31 Desemba, 2017 kama walijiendeleza na vyeti vyao viko sahihi, watulettee Utumishi tutahakiki watarejeshwa kazini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako maredeva ambao waliondolewa katika mfumo wa Serikali kwamba wamemaliza Darasa la Saba, kwa hiyo hawastahili kuwa madereva. Naomba kuiuliza Serikali, ni kigezo kipi ambacho kilitumika kuona kwamba dereva wa Darasa la Saba anaweza kuendesha gari vibaya kuliko yule wa Darasa la 12?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwanza naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali pia inawajali hata hao madereva wa Darasa la Saba. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba madereva wote wale wa Darasa la Saba ambao walikuwa wamebainika kwamba vyeti vyao viko safi na taarifa zao ziko safi na waliandika ukweli, wapo kazini na wanaendelea na kazi kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 168

### **Utaratibu wa Askari wa Barabarani Wanaojificha Vichakani**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Kumekuwa na baadhi ya Askari wa barabarani wanaosimamisha magari hasa yale ya safari ndefu wakitokea vichakani (kujificha) na hatimaye wakati mwingine kusababisha ajali:-

Je, ni Askari wangapi kama hawa wameshachukuliwa hatua za kinidhamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi nchini chini ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 iliyorejewa mwaka 2002, inamtaka Askari wa Polisi kuhakikisha usalama wa watumiaji wote wa barabara. Katika kutekeleza hilo, Polisi

wanatumia mbinu mbalimbali kwa mujibu wa sheria na taratibu ambazo zinawaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani kulikuwa na mfululizo wa ajali nyingi barabarani hususan zile ambazo zinahusisha magari ya abiria. Kwa kuzingatia hilo, Baraza la Usalama Barabarani lililbuni mkakati maalum uliofanikisha kupunguza ajali kwa asilimia 43 mpaka sasa. Mkakati huu ulihusisha mbinu mbalimbali zenye lengo la kuwalazimisha madereva kufuata sheria za usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina ushahidi wa matukio ya askari waliowahi kusababisha ajali barabarani kwa sababu ya kujificha. Hata hivyo, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Usalama Barabarani limejiwekea utaratibu wa kufanya uchunguzi wa kina kwa kila ajali kubwa inayotokea na kuchukua hatua stahiki inapobainika kuna uzembe wa usimamizi wa sheria au uvunjifu wa Sheria za Usalama Barabarani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, askari wa usalama barabarani wamekuwa na matukio ya kujificha vichochoroni, wanajificha vichakani sasa magari yanakuwa yanakwenda kwa *speed* na wanasimamisha gari kwa ghafla na huku nyuma kuna msururu wa magari. Hili Morogoro imeshawahi kutokea na Tukuyu imeshawahi kutokea kutokana na Askari wa Usalama Barabarani.

Je, Serikali ina mikakati gani kuwapitia askari wote ambao wanakaa kwenye vituo vya Usalama Barabarani kuhakiki hii tabia ya kujifichaficha vichochoroni kwani hakuna mbinu mbadala ya kusimamisha magari mpaka mtu utoke vuup na kusimaisha gari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa matrafiki wa barabarani uweledi wao wakufanya kazi baadhi yao ni changamoto hasa kwa barabarani. Je, Serikali ina mikakati gani kuwapeleke matrafiki wote kuwapa mafunzo ya mbinu mbadala na zile tochi kuzitumia kwa sababu zile tochi wananchi wamekuwa wakizilalamikia sana, wanaweza kusema unapigwa tochi wanasema inakwenda *speed*, lakini ile *speed* haifanani na ile tochi? Naomba majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Engineer Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Maryam Msabaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali langu la msingi kwamba tumefanikiwa kupunguza ajali kwa asilimia 43 na hususan ambazo zinasababishwa na magari ya abiria, mafanikio hayo pamoja na mambo mengine yalisababishwa kutokana na mbinu na uweledi wa askari wetu katika kubaini mbinu na njama ambazo zinatumika na madereva wasiokuwa waaminifu kuweza kukiuka sharia. Kwa hiyo hili suala ambalo amelizungumza kwa askari kukaa barabarani kuweza kujificha na mengine yote, malengo yalikuwa ni ya nia njema, lakini kama kutakuwa na upungufu katika utekelezaji wa hayo kwa baadhi ya askari basi tunachukua kama ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba dhamira ya Jeshi letu la Polisi kupitia Vikosi vya Usalama Barabarani si kuburuza wananchi, lakini kusaidia wananchi kuokoa maisha yao hususan kwa wale madereva ambao hawafuati sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la

nyongeza. Kumekuwa na tatizo kubwa wananchi kubambikizwa kesi hasa kwenye hizi kamera, mtu unapigwa kamera ukienda kuhoji wanasema kwamba imekosewa namba ya gari kwa hiyo wananchi wengi wamekuwa wanabambikiziwa makosa ambayo si ya kwao. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na kamera ambazo zimekuwa zinawabambikia wananchi makosa ambayo siyo ya kwao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi haya ya teknolojia tumeanzia na kamera, tuna mfumo *VTS* na tuna mambo mengine mengi ambayo tunaelekea nayo huko, yote haya yana dhamira ya kupunguza hizo dhana dhidi ya askari wetu kuhusiana na kubambikia watu makosa.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba matumizi ya tochi yamekuwa yakitusaidia sana. Hata hivyo, ikiwa kuna changamoto upungufu wa kimaadili wa baadhi ya askari wetu na hilo hatuwezi kulikataa kwa sababu askari nao ni binadamu huwezi kuwa na askari wote hawa wakose wawili watatu ambao watakuwa na upungufu wa kimaadili, tumekuwa tukiendelea kuchukua hatua pale ambapo tunapata taarifa na uthibitisho juu ya kubambikia wananchi makosa ambao hawahusiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kumsisitiza Mheshimiwa Mbunge kwamba tusaidiane kwa pamoja kufichua wale askari wachache ambao watakuwa wanatuhumiwa ama wanajihusisha na tabia kama hizo zilizokuwa kinyume na maadili ya utendaji kazi wa Jeshi la Polisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHH J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika kujibu swali la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali iliandaa mkakati maalum wa kudhibiti ajali barabarani na kwamba umetekelezwa kwa kiwango cha ajali kupungua kwa asilimia 43. Sasa Je, Serikali ipo tayari kuleta huo mkakati iliouandaa Bungeni pamoja na taarifa ya utekelezaji Bungeni ili tuweze kupima kama Wabunge ni ukweli ajali zimepungua kwa asilimia 43?

**MWENYEKITI:** Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Masauni, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Mnyika Mbunge wa Ubungo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleze kwanza kwa ufupi kabisa kuhusiana na mkakati huu. Mkakati huu upo kwa awamu, tulianza mkakati wa miezi sita ambao ulikuwa na lengo la kupunguza ajali kwa asilimia kumi, tukafanikiwa kupunguza ajali kwa asilimia kumi na moja. Tukaja mkakati wa awamu ya pili ambao ulikuwa miezi sita, tuka-*target* asilimia kumi, tukapunguza ajali kwa asilimia 45 nadhani. Tukaona kwamba tuna haja ya kuongeza sasa malengo tukaweka mkakati wa asilimia 25 kupunguza ajali wa miezi sita vilevile, ambao tulifanikiwa kupunguza ajali kwa asilimia 25. Hivi tunazungumza tupo katika mkakati wa awamu ya nne ambao tumelenga kupunguza ajali kwa asilimia 25. Kwa hiyo asilimia 43 tuliyozungumza ni kwa jumla wake kwa maana ya mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niliona nimpe kwanza utangulizi huo aelewe kwamba si mkakati mmoja, ni mkakati ambao tumekuwa tukijipima awamu kwa awamu kupitia Baraza la Usalama Barabarani na mkakati huu upo wazi na Mheshimiwa Mbunge atakapohitaji wakati wowote sisi tutakuwa tayari kumpatia. Tumekuwa tukifanya hivyo kwa sababu malengo ya mikakati hii tunapomaliza tunakuwa

tunashirikisha wadau mbalimbali ikiwemo Wabunge, hata yeye mwenyewe Mheshimiwa tulimwalika juzi katika Kongamano letu la Usalama Barabarani ambapo tulizungumzia mkakati huu Dar es Salaam na Wabunge wengine wa Mkoa wa Dar es Salaam wote, lakini bahati mbaya hatukumwona Mheshimiwa Mnyika japokuwa barua niliisaini mimi mwenyewe kwa mkono wangu ili kuonyesha kwamba hili jambo ni jambo shirikishi na tunatambua umuhimu wa kuwashirikisha na tutaendelea kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, lakini linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Sannda.

Na. 169

**Fidia kwa Watu Waliopisha Mradi wa Makaa ya Mawe  
Mchuchuma na Liganga**

**MHE. EDWIN M. SANNDI (K.n.y. MHE. DEOGRATIUS F. NGALAWA)** aliuliza:-

Serikali iliahidi kulipa fidia wananchi walioachia maeneo yao kupisha miradi ya makaa ya mawe, Mchuchuma na Liganga lakini mpaka sasa hawajalipwa:-

(a) Je, ni lini Serikali italipa fidia hizo ili wananchi husika waendeleo na shughuli nyingine za kiuchumi?

(b) Je, kwa nini Serikali haitoi mrejesho pindi panapotokea mkwamo?

(c) Je, Serikali inaweza kuthibitisha kuwa miradi hiyo itaanza kutekelezwa kama ilivyoahidi Bungeni?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Viwanda na Biashara *Engineer* Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uthaminishaji mali ya wananchi watakaopisha mradi unganishi wa Mchuchuma na Liganga awamu ya kwanza ilikamilika tarehe 18 Agosti, 2015, lakini ulipaji fidia kwa wakati huo haukuweza kufanywa. Kwa vile muda mrefu ulikuwa umepita, Serikali ilifanya uhakiki na uthaminishaji mwingine mwezi Desemba, 2018 ambapo imebainisha malipo stahiki yatakayopaswa kulipwa. Taratibu hizo zimekuwa shirikishi na zikifanywa kwa kuwahusisha Mamlaka husika ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo ya miradi. Malipo ya fidia kwa mujibu wa uthaminishaji wa sasa utafanywa pindi taratibu za msingi za kimaandalizi zikikamilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huo umeanza kutekelezwa kwa kufanya maandalizi ya awali ambapo pamoja na mambo mengine yanajumuisha upembuzi yakinifu wa mradi, uthaminishaji wa mali na maeneo ya wananchi watakaopisha mradi na kujenga barabara ya kiwango cha changarawe kuunganisha eneo la mradi na barabara kuu ya lami ili kuwezesha kufikisha mitambo na huduma nyingine katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo kasi ya utekelezaji imekuwa ndogo kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza hususan majadiliano na mwekezaji kuchukua muda mrefu zaidi kuliko tulivyotegemea. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuangalia njia bora zaidi ya kuwezesha mradi huo kuendelea kutekelezwa kwa tija na kuleta manufaa mapana zaidi kwa wananchi wa eneo hilo na Taifa letu kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngalawa mwenye swali la msingi.



**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Mradi wa Mchuchuma na Linganga umekuwa ukizungumzwa kwa muda mrefu sana kipindi ambacho sasa mpaka wananchi na Watanzania kwa ujumla wanakata tamaa. Sasa je, Serikali haioni kwamba sasa hivi hii hela ya fidia ingeichukua yenyewe badala ya kumwachia mwekezaji na watu wetu wakapata fidia hiyo mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili tumeona jitihada za Serikali kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya kutoka Mkiu - Liganga mpaka Madaba na ya kutoka Mchuchuma mpaka Liganga kilometa 70. Je, ujenzi hasa wa lami na kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanaweza kupitika yataanza lini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, *Engineer Stella Manyanya*.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla sijaendelea na maswali ya nyongeza kwa umuhimu wake kwa niaba ya wanaviwanda pamoja na Wizara yetu ya Viwanda kwa ujumla napenda kutoa pole kwa msiba mkubwa uliotupata kupitia kifo cha mwanakiwanda au mfanyabiashara wetu Mkuu ambaye alikuwa Mwenyekiti wa *Tanzania Private Sector Foundation*, Dkt. Reginald Mengi. Mwenyezi Mungu amrehemu na roho yake aiweke mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza swali la kwanza kuhusu Serikali uwezekano wa kulipa fidia, tunapotathmini mradi huu kuna njia mbili; ya kwanza ni kwa kumtumia mwekezaji aweze kulipa fidia, lakini Serikali inapokuwa na uwezo inaweza ikalipa yenyewe. Kwa hiyo, katika kuangalia mradi huu ambao una umuhimu sana kwa Taifa letu kutokana na rasilimali zilizoko pale, Serikali inaangalia uwezekano pia wa yenyewe kuweza kulipa fidia endapo itawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusiana na barabara kujengwa kwa kiwango cha lami, hayo yote yapo katika mchakato huo wa Serikali kujipanga ili kuwezesha mradi huu ufanyike kwa tija na kwa manufaa mapana ya Taifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda tu niongezee kwamba Serikali inayo mpango wa kujenga kiwango cha lami kuzingatia kama Mheshimiwa Mbunge anavyozungumza katika maeneo ambayo tumeya-*alert* kwa ajili ya uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma. Tumemaliza usanifu wa barabara kutoka Madaba kwenda Mkiu kilomita mia moja kumi na mbili, lakini pia eneo la barabara ya kutoka Mchuchuma kwenda Liganga, ziko kilometa 72 tumesanifu, Serikali ikipata fedha maeneo hayo muhimu tutajenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama ilivyo kwa wananchi wa Ludewa ni lini Serikali itaweka na kuharakisha utekelezaji wa kuwalipa fidia wale wananchi wa Wilaya ya Kyela waliopisha mradi wa *Boarder Post?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, naona wenye barabara wako, hebu subiri namwona Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. Magufuli alipokuwa ziara Kyela ametoa maelekezo ili tuweze kuwalipa mara moja wananchi katika eneo hili, nimwarifu tu Mheshimiwa Mbunge, nami nimeongea na wananchi hawa baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais na tunalifanyia kazi suala hili ili tuweze kuwalipa wananchi hawa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mwakagenda avute subira, sisi tumejipanga kama Serikali na kwa sababu Mheshimiwa Rais pia amekuwa na *concern* hiyo, wananchi watapata haki zao mara moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum na bado inaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Na. 170

### **Serikali Kujenga Viwanda Mkoa wa Rukwa**

**MHE. SILAFU J. MAUFI** aliuliza:-

Mkoa wa Rukwa umeanzishwa mwaka 1974 lakini hadi sasa hakuna viwanda vikubwa vilivyowekezwa na kuwekewa mikakati na Serikali na viwanda vilivyopo ni vya watu binafsi:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kujenga viwanda au kupeleka wawekezaji ambao watajenga viwanda vikubwa Mkoa wa Rukwa ili kutoa ajira kwa vijana?

(b) Mazao yanayolimwa Mkoa wa Rukwa yanapewa bei kiholela na kufanya maisha ya wananchi kuwa magumu? Je, ni lini Serikali itaingia mkataba na viwanda vya uzalishaji?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara *Engineer Stella Manyanya*.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jukumu la Serikali katika ujenzi wa viwanda ni kuwepo mazingira rafiki na wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza na kufanya shughuli za kiuchumi ikiwemo kuzalisha na kufanya biashara. Msimamo huo wa kisera unaihusu mikoa na sekta zote za kiuchumi. Kwa msingi wa utaratibu huo wa kisera, Serikali imeelekeza nguvu zake katika kujenga na kuboresha miundombinu wezeshi na saidizi hususan umeme barabara, maji na mawasiliano. Aidha, katika kuhamasisha uwekezaji, Serikali imeitaka mikoa yote nchini kuandaa Taarifa za fursa za uwekezaji zilizopo (*Regional Profiles*) katika maeneo yake na kuvitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pPia Serikali imeanzisha Mkakati wa zao moja Wilaya Moja (*ODOP*) ili kila Wilaya nchini ijielekeze katika kuendeleza angalau zao moja litakalovutia uwekezaji wa viwanda. Mkakati huu utasaidia kila Wilaya zikiwemo za Mkoa wa Rukwa kuwa na kiwanda angalau kimoja kinachotumia rasilimali zilizopo katika wilaya hizo. Hivyo, natoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote tushirikiane kuainisha fursa zilizopo na kuzitangaza kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mkataba hapa Tanzania kwa sasa kinatumika katika baadhi ya mazao yakiwemo miwa na tumbaku. Katika utaratibu huo wakulima hukubaliana na wanunuzi/viwanda kupewa baadhi ya huduma zikiwemo pembejeo kwa masharti ya kuwauzia mazao hayo na gharama za huduma au pembejeo hizo

hukatwa wakati wa malipo. Katika utaratibu huo Serikali haihusiki moja kwa moja katika kuingia mikataba hiyo bali Maafisa Ugani huwasaidia wakulima kuangalia iwapo mikataba husika itakuwa na tija. Tunawahimiza wananchi kuwa makini wakati wa kuingia mikataba hiyo na wanunuzi. Aidha ili kupata nguvu ya soko, ni muhimu kuuza mazao kupita vyama vya ushirika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maufi.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini bado napenda kufahamu kwamba, ikiwa mikoa na wilaya zimeweza kutanganza fursa ambazo zimo ndani ya mikoa husika, lakini bado mikoa ile ama wilaya zile zinasuasua katika kupata wawekezaji; Je, Serikali haioni umuhimu wa wao wenyewe kwenda kusukuma katika mikoa ile na wilaya zile kuweza kupata viwanda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili la nyongeza, napenda kufahamu kwamba wanapewa muda upi wa utangazaji wa fursa na kama fursa haina majibu Serikali inachukuwa mkakati gani katika mkoa huo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili ya nyongeza, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maufi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuupongeza sana Mkoa wa Rukwa umekuwa ukifanya makongamano mbalimbali ya kuhamasisha uwekezaji na makongamano hayo kwa kweli yamekuwa yakiza matunda. Kwa mfano, wameweza kuhamasisha na kupata kiwanda cha kusindika unga wa mahindi, Kiwanda cha *Energy*, vilevile wameweza kuhamasisha na mpaka kuwezesha mradi wa makaa ya mawe kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali hatuiachi mikoa peke yao isipokuwa mikoa yenyewe kwa sababu inazo fursa hizo kwa karibu zaidi inapohamasisha inaungana na Serikali Kuu kuona kwamba hawa wenye viwanda waweze kwenda kuwekeza huko. Sisi kwa kutumia *Tantrade, TIC* na Wizara kwa ujumla kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji tumekuwa tukiendelea kuhamasisha wenye viwanda au wawekezaji mbalimbali kwenda kwenye maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Yule amesimama amekaa? Mheshimiwa Mlinga. *(Kicheko)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa ambayo ilikuwa vinara wa kuwa na viwanda vingi na imekuwa kitoa ajira nyingi sana kwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro enzi hizo za ujana wetu.

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vilikuwepo viwanda vya maturubai, magunia, ngozi, mafuta ya kupikia, vipuli vya mashine, mazulia hata Ulanga tulikuwa na kiwanda cha pamba lakini baada ya ubinafsishaji viwanda vyote vikawa *kushne*, vikawa magofu ya kufugia mbuzi na Serikali imekuwa ikipiga mikwara mara kwa mara...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, Serikali inatoa kauli gani sasa kwa magofu hayo ambayo yamegeuzwa na wawekezaji badala ya kufanywa kuwa viwanda?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri, tusipoteze muda na historia.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Goodluck, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba wale wote waliokuwa wamebinafsishiwa viwanda na hawajaweza kuviendeleza kama ambavyo mkataba wao ulikuwa na ambavyo Serikali ilitarajia, tunatarajia viwanda hivyo vitarejeshwa. Mpaka sasa Serikali imesharejeshwa viwanda 15 na tunaendelea na zoezi hilo ili hivi viwanda viweze kufanya kazi kwa tija iliyokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Korogwe Mji tulikuwa na kiwanda cha matunda na kama tunavyofahamu Mkoa wa Tanga una kilimo sana cha matunda. Kiwanda kile baada ya kubinafsishwa, yule mwekezaji ni miaka karibu 20 sasa kiwanda kile alishang'oa mashine zote na mabati yote yameshatolewa. Je, mtakuwa tayari sasa kutukabidhi eneo lile ili kusudi tuweze kuwawekea vijana shughuli za kufanya katika eneo lile?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, jibu kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mary Chatanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kiwanda hicho kinachozungumzwa nimekitembelea na kwa kweli hatuwezi kuendelea kukiita kiwanda na Mheshimiwa Waziri alishakitolea kauli ya kukifuta katika orodha ya viwanda. Kwa hiyo, kama ni eneo, naamini linaweza likatumika kwa Halmashauri inayohusika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Msingi wa swali langu uko kwenye swali namba 170, kipengele (b) kuhusiana na suala la bei ya mazao kwamba imekuwa ni holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara itueleze, kwa sababu watu wa Wizara ya Kilimo wanasema wao walishamaliza kazi ya kukusanya, je, korosho ghafi na korosho iliyobanguliwa mnaiuza kwa shilingi ngapi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, jibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi baada ya Serikali kufanya uamuzi wenye hekima kabisa wa kununua korosho kwa hawa wananchi ili kuwapunguzia maumivu ya kuuza kwa bei mbaya, korosho iliyopo sasa hivi tunaendelea kuiuza na hatujapanga bei maalum, inategemeana na mteja anavyokuja na pale itapofikia sisi kuwa imelipa gharama zetu zile ambazo tulitumia. Kwa misingi hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mwambe ukiwa pia ni mdau na mwananchi mwingine yeyote anayenisikia hata watu wa nje korosho ghafi zipo na zilizobanguliwa zaidi ya tani 391 zipo na ziko katika hali nzuri basi yeyote anayetaka kununua karibu sana aweze kuuziwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika miaka ya 70 na 80 Serikali ilikopa kutoka Japan na Italia dola milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya korosho katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Wakati wa ubinafsishaji viwanda hivyo vilibinafsishwa lakini hadi leo viwanda hivyo havifanyi kazi. Mara nyingi Serikali imesema hapa Bungeni itakaa na wawekezaji kuona kwamba...

**MWENYEKITI:** Hebu uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali linakuja, ni kwa nini Serikali imelidanganya Bunge mara kadhaa kwamba itakaa na wawekezaji ili waweze kusaidia viwanda hivi na wananchi wapate manufaa yanayohitajika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi katika viwanda hivyo vipote ambavyo vinafanya kazi vizuri na vimeajiri zaidi ya watu 750 kwa kimoja. Kwa mfano, kiwanda cha Tunduru, cha Korosho Afrika lakini pia Kiwanda cha Newala *Micronics*, hivyo vimeajiri watu 750 kila kimoja lakini pia *Micronics* pale Mtwara kimeajiri kama watu 350. Vilevile kuna Kiwanda cha Mtwara kinachohusika na korosho pia ambacho sasa hivi ndicho kinachosaidia kufungasha hizo korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kuna baadhi ya viwanda havikufanya vizuri, kwa mfano, Kiwanda cha Mtama na Kiwanda cha Nachingwea, hivyo tumeshavyang'anya. Pia kuna Kiwanda cha Lindi Buko, nacho tumeshakinyang'anya na tumeshaanza kukifufua. Hiyo ndiyo hali halisi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata 171 linaulizwa na Mheshimiwa Nuru Awadh, Mbunge wa Viti Maalum kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia.

Na. 171

### **Mafunzo ya Muda Mfupi kwa Walimu**

**MHE. NURU A. BAFADHILI** aliuliza:-

Katika kipindi cha miaka ya 1970 wakati wanafunzi wakienda likizo walimu walikuwa wakienda katika vyuo mbalimbali vilivyokuwa jirani na wilaya zao ili kupewa mafunzo au kupigwa msasa (*refresher courses*) kiasi kwamba walimu walikuwa wanapata ari ya kufundisha vizuri:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha utaratibu huo kwa walimu kupigwa msasa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadh, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa mafunzo endelevu kwa walimu kazini kulingana na upatikanaji wa fedha. Mafunzo hayo yanalenga kuboresha utendaji kazi na kutoa motisha kwa walimu ili kuinua ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, jumla ya walimu wa Shule za Msingi 1,598 wamepata Mafunzo

juu ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Aidha, walimu wa Shule za Msingi 200 na Sekondari 198 wamejengewa uwezo katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Hisabati. Vilevile, walimu wa Elimu Maalum 804 wamejengewa uwezo katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga kiasi cha Sh.502,807,348 kwa ajili ya kufanya mapitio na tathmini ya Vituo vya Walimu (TRC) kwa lengo la kuviwezesha kutoa mafunzo kazini kwa walimu kama ilivyokuwa inafanyika hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inakamilisha maandalizi ya Kiunzi cha Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini ambacho kitatoa utaratibu wa uendeshaji wa mafunzo hayo ili kuweka msukumo zaidi wa mafunzo kazini. Napenda kutumia nafasi hii kuzihamasisha Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo kazini kwa ajili ya walimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nuru Awadh.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mbali na hayo masomo yaliyokwishafundishwa kuna somo la TEHAMA ambalo sasa hivi linafundishwa katika shule mbalimbali lakini kuna baadhi ya walimu katika shule za msingi hawana ujuzi wa kutumia kompyuta. Je, Serikali ina mpango gani ya kuwapa mafunzo walimu hao ili tuendane na wakati huu wa utandawazi na digitali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa walimu wanafanya kazi zao vizuri na tunastahili kuwapa motisha. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa ile *Teaching Allowance* kama walivyowapa Wakuu wa Shule pamoja na Waratibu ili nao waweze kuipenda kazi yao na kupata morali ya kufundisha? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya maswali haya mawili, kwa ufupi tu, Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nuru Awadh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kuwajengea walimu uwezo katika masuala ya TEHAMA, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa TEHAMA ni kati ya maeneo mapya ambayo lazima walimu wote wajengewe uwezo kwa sababu katika enzi tulizopo sasa TEHAMA ni moja ya vitu muhimu katika elimu. Kwa hiyo, katika mipango ya Serikali TEHAMA ni moja kati ya maeneo muhimu ambayo walimu watajengewa uwezo na hili litafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la motisha, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya walimu kadiri ya uwezo utakavyoruhusu. Siku za mbele hata masuala ya motisha ni moja kati ya masuala ambayo yanaweza yakaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi ni Naibu Waziri wa Elimu, naomba nitumie fursa hii vilevile kuwatakia kila la kheri vijana wetu 91,440 wa Kidato cha Sita na wale 12,540 wa Vyuo vya Ualimu ambao leo wanafanya mitihani yao ya mwisho. Hata hivyo, nitoe rai kwao kwamba wafuate sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza mitihani na kamwe wasije wakajihusisha na vitendo vya wizi na udanganyifu katika mitihani.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Na. 172

## Hitaji la Viwanda vya Nyama, Ngozi na Maziwa Nchini

**MHE. JULIUS K. LAIZER** aliuliza:-

Tanzania ni nchi ya tatu (3) Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya takribani mifugo milioni 25 lakini sekta hii bado mchango wake katika pato la Taifa ni ndogo ukilinganisha na idadi ya mifugo tuliyonayo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga viwanda vya nyama, ngozi na maziwa hapa nchini ili kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na mifugo?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kutoa ruzuku ya madawa kama Ndigana Kali, Homa ya Mapafu na dipu kwa wafugaji wetu nchini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mkakati wa kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini kwa kuboresha kosaafu, malisho, kuelimisha wafugaji kuhusu ufugaji wa kisasa, kuimarisha utafiti na kuweka mazingira bora ya kuvutia wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kusindika na kuongeza thamani mazao ya mifugo. Aidha, Wizara kupitia Taasisi ya *NARCO* imeingia mkataba na Kampuni ya *NECAI* ya Misri kujenga kiwanda cha kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo katika Mkoa wa Pwani (Ruvu). Aidha, viwanda kumi na nne (14) vya nyama na maziwa vipo katika

hatua mbalimbali za ujenzi kikiwemo kiwanda cha kisasa cha *Elia Foods Overseas Ltd* kinachojengwa katika Wilaya ya Longido kitakachokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 400 na mbuzi 2,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mkakati wa kudhibiti magonjwa ya mifugo, Wizara imenunua na kusambaza kiasi cha lita 8,823 za dawa ya kuogesha mifugo (dipu) kwa ruzuku ya asilimia 100 katika mkoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, Serikali imewezesha uzalishaji wa chanjo muhimu nchini zikiwemo chanjo za Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) kupitia Taasisi ya TVLA pamoja na kuanzisha mfumo wa ununuzi wa dawa, chanjo na viwatilifu kwa pamoja (*Bulk Procurement*) ili kurahisisha usimamizi na upatikanaji wa pembejeo hizi kwa urahisi na kwa bei nafuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, sekta hii ya mifugo bado inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwepo utitiri wa tozo mbalimbali kwa wafugaji ambao karibu ng'ombe moja tozo zake zinazidi shilingi elfu hamsini. Swali la kwanza, je, nini mkakati wa Serikali kuwapunguzia wafugaji tozo hizo ili waweze kuzalisha kwa tija?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tatizo linalowakabili wafugaji wengi nchini ni pamoja na ugonjwa wa Ndigana Kali ambapo wafugaji tunapoteza zaidi ya asilimia 60 ya ndama wakati wanapozaliwa na chanjo hii bei yake ni shilingi 12,000 kwa ndama. Je, nini mkakati wa Serikali wa kuweka ruzuku au kuondoa kodi katika chanjo hii ili wafugaji waweze kumudu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, kwa ufupi tu Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya mawili ya Mheshimiwa Laizer, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utitiri wa tozo, Wizara imeendelea na utaratibu wa kupitia tozo zote zinazotozwa katika sekta hii ya mifugo na zile zinazoonekana kuwa ni kero kwa wafugaji wetu na wafanyabiashara wa mifugo tumeendelea kuzipunguza. Vilevile zile ambazo zimeonekana kuwa ziko chini tumeendelea kuziongeza kwa manufaa mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili anataka kujua kuhusiana na chanjo. Taasisi yetu ya TVLA na TV/mpaka sasa Tanzania sisi wenyewe tumefanikiwa kutengeneza chanjo tano na chanjo ya Ndigana Kali ni miongoni mwa chanjo tunayoifikiria kuiongezea. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili lipo katika mkakati wa Wizara na yenyewe itatengenezwa hapa Tanzania na tutakapofanikiwa itapunguza bei na kuwasaidia wafugaji wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matembe.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Singida kama ilivyo Monduli ni mabingwa wa kufuga ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuanzisha kiwanda kikubwa cha ngozi na nyama ili kuendana na falsafa ya Tanzania ya Viwanda?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Singida juu ya kuanzishwa kiwanda cha kuchakata nyama na mazao ya mifugo katika Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba Serikali imekuwa na mkakati huo na maeneo mbalimbali katika Taifa letu hivi sasa viwanda vinajengwa. Wazo hili la kujenga pale Manyoni ni jema, naomba tulichukue tulipeleke kwa wawekezaji ili tuweze kupata kiwanda pale Manyoni ambako ni *center* kwa mifugo inayotoka katika Mkoa wa Kigoma na Mikoa ya Bara kwa maana ya Shinyanga na hata Nzega na Tabora wote wanaweza kupata huduma hii ya kuchakata mifugo kwenye eneo hili kwa kuwa eneo hili ni la kimkakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na. 173

### **Sera ya Kupunguza Idadi ya Mifugo Nchini**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y. MHE. AUGUSTINE V. HOLLE)** aliuliza:-

Migogoro ya wafugaji na wakulima nchini imekuwa ya kudumu na hivyo kusababisha vifo kwa watu na uharibifu wa mali:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kuja na Sera ya kupunguza idadi ya mifugo nchini ili kuwa na ufugaji wenye tija?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza mpango wa kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu ufugaji bora na uzalishaji wa malisho kupitia mashamba darasa ili kufuga kwa tija pamoja na kuendeleza malisho katika maeneo yaliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu inayotolewa itawezesha uboreshaji wa kosaafu za mifugo, udhibiti wa magonjwa, matumizi sahihi ya madawa na viuatilifu, uelewa wa sheria, kanuni na miongozo ya sekta ya mifugo ili kuepokana na migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Aidha, elimu inalenga kuwaongezea wafugaji maarifa kwa kuwapatia teknolojia mpya ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa na kibiashara nchini. Pia elimu hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji wa malighafi zitokanazo na mifugo zenye viwango bora ili kukidhi mahitaji ya viwanda vya vyama, maziwa na ngozi vinavyoendelea kujengwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango wa kufanya mapitio ya sera ya Taifa ya mifugo ya mwaka 2006 ili iweze kuendana na mabadiliko ya mazingira ya sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Msitu wa Makele kusini ambao tayari umesha poteza sifa ya uhifadhi, na kwa kuwa tayari yapo maelekezo ya kutoa sehemu ya misitu hii kwa sababu ya wafungaji ili kuondoa usumbufu uliopo kwa nini sasa Serikali isitoe msitu huu wa Makele kusini kwa ajili ya wafugaji?

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili la mifugo imekuwa na changamoto kubwa, sambamba na Jimbo la Nyamagada unapozungumzia masuala ya mifugo kwenye minada ya upili watu wana Nyamagana hawana kabisa eneo la kufanyika shughuli zao za uchinjaji na kwa maana mnada. Na kwa sababu na mifugo hii imekuwa inatangatanga mtu anayetoa mfugo Magu lileta Mwanza au anayetoa mfugo Kwimba kuleta Mwanza analazimika kupeleka Misungwi kwenye mnada wa upili ndio arudishe Nyamagana kwa ajili ya uchinjaji au llemela na matokeo yake kuongeza gharama za mchinjaji. Ni nini Serikali inatoa kauli gani juu ya minada hii kwa nini usirudishwe pale pale ulipo Nyamagana na watu wakachinja kwa uzuri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni juu ya kuomba msitu wa Makele kusini kupewa wafugaji. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwaka 2016 alipotembelea katika Mkoa wa Kigoma, alipita katika Wilaya Kasulu na wananchi wa Kasulu walimpa maombi yao ya kuomba msitu huu wa Makele kusini upewe wananchi kwa maana ya shughuli za ufugaji na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alielekeza hekta zipatazo 10,000 zitolewe kwa vijiji viwili 5,000 na 5,000 zigawiwe kwa Halmashuri ya Kasulu. Watendaji wa *TF*Skupitia Wizara ya Maliasili na Utalii wametokeleza agizo hili na wananchi wa Kasulu wamepatiwa. Hivi sasa tulichokipendekeza baada ya maelekezo mengine juu ya Rais wetu juu ya kuwapa wafugaji na wakulima maeneo ya ziada kwa ajili shughuli zao tumependekeza eneo la Mkuti katika Wilaya Kasulu na Uvinza ndio sasa yaelekezwe kuangaliwa kama yamepoteza sifa yapewe wafugaji na wakulima. Naomba Mheshimiwa Vuma na wafugaji na wakulima wote katika Wilaya ya Kasulu waendeleo kuwa na subra pindi jambo hili litakapokuwa tayari watapata manufaa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linahusu minada ya Upili na kwa nini wachinjaji wa pale Mwanza Jiji wanalazimishwa kupeleka mifugo yao katika mnada wa Upili wa Msungwi ndipo waende kuchakata mifugo hiyo pale Mwanza Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni urasimu kwa sababu mifugo tumekubaliana ya kwamba minada ya Upili dhumuni lake ni kwa ajili ya wafanyabishara kwa kiwango cha kati na kuwango cha juu. Kwa wale wafanyabishara wadogo wadogo wenye ng'ombe mmoja wawili ama mbuzi mmoja wawili wanaruhusiwa kununua katika minada yao ya misingi na kwenda kuchakata moja kwa moja kwa ajili yakuweza kufanya shughuli hizi za kujipatia kipato na kuhudumia wananchi. Natoa maelekezo kwa watendaji wetu wasimamie sheria kanuni zetu bila kuathiri wananchi wetu na kuinua vipato vyao na kuendeleza maisha yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa kwa sababu ya muda tunaendelea swali linalofutata linaulizwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka Mbunge wa Liwale linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Hamida upo? Aaaaah.

Na.174

### **Mgogoro wa Mpaka Kati ya Kijiji cha Kikulyungu na Hifadhi ya Selous**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Mgogoro wa mipaka kati ya Kijiji cha Kikulyungu na Hifadhi ya Selous ni wa muda mrefu:-

Je, Serikali itamaliza lini mgogoro huo?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa swali hilo Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa mgogoro wa mpaka kati cha kikulyungu na poro la Akiba Selous umekuwepo kwa muda mrefu. Chanzo cha mgogoro huo ni wananchi wa kijiji hicho kufutiwa kibali cha kuvua samaki katika bwawa la kihurumila ambalo limo ndani ya Pori la Akiba Selous baada ya wananchi wa kijiji hicho uanza kuvua kwa njia zisizo endelevu au haribifu ikiwemo kutumia sumu. Baada ya kufutiwa kibali wananchi wa Kikulyungu walianza kulalamika na kudai kuwa mpaka wa Selous na kijiji hicho upo mto Matandu jambo ambalo ni kinyume na Tangazo la Seriklai Na.475 la Mwaka 1974.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uhakika wa mipaka imekamika na taarifa imewasilishwa Wizarani kwangu. Aidha, zoezi la kuhakika mipaka hiyo lilienda sambamba na uwekaji wa alama za kudumu baada ya maridhiano ya pande zote kwa kuzingatiwa tangazo la Serikali kuanzishwa kijiji cha Likulyungu, Tanganzo la Serikali kuanzishwa pori la Akiba la Selous GN. Na. 275 la 1974 na Tanganzo la Serikali la kuanzishwa pori tengefufu Kihurumila Na.269 ambalo pia ni la mwaka 1974 lililopo kati ya kijiji cha Likulyungu na pori la Akiba Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uhakiki huo umefanywa na wataalam kutoka Wizara yenye dhamana ya ardhi na kushirikisha pande zote zilizohusika katika mgogoro huo, ni imani kuwa mgogoro huo umemalizika.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante wa majibu ya Serikali athari kubwa ya mgogoro huo ni kijiji cha Kikulyungu kuondolewa kwenye WMA ya Jumuiya ya Magingo na kwa majibu haya inaonekana mgogoro huu umefika mwisho.

(i) Sasa ni lini Serikali itakuja Kikulyungu kuwapa wananchi matokeo ya maamuzi haya na kuwapa kibali au kuwapa kibali au kuwapa hati ili waweze kurudishwa kwenye Jumuiya ya Magingo?

(ii) Na kwa sababu sisi tunaishi kwenye maeneo ya hifadhi kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa mazao unaotokana na wananyama waharibifu kama tembo, nguruwe, na wananyama wengine waharibu. Na Serikali imekuwa ikitoa kitu kinachoitwa kifuta machozi sasa ni lini Serikali itakuja na marekebisho ya sheria ili badala ya kutoa kifuta machozi iwe wananchi wao wanapata fidia inayotokana na uharibifu wa mazao ya mashambani?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa maswali hayo mawili kwa kifupi tu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka Mbunge wa Jimbo la Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuahidi kwa kuwa taarifa ya kamati ambayo ilienda kuhakiki mipaka imekamilika na ipo mezani kwangu, kwamba baada ya Bunge hili la Bajeti kuisha aidha nitaenda mwenyewe ama nitamtuma Mheshimiwa Naibu Waziri kwenda kuzungumza na wananchi wa kijiji cha Kikulyungu kwenda kuwapa matokeo ya taarifa ya kazi iliyofanywa na kamati iliyokuwa chini ya uzongozi wa Wizara ya Ardhi ambayo ili hakiki mpaka ule kwa hivyo ni lini baada ya Bunge la Bajeti kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kuhusu Serikali kuachana na kulipa kifuata machozi ama pia na kifuta chasho kutokana na uharibifu wa unaofanywa na wanyama wakali na waharibifu badala yake tulipe fidia. Ngumu kwa

Serikali kuji-*commit* kwamba itaanza kulipa fidia ya uhalibifu unaofanywa na wanyama wakali na wanyama waharibifu na sababu zipo wazi. Kwa mfano mnyama amesababisha umauti wa raia wa mwananchi huwezi kusema utalipa fidia ya mnyama kuua mwanadamu kwa sababu thamani ya mwanadamu haiweezi kulinganishwa na kitu chochote kile.

Kwa hivyo, hiyo ni bahati mbaya ambayo inakuwa imetokea tunachoweza kulipa pale ni kufuta machozi na sio fidia. Lakini thamani ya mazao vilevile ni ngumu kusema Serikali itaji- *commit* kulipa fidia balada ya kufuta jasho kwa sababu changamoto zilizopo ambazo zinahusiana na wanyama hawa kwenda kwenye maeneo ni nyingi wakati mwingine wananchi wanawafuata wanyama kwenye mapito yao ama kwenye mazalia yao ama maeneo ya mtawanyiko na wakati mwingine sisi viongozi tukiwemo Wabunge, madiwani tunahamasisha sana Serikali imege maeneo ya hifadhi ambayo kiuhasili ni lazima yatapitiwa na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kusema Serikali itaji-*commit* kwa kweli kulipa fidia ni jambo gumu kwa sababu gharama itakuwa kubwa sana mwisho wa siku tutashindwa kutunza hizi maliasili ambazo sisi zote tunapaswa kuzilinda kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 27.

Kwa hivyo ninawaomba sana wa kwa Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wote watambue kwamba wanyamapori ni maliasili ya Taifa, ni utajiri, ni urithi wa Taifa letu na hatuwezi kwamwe kuacha kuilinda kwa ajili ya matumizi ya sasa na vizazi vijavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea kwa sababu ya muda swali linalofuta linaulizwana Mheshimiwa Hawa MchafuChakoma Mbunge wa Viti Maalum linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Na. 175

**Miradi ya Maji Vijiji vya Lupunga, Ruvu Dosa na Kipandege-Kibaha**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Miradi ya maji katika vijiji vya Lupunga, Ruvu Dosa na Kipandege Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha bado inasuasua mpaka sasa.

Je, ni lini miradi hiyo itapatiwa fedha ili iweze kukamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Lupunga uliopo Kata ya Kikongo ulianza kutekelezwa Novemba, 2013 na ulikamika mwaka 2016 na unaendelea kutoa huduma ya maji katika vitongoji tisa vya Ngeta, kikongo, Lupunga, Mwanabwito, Makongotopola, Kisabi, Madimula, Msongola na Makazi Mapya kwenye mamlaka ya mji mdogo wa Malandizi. Mradi huo ulikuwa na changamoto za kiundeshaji ambapo kamati ya Maji ya awali ilivunjwa na kuundwa kamati mpya inaendelea kutoa huduma ya maji maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Ruvu kwa Dosa uliopo katika Kata ya Matambani ulianza kutekeleza mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2016 kutoka bomba kuu la DAWASA. Kwa sasa mradi unaendelea kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi 1800 kwa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji kipandege uliopo katika Kata ya Soga ulianza kutekelezwa Novemba, 2013 na kukamilika mwaka 2017. Mradi huo kwa sasa una changamoto za kiufundi ikiwa ni msukumo mdogo wa maji toka bomba la DAWASA. Tayari Mkandarasi na Mhandisi Mshauri aliyesanifu wanashukulikia tatizo hilo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha miradi yote inatoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa maeneo hao.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chakoma.

**MHE. HAWA MCHAFU CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri sasa ningependa nimuulize maswali wadogo wawili yangongeza. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuikabidhi miradi ya serikali kwa DAWASA ikiwemo mradi wa Bokomnemela Vikuruti na Ngeta.

(i) Ni lini sasa DAWASA itakamilisha zoezi la ufungaji maji majumbani ikizingatiwa wananchi wanauhitaji mkubwa wa maji na hivi tunavyozungumza ni nyumba 30 tu zilizofungwa kati ya wananchi wote walojaza fomu?

(ii) Nataka kujua ni kwanini DAWASA wanafanya ucheleweshaji wa kijiji cha kipangege Kata Soga. Kijiji hakipati maji ya kuridhisha presha yake ni ndogo na wakati mwingine hakuna kabisa maji nataka kusikia kauli ya Serikali inasema nini juu ya uchelewashi huu unaofanywa na DAWASA?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji majibu kwa maswali hayo kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ni miongoni mwa Wabunge makini katika ufuatiliaji na kupigania maendeleo ya watu wake katika Mkoa wa Pwani. Lakini kikubwa maji hanaya mbadala sasa niagize Mkurugenzi wa Mamlaka wa Majisafi na Usafi wa Mazingira DAWASA Eng. Luhemeja katika kuhakikisha suala la ufungaji mita kwa



wananchi lakini pia mradi huu wa Soga uwezi kukamilika kwa wakati ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na niweze kuuliza wali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo yanayowapata watu Kibaha yanafanana na watu wa Kigamboni

Je Serikali ina mpango gani wa kukamilisha mradi wa visima vya Kimbiji na Mpera ili wananchi wa Kigamboni, Tuangoma, Chamazi na Mbagala waweze kupata maji safi na salama?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya lakini kikubwa katika kuhakisha tunatatua tatizo la maji katika Mkoa wa Dar es Salaam. Wizara yetu ya maji kupitia Wizara ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira DAWASA imechimba visima zaidi ya 20 Mpera na Kimbiji. Sasa agizo la Mheshimiwa Waziri nikuhakisha visima vitano wanatangaza tenda mkandarasi ampatikane ili wananchi wa maeneo ya Kigamboni na Mbagala waweze kupata maji safi, salama na ya kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tupo katika hatua hiyo tunataka mkandarasi akapopatikana kazi ianze mara moja na wananchi hawa waweze kupata maji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuko nyuma ya muda. Wageni walioko jukwaa la Spika wageni 55 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Maafisa kutoka kampuni za simu za mikono ambazo ni TTCL, Airtel, Tigo, Vodacom, Halotel na Zantel ambao wamekuja kufanya usajiri wa *line* za simu kwa kutumia alama za vidole kwa waheshimiwa Wabunge na

Watumishi wa ofisi ya Bunge kuanzia tarehe 06 hadi tarehe 13 Mei, 2019 wakiongozwa na asa kutoka TCRA Ndugu Godliving Kessy wapo wapi karibuni sana wageni wetu. Waheshimiwa Wabunge tuitumie fursa hiyo vizuri. *(Makofi)*

Wageni pia wa Waheshimiwa Wabunge tuna mgeni wa Mheshimiwa Stella Ikupa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeishughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu ambaye ni Mwandishi wa Habari kutoka Jiji Dar es Salaam ndugu Danson Rioba.

Wageni sita wa Mheshimiwa Jumaa Aweso Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ambao ni ndugu zake kutoka pangani Mkoani Tanga ambao ni Fatma Masanga mama yake mzazi karibu sana mama yetu, karibu sana, karibu sana ameambatana na kaka na dada zake Mheshimiwa Aweso.

Wageni saba wa Waheshimiwa Subira Mgalu (Mb) Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Zainabu Vulu na Mheshimiwa Hawa Mchafu ambao ni viongozi wa UWT kutoka Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Farida Mgomi karibu sana viongozi wa CWT Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Wageni 37 wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea (Mb) ambao ni wanakwawa wa kanisa la Wasabato Dovya kutoka Temeke jijini Dar es Salaam wakiongozwa na ndugu Deodatus Biranda karibu sana mmependeza kweli kweli eeeh! Mmmh! Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Daniel Mtuka ambao n wafanyakazi wa *Policy Forum* kutoka jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Meneja wao Ndugu Nicholas Lekule mko wapi Waheshimiwa wageni wetu karibuni sana.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Mbeya, wakiongozwa na Askofu Enock Kapuguso. Karibu sana, *(Makofi)*

Tunao wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo Watendaji watatu toka Taasisi ya *AMKA ARISE* ya Jijini Arusha ambao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi zake, Karibuni sana kwa mafunzo.

Wapo viongozi 10 wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Arusha, wakiongozwa na Ndugu John Mudanzi, karibuni sana.

Tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Jesca Kishoa ambaye ni mdogo wake anaitwa Lucy Njiku, karibu sana. (*Makofi*)

Matangazo mengine. Hili la *line* ya simu, nalirudia tu, lakini ni hao hao ambao nimewatangaza wako kwenye jukwaa la Spika. Mheshimiwa Venance Mwamoto, Balozi; anawaomba Wabunge wote, wanaoishi kwenye nyumba za Wakala wa Nyumba wa Serikali (*TBA*) mkutane leo mara baada ya shughuli za Bunge kuahirishwa saa 7.00. (*Makofi*)

Zoezi la utoaji chanjo ya ini Awamu ya Tatu na upimaji wa afya litakaloratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*).

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa niwatangazie kuwa Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya utaendelea na zoezi la utoaji wa chanjo ya Homa ya Ini kwa awamu ya tatu kuanzia leo tarehe 6 Mei hadi tarehe 17 Mei. Inasisitizwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopata chanjo kwa awamu ya kwanza na ya pili, mnaombwa mkamalize chanjo hiyo ya awamu ya tatu na ya mwisho.

Aidha, kutakuwa na zoezi la upimaji na ushauri wa afya litakaloratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* Dar es Salaam; na huduma zitakazotolewa ni kama ifuatavyo.

Upimaji wa magonjwa ya moyo, upimaji wa magonjwa ya saratani, uchunguzi wa mfumo wa mkojo, uchunguzi wa magonjwa ya akina mama, uchunguzi wa magonjwa ya ndani. Zoezi litafanyika Kituo cha Afya cha Bunge kuanzia leo tarehe 6 mwezi wa tano hadi tarehe 17 mwezi wa tano kila siku kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa 12.00 jioni na litawahusisha Waheshimiwa Wabunge, watumishi wa Bunge na familia zao. *(Makofi)*

Makamu Mwenyekiti wa Bunge *Sport Club* Mheshimiwa Esther Matiko, anatoa taarifa kwamba Jumamosi Bunge *Queens* ilicheza mechi na wakufunzi wa CHANETA. *Bunge Queens* ilifanikiwa kuwachakaza Wakufunzi wa CHANETA kwa magori 31 kwa 27, kitu kilichopelekewa Wakufunzi pamoja na kujua Sheria 15 za *Netball* kubaki mdomo wazi. Hee! Hongereni sana. *(Makofi)*

*Bunge Sport Club* inawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla waliojitokeza kwa wingi kwenye mchezo huo. *(Makofi)*

Hayo ndiyo ninayo hapa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 47.

**MWENYEKITI:** Unaiielewa?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Naam.

**MWENYEKITI:** Ina hatua ngapi?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ina hatua moja mbili, tatu, nne.

**MWENYEKITI:** Aah aah, ina hatua mbili tu. Hatua ya kwanza unaniomba kwa kifupi tu nipime kama ni dharura. Halafu nikiona ni dharura, ndiyo unaingia hatua ya pili, ndiyo wanakuunga mkono.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa hoja ya dharura kwamba, hivi karibuni katika nchi yetu kumekuwa na matukio ya mauaji, utekaji, na watu kupotea. Ninavyozungumza, juzi kuna kijana mmoja anaitwa Mduda Nyagari kule Mbozi, ametekwa akiwa nyumbani kwake mbele ya macho ya watu. Alivyojaribu kupiga kelele, wale watu walionesha silaha wakamkamata wakamweka kwenye buti ya gari. Tumekwenda kwenye Vituo vya Polisi, polisi wamesema sio wao, lakini wamekataa kufungua jalada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hajatekwa alikuwa ametoa ripoti polisi kwamba kuna watu walikuwa wanamtafuta, polisi bado walikataa kufungua jalada. Haya matukio ambayo ukiangalia huko nyuma, watu wengi wameyajadili hata kwenye hotuba ya Mambo ya Ndani, tulitaka Serikali iji-*commit* yamekuwa yakiendelea na mwendelezo mkubwa. Kwa mfano, aliwahi kutekwa Roma Mkatoliki Serikali haijatoa ripoti na wengine kadha wa kadha kama akina Nape, lakini Serikali haijafanya.

Sasa *trend* hii imekuwa ikiendelea na wajibu wa polisi na Serikali ni kulinda raia na mali zao. Naomba suala hili tulichukue kwa uzito wake kwa sababu watu wanapotea na Serikali haitoi majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ili jambo hili liweze kujadiliwa. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kuunga mkono  
hoja ya Mhe. Mch. Peter S. Msigwa)*

**MWENYEKITI:** Katika hatua hiyo hamuungi mkono. Eeh, ndiyo maana nimekusikiliza. Nimekuruhusu hiyo hatua ya kwanza. Kweli ni suala la dharura. Suala lolote linalohusu maisha ya Mtanzania, ni suala zito sana, lakini hiyo haimaanishi kwamba mtu anapotoweka; mimi hapa nina taarifa Jimboni kwangu kuna kijana mmoja aliondoka nyumbani kwake juzi, hajaonekana mpaka leo. Sasa haiwezekani mtu ameamua tu kwenda kwa shughuli zake halafu hakurejea...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ngoja, sikia, nafika huko. Eeh, vipi mbona mna mambo ya..., najaribu kuwasaidia. Sasa tuwe tunatofautisha sana.

Katika hili ambalo umesema na wananchi wameona na jitihada zikafanyika lakini bado maelezo yake hajanyooka vizuri, nadhani itakuwa vizuri hapa badala ya sisi kuanzisha mjadala ambao maudhui yake hatuyafahamu sana kama Wabunge, ni vyema tu Serikali ikatoa maelezo kama wanaweza sasa hivi, lakini kama hawawezi waji-*commit* baadaye watoe maelezo ili Watanzania wajue kuhusiana na hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba uridhie angalau tu kwa hatua ya awali, kwa sababu wakati mwingine yanapotokea mambo kama haya na Serikali ikakaa kimya, sidhani kama tunajitendea haki pia sisi Serikali ama wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hatua hii ya mwanzo tumruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani aweze kusema kitu kama anacho chochote cha

kusema kwa hatua hii ya awali, anaweza kuisemea Serikali.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kueleza masikitiko ya Serikali kutokana na matukio ya mbalimbali machache ya uhalifu ambayo yanatokea nchini, juu ya jitihada kubwa ya Serikali kupitia vyombo inayochukua, lakini kama ambavyo mnafahamu kwamba ndiyo maana vyombo hivi vipo kwa sababu ya *nature* na hulka ya binadamu kufanya uhalifu. Hata hivyo kwa kiasi kikubwa, niendeleo kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja hii mahsusi ambayo Mheshimiwa Msigwa ameizungumza, kwanza nataka nimsahihishe Mheshimiwa Msigwa, siyo vizuri kumwita Mheshimiwa Mbunge mwenzangu mwongo, lakini nimsahihishe na usahihi wa taarifa ambazo amezitungumza. Amesema kwamba huyo mtu ametekwa na vilevile polisi wamekataa kufungua jalada, kitu ambacho siyo sahihi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, usahihi wa taarifa ni kama ifuatavyo: Ni kweli mtu huyu hakuonekana, maana ukisema ametekwa, maana yake wewe unajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Msigwa amelithibitishia Bunge kwamba huyu mtu ametekwa, bila shaka yeye ana taarifa hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilielekeza Jeshi la Polisi, kwanza kabisa wamtafute Mheshimiwa Msigwa ili aisaidie Polisi. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Hilo la kwanza. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba mpaka sasa hivi tunapozungumza, Jeshi la Polisi limeshafungua Jalada. Siyo kweli kama ambavyo Mheshimiwa Msigwa amesema; na uchunguzi umeshaanza. Kwa kuwa suala hili tumelichukulia kwa uzito, tumeongeza hata nguvu kutoka Makao Makuu kwenda kufanya uchunguzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili tumelichukua kwa uzito, kama ambavyo matukio yoyote ya uhalifu yanapotokea nchini ikiwemo hata ullozungumza la wananchi wako, tutaendelea kulichukulia kwa uzito kama Serikali na pale ambapo tutabaini kwamba tukio hili limetokea kwa njia ya uhalifu, basi hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo hili, linataka kuchukuliwa kisiasa zaidi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...na kwa sababu pengine limemtokea mwanachama wa Chama fulani maelekezo mengine ambayo tunataka kuyatoa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*



**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...ni kwamba tunaendelea kuisitiza wananchi kutoa nafasi kwa Vyombo vya dola kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na desturi ya baadhi kwa wananchi, hususan vijana kutumia mitandao ya kijamii vibaya, kuichafua Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe wito kwa vijana hao kuwa waangalifu. Jeshi la Polisi liendeleo vilevile kuwatafuta na kuwahoji wale wote ambao wanasambaza taarifa za kuichafua Serikali kwenye mitandao ili na wenyewe wakaisaidie polisi. Hilo la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu na la mwisho ni kwamba kwa sababu mazingira ya mtu huyu kupotea yanatatanisha; na ndiyo maana mpaka tunapozungumza sasa hivi, hakuna mtu yeyote ambaye amekwenda Polisi kueleza...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...kwamba huyu mtu alishuhudia kuna watu sijui wamemteka na risasi na kadhalika, milango iko wazi kwenye Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi lianze kuwatafuta watu walio karibu vilevile na mhusika ili waweze kuwahoji, wao watakuwa wanajua vizuri nyendo zake, isije ikawa ni jambo ambalo limefanyika katika mazingira ya kutaka kuipaka matope Serikali. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili Serikali imelichukulia kwa mapana yote...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...na pale ambapo uchunguzi utakamilika, tutatoa taarifa rasmi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu tuheshimiane.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** *Just shut-up please.*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nimesema kaa chini.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Niambie kuhusu utaratibu, mimi nimekiuka nini? Mimi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, sio wewe, aliyekuwa anazungumza, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiuka.

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Kaa chini Mheshimiwa. Kaa chini *please*.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nawaombeni sana, sisi ni Viongozi wa ngazi ya juu sana kwenye Taifa hili. Kwa kipindi hiki, hata kama huridhiki na maelezo ya upande wa Serikali, tuna taratibu zetu. Huwezi ukatoa *judgment*, yaani ukahukumu pale pale kwamba anachokisema Mheshimiwa kwamba hakifai. *(Makofi)*

Yawezekana katumia maneno fulani ambayo wewe hukubaliani nayo, lakini hoja ya msingi aliyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ni kwamba Serikali inalifanyia kazi suala hili tena kwa karibu. Wanaomba sana, kama kuna mwananchi yeyote tukiwepo na sisi kama tunaweza tuisaidiea Polisi kwa suala hili. Hicho hicho anachosema. Mlango uko wazi.

Hatuwezi kuruhusu mazingira ya watu wetu wanatoweka tu na vyombo vya ulinzi na usalama vipo. Mimi nasema tuiachie Serikali kama walivyoahidi wayafanye haya kwa haraka, lakini itapendeza hili suala lisitokomee tu, eeh, waje watuambie *progress* ya suala hili imekaa vipi? Eeeh. mimi nadhani tukienda hivyo tutakuwa tumekaa vizuri. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na mjadala wetu. Nina orodha hapa kutoka Kambi zetu humu Bungeni. Tunaanza na wafuatao, tutaendelea hivyo baadaye. Tunaanza na Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kafumu na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla ajiandae.

Mheshimiwa *Engineer* Chiza.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hii ambayo nami niliwahi kuitumikia kwa kuleta hotuba nzuri ambayo inatuelekeza tuchukue mwelekeo gani ili kuweza kuwafikishia wananchi wetu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua bado ziko changamoto nyingi, najua yako malengo mengi ambayo hatujayafikia, lakini hatuwezi kuyafikia bila kuwa na utaratibu ambao tumejiwekea. Kwa sababu hii, naanza moja kwa moja kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hata kama sijaunga mkono, haitatusaidia sisi kueleza ule upungufu ili akaufanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono kabisa kwa asilimia mia moja ili niweze kusema mambo yangu sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa sababu kwa nyakati tofauti Waheshimiwa hawa wamefika katika Wilaya yangu ya Kakonko, wakakagua miradi ya maji ambayo ni kero kubwa, miradi ambayo haijakamilika tangu miaka karibu kumi iliyopita na kwa nyakati tofauti wakatoa maelekezo ni hatua gani zifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua nimepitia kwenye kitabu hiki, nimekuja leo tu, sikuwepo kwa muda mrefu kwa sababu zisizozuilika, baadhi ya mambo nimeona yametekelezwa, lakini yako mengine ambayo hayakutekelezwa; na hayo ndiyo nataka angalau nizungumze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri mara kadhaa anapojibu maswali anasema vizuri sana kwamba maji ni uhai, maji hayana mbadala na huo ni ukweli. Mahali ambako hakuna maji hakuna uhai, hata watu wanaokwenda mwezini huko au katika sayari zingine wanaridhika kabisa kwamba kule hawajaona maji na kwa kuwa hakuna maji hata viumbe hai havionekani. Kwa hiyo Mheshimiwa Aweso anachosema ni kweli kabisa kwamba maji hayana mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sera yetu ya Maji, nakumbuka vizuri nadhani ilikuwa mwaka 2002 na mimi nilishiriki, tulikwenda mpaka Zimbabwe mpaka South Afrika tukajiwekea malengo kwamba ifikapo Mei, 2010 upatikanaji wa maji mijini miaka ile ungekuwa asilimia 90, upatikanaji wa maji vijijini mwaka ule ungekuwa asilimia 65. Najua bado ziko changamoto nyingi, kila unapokwenda sasa hivi kilio ni maji, maji, maji. Upatikanaji wa maji Wabunge wengi wamezungumza, mimi sikuwepo lakini nilikuwa nafuatilia angalau kwa vyombo vya habari, upatikanaji wa maji bado hatujafikia malengo, bado hali ni tete. Kwa mfano katika Halmashauri ya Kakonko, idadi ya vituo vya maji ni 576, vituo visivyofanya kazi 283, ukokotoaji wa upatikanaji wa maji inasemekana ni asilimia 52 au 53 kulingana na taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nafuatilia wakati mwingine huu ukokotoaji wa upatikanaji wa maji na naomba Mheshimiwa Waziri nimefuatilia nikagundua wakati mwingine ukokotoaji hauendani na hali halisi, kwa sababu kwa mfano nilimuuliza Mhandisi mmoja unakokotoaje upatikanaji wa maji ukapata *percentage*? Akaniambia naangalia visima vilivyopo huenda vinafanya kazi au havifanyi kazi yeye anahesabu visima vilivyopo. Anaangalia kisima kimoja kinatoa maji kiasi gani, *per capita onsumption* ya maji vijijini na mijini ni kiasi gani? Sasa yeye anajumlisha anasema upatikanaji wa maji kulingana na visima vya maji vilivyopo kulingana na vyanzo vya maji ni huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba lisahihishwe kwa sababu huo si ukokotoaji halisi, huo ni ukokotoaji ambao

unajumuisha vyanzo vinavyotoa maji, vyanzo vya maji ambavyo miradi bado haijaanza kufanya kazi au imekamilishwa lakini haitoi maji, lakini akikokotoa anasema tumepata asilimia kadhaa. Haitusaidii sana kwenda namna hii, ni bora kabisa kwenda na hali halisi ili tunapokuja sasa kuiomba Serikali twende tukiwa na takwimu halisi, ni afadhali tuwe na miradi michache inayotekelezwa mara moja na kutoa maji, halafu tukimaliza tunahamia kwenye miradi mingine kidogo kidogo hivyo kuliko kujiwekea malengo au takwimu ambazo hazitoi hali halisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri upatikanaji wa maji katika Wilaya yangu ya Kakonko bado sidhani kama ni asilimia hii. Mheshimiwa Waziri alipokuja mwenyewe nilimpeleka akaona alitembelea baadhi ya miradi akaona mahali ambako miradi mingine walimwambia imetekelezwa kumbe iko asilimia tano, pale Kakonko Mjini aliona mwenyewe, tulikwenda katika miradi mingine Gwijima, tukaenda Kiduduye, Miradi ya Muhange, Katonga, Kiga, Gwalungu, Nyeguye, yote hiyo ama haifanyi kazi au imetekelezwa kwa kiwango ambacho hakistahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ziko wazi kwa nini baadhi ya miradi haitekelezwi vizuri. Naomba ku-*declare interest* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC, nimepata nafasi kupitia miradi mingi hasa ya ujenzi, barabara, shule, maji, changamoto kubwa ambazo niliziona na hizi ndizo nataka niziseme halafu niketi, lakini Mheshimiwa Waziri azifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo nimeiona katika miradi yetu ya maji, Mheshimiwa Waziri amesema tuna uwezo wa kitaasisi katika mikoa, katika mabonde ya maji na katika halmashauri na nimesoma katika kitabu chake ukurasa nadhani wa 12, lakini hali halisi kwa kweli bado bado hasa katika halmashauri, bado uwezo wa kitaasisi ni mdogo na uwezo huu naupima. Mimi nimekuwa katika Kamati ya LAAC tunachokifanya, tunatazama kwanza taarifa za CAG, halafu tuna- *single out* miradi fulani Fulani, unaikagua. Tulichokibaini na wenzangu akina Mheshimiwa

Mwalongo na Waheshimiwa wengine bila shaka watakubaliana na mimi, tulichokibaini ni uwezo mdogo kwanza katika mchakato mzima wa kutoa zabuni hizi, zabuni hizi zinatolewa kwa wakandarasi, baadhi ya wakandarasi wasio na sifa hawana...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Chiza kwa ushauri wako, mengine unaweza ukamalizia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Dkt. Kafumu, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla na Mheshimiwa Margaret Sitta ajiandae.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo hoja hii ya Maji. Namshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii kwa sababu ni Mungu pekee anayetupa haya yote. Naishukuru Serikali sana kwa kuliangalia jambo la maji na hasa katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Simiyu na mikoa mingine kame kwa kutuletea maji ya Ziwa Victoria, ahsante sana Serikali kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Igunga tumekuwa na tatizo la maji la siku nyingi kwa sababu ni wilaya kame, lakini wametuletea mradi huu ambao kwa kweli utatusaidia sana. Mradi huu utafikia kwenye Jimbo la Igunga kata kama sita hivi ambazo ni Kata ya Nanga, Mwamashiga, Bukoko, Itumba, Mbutu na Itunduru. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuangalia hali ya maji katika jimbo letu.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema Wabunge waliotangulia kuna miradi mingi sana ambayo imetekelezwa, ilitekelezwa ikafikia kiwango cha kufanya kazi, lakini ikatelekezwa ama kwa sababu chanzo cha maji hakikupatikana ama miundombinu haikujengwa vizuri. Kuna

mfano wa Mradi wa Maji Kata ya Itunduru, kule Jimbo la Igunga, mradi huu ulijengwa mwaka 2010. Miundombinu ya kupeleka maji kwenye kata hiyo na hasa Makao Makuu ya Kata ilijengwa vizuri ikiwepo *tank* pamoja na mabomba lakini chanzo cha maji kilikosekana, hata hivyo, mkandarasi alilipwa akaondoka. Wananchi tangu wakati huo leo mwaka wa kumi wanailalamikia Serikali mmetutengenezea mradi tunaangalia tu mabomba tunaangalia *tank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsumbua sana Waziri wa Maji juu ya jambo hili na naomba niliseme tena, naomba Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza Mradi wa Ziwa Victoria atupelekee maji pale ni kuunganisha tu na tumepeleka hata *design* pamoja na bajeti ni shilingi milioni 100 tu, ukitoa hizo unaweza ukafanya *adjustment* na mradi wetu ukapata maji, sio mbali sana kutoka bomba kuu la maji. Wananchi wa Itunduru wataishukuru sana Serikali, watafurahi sana na kwa kweli wataipenda Serikali yao, tafadhali sana namwomba Mheshimiwa Waziri anisikilize juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mambo mengi ya kusema sana, lakini naomba niseme Wilaya ya Igunga kuna sehemu ambazo hakuna maji ya chini, kwa hiyo kuna vijiji ambavyo tumechimba maji tumepata na tumepewa katika bajeti hii baadhi ya vijiji kuchimba maji. Hata hivyo, sehemu zingine kata nyingi kama kata saba hizi ambazo hazifikiwi na huu Mradi wa Ziwa Victoria hazina maji ya chini, tunajenga vibwawa, tumejitahidi. Namshukuru sana Mheshimiwa aliyekuwa Mbunge kabla yangu mimi alisaidia sana kujenga mabwawa kwenye kila kijiji na hasa kata na mimi nimeendeleza jambo hilo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo. Naiomba Serikali, naomba sana Wizara, wanapoangalia maeneo ambayo yana matatizo ya maji sana kama mikoa ya kwetu ile ambayo ni kame, basi watusaidie kutoka kwenye Mfuko wa Maji kutusaidia kujenga haya mabwawa madogo madogo wakati tunasubiria usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria kwenda kwenye kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo la mwisho kuhusu Mfuko wa Maji. Najua Wabunge tumesema sana juu



ya jambo hilo kwamba tuwaongeze huo Mfuko ili upate fedha za kutosha kama ilivyo kwenye umeme. Tunasema umeme kwenda kila kijiji na kuna fedha kule *REA* tumeweza kabisa kabisa, sasa kwa nini tusiwe na *REA* ya maji ambayo ina uwezo wa kufanya na tuseme maji kila kijiji. Kwa wananchi wetu hili ni jambo kubwa na ni tatizo kubwa sana ambalo tukiweza kulitekeleza hili tutalitendea haki Taifa hili jambo zuri sana, tuweze kuwatua ndoo wananchi wetu, akinamama wa vijijini wanahitaji kutuliwa ndoo kichwani. Kwa hiyo mimi naomba pamoja na kelele ambazo zimepigwa mwanzoni mwanzoni hapa kuomba shilingi 50 ziongezwe, nasema tu kwamba ni lazima tutafute vyanzo hata kama sio shilingi 50, basi tutafute vyanzo ambavyo tutatunisha huu Mfuko uweze kuwahudumia wananchi wetu. Serikali wakilifanya hili la maji vijijini watafanya kazi nzuri sana na wananchi watafurahi sana na wataipenda Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema, ukokotoaji wa *percentage* ya *coverage* ya maji kwenye vijiji haufanywi vizuri, Wabunge wengi wamesema na ndugu yangu, kaka yangu Chiza amesema. Kule kwetu Mwamashimba kule, Mwamakona, Mwanyalali kule na sehemu zote zile ambazo ni mbuga ambako ni ziwani hakuna maji chini, unaona *calculation* anasema maji asilimia 30. Kweli ukienda kule unakuta visima havina maji vyote au unakuta hakuna kisima kuna kibwawa kimoja kinachokauka lakini asilimia 30 *coverage*, wanafanyafanyaje?

Naiomba Serikali kwenye jambo hili wafanye *evaluation* ya nchi nzima tena upya ili tuweze kupata *percentage* ya *coverage* ya maji inayolingana na ukweli na tukiweza kufanya hivyo tunaweza kutafuta fedha kwa sababu tutajua *gravity* ya tatizo lenyewe, lakini kwa jinsi hii tunaonekana kama vile maji tumepiga hatua, lakini tuna hali mbaya sana kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba niishukuru Serikali tena kwa Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda Nzega, Igunga na Tabora na Katibu Mkuu aliniambia

wanaweza kufikisha hata kwenye jimbo la jirani la ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu pale Shelui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. Mungu awabariki sana, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Daktari Kafumu kwa mchango wako Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kushukuru kipekee kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wote ambao walikuja kuniona nilipokuwa nimelazwa pale Hospitali ya Muhimbili, nasema ahsante sana wote mliokuja na ambao hamkuja wote mlifanya kazi moja ya kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu ambayo ninataka kuchangia ni Mradi wa Matamba na Kinyika, Wilaya ya Makete ambao Wizara imeandika barua ya kwamba kupewa *no objection*. Mpaka sasa hivi hatujapewa *no objection* na mradi huu ni wa bilioni 4.6, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akaupa *no objection* mradi huu ili mambo yaende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni wa Bulongwa ambao unajumuisha Bulongwa, Iniho, Kapagalo, Usililo, nayo ni umeshakamilika unahitaji milioni 264, lakini huyu mtu amemaliza kufanya kazi hiyo, fedha hajapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mwingine ni Mradi wa Lupalilo- Tandala ambapo zinahitajika milioni 161, mpaka sasa hivi bado hajapewa, naomba sana Mheshimiwa Waziri ukumbuke kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mwingine ni Mradi wa Igumbilo ambao ni milioni 308 zinahitajika ili ziweze kutekeleza mradi huo, naomba sana sana Wizara iweze kutoa fedha hizo ili mradi uweze kutekelezeka. Zaidi ya hapo nipongeze

sana sana Serikali ya CCM, Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa, Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwezesha miradi hii kutekelezeka. Mungu awabariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa kwa mchango wako mzuri na kwa kuzingatia muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Bura na Mheshimiwa Edward Mwalongo ajjandae

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mezani. La kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, lakini la pili nawashukuru sana wananchi wa Urambo kwa kunipa ushirikiano wakati wote, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kuishukuru Wizara ya Maji ikiongozwa na Profesa Mbarawa, Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu Profesa Mkumbo, Naibu wake na watendaji wote kwa kweli kazi wanachapa, nawatakia kila la heri waendeleo kuchapa kazi, kazi wanaiweza, kitu kikubwa ni kuwezesha kifedha tu. Ni uhakika usiopingika kwamba chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kazi inafanyika katika Wizara ya Maji, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa niaba ya wananchi wa Urambo nichukue nafasi hii kushukuru sana Wizara kwa kutuwezesha sisi watu wa Urambo kuingizwa katika Mradi wa Maji kutoka Lake Victoria. Nawashukuru sana sana kwa sababu tulikwenda sisi kwenye Mto Malagarasi tukaona umbali ulioko kutoka Malagarasi mpaka Urambo halafu pia na mwinuko wa nchi, kwa kweli tunashukuru kwamba tunapata maji kutoka Lake Victoria kwa sababu ni kilomita 90 tu kutoka Tabora, tunashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali moja tu ambalo ningepomba wanijibu kwa niaba ya wananchi wa Urambo wakati wa kuhitimisha ni kwamba, sasa huu mradi wa maji

kutoka Lake Victoria ni wa mwaka gani wa fedha ili na sisi tuishi kwa matumaini. Kwa hiyo tutashukuru sana kujua ni lini tunapata maji kutoka *Lake Victoria*, mwaka gani wa fedha. Kwa kuwa Urambo kuna shida kubwa sana ya maji kwa kweli nikiulizwa wakati wowote kipaumbele au shida kubwa inayowakabili wananchi wa Urambo; la kwanza nitasema maji kwa sababu sisi *water table* imeshuka, yaani maji yameshuka chini sana kwa hiyo ni vigumu kupata maji na hakuna njia nyingine ambayo inaweza kutuwezesha kupata maji kipindi hiki ambako tunasubiri Mradi wa kutoka *Lake Victoria* isipokuwa visima. Kwa hiyo naomba sana Wizara ya Fedha izingatie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2018/2019 tulitengewa fedha kama shilingi milioni 620 kwa ajili ya kujenga visima 30 katika vijiji, tunaomba Wizara mtuwezeshe hilo kwa sababu naanza kutetemeka kidogo kwa kuwa sasa hivi tayari tuko mwezi Mei na bado fedha hazijatoka. Uzuri wetu sisi watu wa Urambo, tuliipa Wakala wa Serikali (*DDCA*) kazi hii ya kuchimba visima. Kwa hiyo, tutashukuru tukipata hiyo shilingi milioni 620 ili *DCCA* iweze kuchimba visima 30 kwenye vijiji wananchi waweze kupata maji wakati tunasubiri mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo mjini Urambo kuna shida ya maji sana na mtandao mzima wa maji una changamoto. Katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, tuliomba na tukaahidiwa kupata shilingi milioni 429 ili tuchimbe visima Mjini Urambo lakini pia tuweze kurekebisha miundombinu. Tutashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla mkitupa fedha hizo ili tuweze kupata maji kwa njia ya visima wakati tukisubiri mradi mkubwa kutoka Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmojawapo kati ya watu waliopata bahati kwenda Bermuda ambacho ni Kisiwa America Kusini. Jambo ambalo nilijifunza, naomba niliseme hapa, wao wamegundua kwamba nchi yao hawawezi kupata maji mazuri, wakajiwekea wenyewe katika sheria yao kwamba yeyote anayeomba kibali cha kujenga, kwanza

wanakagua kama ameweka miundombinu wa kuvuna maji. Mimi niliona ni jambo zuri sana lakini kwetu sisi kwa sababu bado halijawekwa katika sheria na utaratibu wa ujenzi kwamba lazima mtu anapojenga nyumba aweke miundombinu ya kuvuna maji, mimi ningeomba ianzie na shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu nyingi sehemu wanazojengwa maji huwa ni haba, kwa hiyo, utakuta watoto barabarani wanatembea na chupa na vidumu vya maji. Niiombe Serikali kwa sababu ni moja wakashirikiana Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI kuona waweke sharti gani kwa watu wanaojenga shule ili miundombinu ya kukusanya maji iwepo. Mimi nasema inawezekana, kwa sababu bila maji ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kushirikiana na Mheshimiwa Spika tumeendesha zoezi zuri sana la uchangiaji wa vyoo ili watoto wa kike wapate vyoo vya kuwahifadhi. Pia katika ramani ile ambayo tulipendekeza, inaonesha lazima kuwe na maji na njia pekee ambayo inaweza kutuhakikishia upatikanaji wa maji ni kuweka miundombinu ya ukusanyaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono Kamati ya Kilimo, Uvuvi na Maji ambayo kwenye kitabu chake ukurasa 20, wamependekeza kwamba Serikali itilie mkazo suala la uvunaji wa maji ya mvua. Kwa hiyo, ni suala tu la kuongea na sekta husika ili tuone kama wanaweza kuweka kiwe ni kipengele kimojawapo kwamba kabla shule haijafunguliwa au haijajengwa lazima kuwe na ramani ya utaratibu wa ukusanyaji wa maji shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, naomba nichomekee hapo hapo, kama wataweka sharti mojawapo la ujenzi wa shule kwamba kuwe na miundombinu ya kuvuna maji, pia naomba nipendekeze kwamba kuwe na utaratibu kwamba kabla shule haijakaguliwa au inapokaguliwa la kwanza kuangaliwa ni suala la vyoo ambapo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza ramani nzuri ambayo

inawahifadhi watoto wa kike, watoto wenye ulemavu na watoto wote kwa ujumla. Kwa kweli vyoo na maji iwe kama ni sharti mojawapo la kwanza la kuzingatiwa kabla shule haijajegwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji halina ubishi, sisi wanawake ndiyo tunahitaji sana maji kwa sababu baba anapokuja nyumbani anategemea akute maji. Kwa hiyo, nashukuru sana kwamba Wabunge wote tumeungana kuiomba Serikali ione utaratibu ambao unaweza kuiwezesha kupata fedha kutuwezesha sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla kupata maji katika maeneo yetu jambo ambalo litakuwa ni ukombozi. Sisi wote tunasema mtu ni afya lakini huwezi kuwa na afya bila kuwa na maji kwa sababu maji hayana mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo kwa kuishukuru tena Serikali kwa kutuwezesha sisi watu wa Urambo kuingizwa katika Mradi wa Maji kutoka *Lake Victoria* kama inavyooneshwa kwenye ukurasa wa 88 wa kitabu hiki halafu pia imerudiwa kwenye ukurasa wa 148 kwamba tutapata maji kutoka *Lake Victoria*. Tunawashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Urambo na tunaomba tu Mheshimiwa Waziri mtakapokuja kujibu hapa basi mtupe matumaini lini tunapata maji kutoka *Lake Victoria* kama ukombozi wa kudumu au suluhisho la kudumu la upatikanaji wa maji katika Wilaya yetu ya Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Sitta kwa mchango wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mwalongo na Mheshimiwa Shaaban Shekilindi wajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge

Iako Tukufu lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na kwa neema yake aliyotupatia siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa shughuli za maendeleo zinazofanyika kwa mkoa wetu na nashukuru kwamba inawajali wananchi wake. Jiji la Dodoma linakua kwa kasi sana na watu wanaongezeka kwa wingi sana na kwa hiyo mahitaji ya maji ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya pembezoni kama Mpunguzi, Mtumba na maeneo mengine hawajapata maji kwa sababu mtandao unaohitajika kule unahitaji fedha nyingi. Sisi kama Jiji tumeomba shilingi milioni 800 kupitia Shirika letu la Maji la *DUWASA* ili waweze kuchimba visima vya maji katika maeneo ya pembezoni ili viwanda vitakavyojengwa maeneo hayo na ofisi zitakazofunguliwa wasipate shida ya maji. Kwa hiyo, tumeomba shilingi milioni 800 kwa ajili kuongeza visima kwa maeneo ya pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka takribani nane au kumi na kila mwaka suala la Bwawa la Farkwa (bwawa la mkakati) linazungumzwa katika bajeti ya Waziri wa Maji na hatuoni jambo linaloendelea katika uchimbaji wa bwawa hili la mkakati. Bwawa hili kama alivyosema Waziri mwenyewe litawasaidia wakazi wa Jiji la Dodoma, Wilaya ya Chemba na Bahi na hasa wakazi wa Bahi ambao ni wakulima wazuri wa mpunga na wakulima hawa wanalisha Jiji la Dodoma na Mkoa wa Singida. Mwaka huu hatuna mchele kwa sababu mvua haikunyesha na bwawa lile halijachimbwa na kila mwaka tunaambiwa ni bwawa la mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa ifike wakati bwawa hili lichimbwe liweze kuwasaidia wananchi wa Chemba, Jiji la Dodoma na Bahi. Nia ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kumtua mama ndoo kichwani na wananchi ambao mradi huu utapita katika maeneo yao wanahitaji mkubwa wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie sasa mradi wa Ntomoko. Mradi huu ni wa miaka mingi sana na ni maporomoko ambayo yana maji ya kutosha. *DUWASA* ambao wamepewa kazi ya kutengeneza miundombinu na kufufua miundombinu iliyochakaa, wameomba shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuanza uchimbaji na kutengeneza mradi huu wa Ntomoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ntomoko wamesubiri vya kutosha, wamesubiri miaka na mimi katika Ubunge wangu nimesimama katika Bunge hili mara nyingi nikiomba wananchi wa Ntomoko wapewe maji. Vile vijiji 12 vinavyozunguka mradi huu wa Ntomoko, maji hayajapatikana mpaka leo. Waliohujumu mradi huu na wako mahakamani, lakini kuwepo kwao mahakamani hakumfanyi mwananchi akapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Serikali yangu sikivu, wananchi wa pale wapewe maji, wananchi wa Ntomoko wanaona maji yanabubujika pale lakini hawajawahi kupata maji. Nashauri wachimbiwe kisima basi wapate maji kupitia kisima kwa sababu wao hawakula fedha za mradi, waliokula fedha za mradi wanajulikana, kwa nini wasipate maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 52 Serikali imesema kwamba vijiji 11 vinavyozunguka mradi huu watapata maji kupitia mradi mkubwa wa bwawa linalotarajiwa kuchimbwa, bwawa hili linachimbwa katika kata gani? Naomba Mheshimiwa Waziri ukija kujibu uniambie bwawa hili linachimbwa katika kata gani na kijiji gani ili hata Mbunge wa Chemba au mimi mwenyewe nitakapokwenda niwaambie wananchi kwamba vuteni subira, bwawa linakuja kuchimbwa hapa katika kijiji Fulani. Hata bajeti, anasema katika mwaka wa fedha 2019/2020, sijaona fedha zilizotengwa kwa ajili ya uchimbaji au usanifu wa bwawa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kule kwenye Bwawa la Farkwa kusema kwamba, hata wananchi wa kule Farkwa hawajalipwa fidia. Unasemaje kwamba mradi wa mkakati



wakati wananchi hawajalipwa fidia? Niombe wananchi wa Mombosee na Bubutole walipwe fidia ili mradi utakapoanza basi kusiwepo na tatizo lolote la wananchi kudai fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi Ntomoko, naomba wananchi wale wakumbukwe walichimbiwe hata kisima. Wananchi wa Ntomoko, Fai na vile vijiji 11 kama nilivyosema Waziri atuambie kwamba bwawa hili linachimbwa katika kata ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie suala la maji kule Kondoa. Kondoa tumepewa shilingi bilioni 4 kwa ajili ya visima, visima vimechimbwa, maji yako ardhini lakini hakuna miundombinu. Kwa hiyo, ukimwambia mwananchi kwamba kisima kimechimbwa inawezekana aliona gari likichimba kisima pale lakini, je, maji anayo? Mwananchi anachotaka ni maji, basi tuwajengee miundombinu wapate maji wale wananchi wa Kondoa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo liko Chilonwa, Wilaya ya Chamwino, visima 12 vimechimbwa maji yapo tena virefu lakini hakuna miundombinu. Kwa hiyo, wanawake bado wanahangaika kilometa 10, 15 kwa ajili ya kutafuta maji. Tunajua Mkoa wa Dodoma ni kame, hakuna maji, maji lazima yatafutwe ardhini. Niombe sana Serikali yetu sikivu maeneo ambayo maji yamekwishachimbwa na yapo sasa miundombinu itengenezwe ili wananchi wapate maji, wanawake na watoto wafanye shughuli zingine waondokane na tatizo la kuamka saa kumi usiku na kuacha shughuli za nyumbani wakienda kutafuta maji. Vijiji vya Deti, Zajilwa, Itiso, Segala, Dabalo, Chilonwa, Nsamalo na Manchali visima vipo na viko visima nane vilivyochimbwa mwaka huu maji yapo lakini hakuna miundombinu na fedha tumeomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvunaji wa maji limezungumzwa na Wabunge wengi, naomba sasa Serikali yetu kama hatuna uwezo wa kuchimba visima na kutoa maji maeneo ya mbali kwa ajili ya kuwasaidi wananchi wetu, basi Taasisi za Serikali, shule za msingi, shule za sekondari, zahanati, vituo vya afya, tujenge miundombinu ya kuvuna maji ya

mvua. Inawezekana kabisa kero ya maji kwa wananchi wetu ikapungua. Naomba Serikali iweke mkakati huo na uvunaji wa maji hauchukui fedha nyingi na Mheshimiwa Waziri na Serikali inajua. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bura kwa mchango wako.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwalongo, Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Mendrad Kigola wajiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Maji ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitoe pongezi nyingi sana kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayofanya. Nikisema juu ya Mheshimiwa wetu Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, alifanya ziara katika Mkoa wa Njombe na pale Njombe Mjini alituahidi kwamba kuanzia Septamba mkandarasi atakuwepo *site* kwa ajili ya maji ya Mji wa Njombe. Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri na wewe mwenyewe ulithibitisha mbele ya Mheshimiwa Rais kwamba mkandarasi atakuwepo Njombe kwa ajili ya mradi wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana jambo hilo litekelezwe kwa sababu Mji wa Njombe unakua kwa kasi na una shida kubwa sana ya maji. Kwa kuwa shida ile ni kubwa na shida yenyewe inasikitisha kwa sababu Njombe kila bonde lina maji ya mwaka mzima sasa tunapokuwa na mji hauna

maji na mabondeni kuna maji o hapo masikitiko yanaongezeka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wetu wa Wizara ya Maji kwa maana ya Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Maji tunawapongeza sana. Wanafanya kazi nzuri, ni wasikivu na wanachukua hatua pale tu ambapo tunakuwa tumeshawaeleza matatizo yaliyopo katika Majimbo yetu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Njombe, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri umeingilia Mradi wa Igongwi ambao unaleta shida sana katika Jimbo la Njombe Mjini na nakushukuru sana kwa sababu kasi inakwenda vizuri. Niwaombe wenzangu kule Jimboni, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, Mhandisi wa Maji na Mwenyekiti wangu wa Halmashauri wafanye haraka kadri ya maelekezo yako ili kusudi tuweze kumruhusu tena mkandarasi wa *Lot One* ya Igongwi ili vijiji vinavyoangukia katika mradi huo viweze kupata maji ambavyo Vijiji vya Uwemba, Njomlole, Luponde pamoja na Kitulila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Njombe kiko kijiji kinaitwa Lugenge katika Kata ya Lugenge, kina mradi ambao umekadiriwa kusaidia zaidi ya vijiji sita. Mradi huu ulikuwa ni wa miezi tisa lakini mpaka hivi tunavyoongea una miaka saba haujakamilika. Mheshimiwa Naibu Waziri unakumbuka tulifika katika kile kijiji na tuliona ule mradi, mkandarasi alituahidi kwamba ndani ya miezi mitatu atakuwa amefikisha maji kwenye tenki hadi dakika hii ninavyoongea mkandarasi yule hajamudu kazi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mtusaidie wananchi wa Lugenge wapate maji. Miundombinu ya usambazaji na matenki ya Vijiji vya Lugenge, Kiyaula, Kisilo, Ihalula na Otalingolo yalishakamilika lakini miundombinu ya kuleta maji kutoka kwenye chanzo mpaka leo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya tatizo kubwa tunalopata kwenye miradi ya maji, kadri nionavyo mimi hatuna mipango kwa maana ya Halmashauri kuwa na mpango wa maji wa Halmashauri kwamba tunatekeleza mradi upi, kwa ajili ya kijiji kipi, kwa gharama zipi na tukimaliza huu tunaenda upi. Niombe sana sasa Wizara itoe hayo maelekezo kwamba kila Halmashauri sasa iwe na mpango kwa maana kwamba kuwe na usanifu wa kila kijiji ili kuwezesha vijiji viweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Njombe Mjini kuna Vijiji kama Mtila, Lusitu, Idihani, Idunda, lhanganga, Uliwa, havina dalili kabisa ya kupata maji ya bomba. Niombe sana Serikali isaidie kutoa maelekezo kwa Halmashauri kusudi vijiji hivi vifanyiwe usanifu, viwekewe mipango ya maji ili tujue kabisa kwamba katika utekelezaji wa mipango yetu ya maji vijijini ni lini itatekelezwa na kwa gharama zipi ili kusudi tunapowaeleza wananchi kwamba tuna jitihada ya kuleta maji hapa, wawe wanafahamu kwamba ni kweli jitihada ya kuleta maji inafanyika kuliko unasema kwamba una jitihada ya kuleta maji lakini hata usanifu haujafanywa, haijulikani ni lini maji yatapelekwa mahali hapo na ni nani atafanya kazi hiyo. Niombe sana jambo hilo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalalamika sana juu ya miradi ya maji lakini tatizo kubwa ambalo tunaliona sisi kama wawakilishi wa wananchi na hasa hasa katika Jimbo langu la Njombe Mjini ni tatizo la usanifu. Unaona kabisa kwamba usanifu umefanyika hasa hasa ile miradi ya vijiji 10, mimi katika Jimbo langu kuna mradi wa Vijiji vya Ngalinga na Utengule, usanifu umefanyika katika mazingira ambayo hayana maji na mkandarasi amepewa kazi ya kutekeleza ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naye katika utekelezaji wake anatekeleza kwa viwango vya chini sana. Anaweka mabomba ambayo hayawezi kuhimili *pressure*, unajiuliza ni nani hapa mwenye mapungufu, ni Mhandisi wa Maji wa Halmashauri, ni msanifu aliyesanifu mradi au mkandarasi? Hakuna teknolojia rahisi kama ya maji, inabidi

wataalam wetu huko Wizara ya Maji watafakari na wajiulize kwamba ni kweli wanastahili kuendelea kutoa huduma katika Wizara hiyo? Kwa sababu haiwezekani teknolojia rahisi inashindwa kutoa huduma. Hivi kama leo tungefanya mabadiliko tukasema Wizara ya Maji ndiyo iwe Wizara ya Ujenzi, ina maana madaraja yangebomoka siku ya pili yake, barabara zingebomoka siku ya tatu yake, tungekuwa hatuna huduma kabisa. Teknolojia rahisi kama ya maji tunashindwa kweli kusafirisha maji yawafikie wananchi na tunaona Serikali inatoa fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, wataalam wa Wizara ya Maji wakishirikiana na Wahandisi wa Wizara ya Maji walale kwenye taaluma zao, wafanye kazi kitaalam. Sisi ni wanasiasa lakini tunafika mahali tunaona kabisa kwamba usanifu uliofanywa siyo sahihi kabisa lakini wao kwa vigezo vyao vya utalaam wanasema hivi ndiyo inavyotakiwa, kwa kweli inasikitisha sana. Mimi najua kabisa Waziri, Naibu Waziri na Katibu wetu Mkuu mko makini sana, hebu waangalieni hawa wataalam, kweli wana moyo wa dhati wa kuwasaidia Watanzania wapate maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunalo tatizo sana la watengenezaji wa vifaa vya mabomba. Watengenezaji wa vifaa vya mabomba wamekuwa wakiingia katika mitego ya gharama wakishirikiana na Maafisa Manunuzi katika maeneo mengine lakini wakati mwingine wanaingia kwenye mitego ya gharama wakishirikiana na wakandarasi. Mkandarasi *BOQ* inamuambia bomba labda la PN9 lakini kwa sababu bomba la PN9 ni la gharama kwa hiyo mkandarasi anaongea na mwenye kiwanda, mwenye kiwanda yuko tayari kugonga muhuri wa PN9 kwenye bomba la PN6 ama PN5 matokeo yake ule mradi unakuwa unavujisha maji mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama tunavyosema kwamba tujali viwanda vya ndani, naomba Serikali na sisi Wabunge tusimame pamoja tuwaambie wenzetu wanaotengeneza vifaa vya mabomba kama kweli wanataka tuendeleo kuwaunga mkono ili kusudi uzalishaji

wa vifaa vyao vya maji viweze kununuliwa na vitumike kwa wananchi basi wawe waaminifu, wakweli na wawe wanatengeneza vitu ambavyo ni imara kwa sababu haiwezekani Serikali itoe fedha nyingi wananchi hawapati huduma, yaani haiwezekani kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, inafika mahali wakati mwingine mkandarasi anakwambia kabisa ni bora nikaagiza bomba kutoka nje ya nchi ni nafuu kulliko kununua ndani. Kwa hiyo, ina maana sasa hata kumuunga mkono huyo mzalishaji binafsi haisaidii kitu. Kwa hiyo, niombe sana kama itawezekana kwenye upande wa usanifu, Serikali iangalie sana kwenye usanifu pamoja na *engineering cost* kwa sababu hapa mahali pawili ndipo ambapo wakandarasi pamoja na watu wa manunuzi pamoja na *consultants* wanacheza na gharama za miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mbinu ya pekee ambayo inaweza ikasaidia. Kama inawezekana kabisa, tunao wahandisi katika idara mbalimbali za Serikali, tunao wahandisi wa Jeshi wako Mzinga, wako Suma JKT, tuwe tunawashirikisha kuona hizi *engineers cost* ziko sahihi kweli kwa sababu bila kufanya hivyo tunamuachia mhandisi na mtu wa manunuzi wanaweka ile *engineers cost* matokeo yake mradi unakuwa na gharama kubwa halafu unakuwa hautekelezi lakini ukishaona kwamba mahali panapoingia nafsi ya ulafi maana yake hata ufanisi wa kazi unashuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalongo. Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Kigola na Mheshimiwa Mnyika wajiandae.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehemu ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuweza kuchangia Wizara hii ya maji. Pili, nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya hakika sisi hatuna cha kumlipa ila Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiyo atajua cha kumlipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru kwanza Waziri Mbarawa, Naibu wake Aweso, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya, kwakweli Watanzania wanaona kazi kubwa mnayoifanya. Endeeleni kufanya hivyo, naamini na Mungu atawasimamia na malengo tutayafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru kwa kupewa milioni 500 kwa ajili ya mradi wa Ngulu. Mradi ule umekamilika na sasa nimuombe Waziri au Naibu Waziri aende sasa kwenda kuufungua. Lakini sambamba na hayo, nimepewa milioni 770 kwa ajili ya maji mjini, milioni 770 hizi zimepan giwa zijenge tenki la lita 650 ambalo tenki hilo liko sehemu ya Magamba na tenki lile linaendelea kujengwa mpaka sasa hivi, na banio la sehemu moja inaitwa Kindoi na banio hilo bado linaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwa kuwa kuna kata mbili ambazo ziko chini vyanzo vyake viko juu Lushoto basi nilimuomba Waziri baada ya kufika Waziri Mheshimiwa Prof. Mbarawa baada ya kufika Lushoto kuangalia hali ile halisi ilivyo. Basi nikamuomba kwamba pamoja na kujenga tenki hili, kulijenga, basi kuna banio linajengwa sehemu ya Kindoi niombe banio lile litolewe matoleo mawili kwa ajili ya kata mbili, kwa ajili ya Kata ya Ubiri na Kata ya Ngulwi.

Kwa hiyo, niombe Serikali yangu tukufu kwamba Mheshimiwa Waziri, naomba sasa unipangie fedha au unipe fedha kwa ajili ya kata zile ambazo nimeshazitaja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, hili tenki la lita 650 naishukuru sana Serikali lakini hakuna mabomba ambayo yanatakiwa kuanza kwenye chanzo kuja kwenye tenki na kutoka kwenye tenki, kwenda Lushoto mjini. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu sasa kwamba pamoja na kupata fedha hizi lakini bado hakuna fedha za miundombinu ya bomba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali yangu initengee fedha hizo ili tuweze kukamilisha miundombinu ya bomba. Sambamba na hayo, miundombinu ya bomba ambayo iko Lushoto Mjini ni ya zamani sana, ni ya tangu mkoloni. Bomba zile ni za chuma Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nikuombe sasa unitengee pesa nyingine kwa ajili ya kutoa miundombinu ile ya zamani ili tutoe miundombinu chakavu, tuweke miundombinu mipya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamoja na banio hilo niombe sasa kwamba nipate fedha kwa ajili ya kupeleka maeneo yale ambayo nimeyataja kata zile mbili ambazo ni Ubiri na Ngulwi maana nikikosa kwenye eneo hili basi ujue kabisa kwamba wale watu wa Ngulwi na Ubiri hawataweza kupata maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe tena, nikuombe Mheshimiwa Waziri kwamba kuna mradi mkubwa ambao umeshafanyiwa upembuzi yakinifu. Mradi huo unaitwa chanzo cha wanaitwa mstari namba tisa ambao uko Magamba. Chanzo kile kikienda kutekelezwa kitaenda kutatua tatizo la maji katika kata 12 ambazo kata hizo ni Kata ya Makanya, Mbwehi, Malibwi, Kwekanga, Kwahi, Migambo, Kilole, Gare, Ngwelo, Ubiri, Ngulwi pamoja na Kata na Kwemashao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua Lushoto, jiografia yake ni ya milima kwa hiyo vyanzo vya maji viko Lushoto. Sisi tumekosa miundombinu ya maji na maeneo haya ina maana yako mlimani, vyanzo viko mlimani, maeneo yako bondeni. Kwa hiyo, kwenye maeneo haya niliyotaja nikipata miradi miwili tu basi ina maana tunaenda kutatua tatizo



kubwa katika kata ile. Cha kushangaza na cha kusikitisha, wenzangu wanaongelea vijiji havina maji lakini mimi naongelea kata hazina maji, hebu angalia *distance* iliyopo hapo. Nimuombe Waziri aliangalie hili kwa jicho la huruma ili niweze kuongelea vijiji, sio kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri anafahamu kabisa Lushoto na Waziri mwenyewe Mheshimiwa Prof. Mbarawa anafahamu Lushoto. Lushoto kule wananchi wanapata taabu sana hasa katika Kata ya Kwai, Makanya, Malibwi, Mbwehi, Kilole, Kwekanga wananchi wanapata taabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mistari ya dini inasema *kullukum rai wakullukum masuul*. Hii ni dhamana, viongozi tutakwenda kuulizwa juu ya jinsi tunavyolinda mali zetu au tunavyowaongoza wananchi wetu. Kwa hiyo, sisi tusije tukawa masiula, Mheshimiwa Waziri usije ukawa Masiula, Naibu Waziri usije ukawa Masiula. Hakika, wewe Mheshimiwa Naibu Waziri unafahamu Lushoto. Dada zetu wanapata tabu sana, wanatoka mpaka vipara, hakuna hata wa kuwaoa *angel face* hazikai usoni, *carolite* hazikai usoni hata *lipstick* hazikai mdomoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe usije ukawa masiula, hebu angalia suala hili kwa makini, tusije tukaulizwa na Mwenyezi Mungu kwamba umewatendea nini wananchi wa Lushoto hususan akina mama. Nikuombe upeleke fedha katika Jimbo la Lushoto na maene haya niliyoyataja ili wananchi wangu hususan akina mama tuanze kuwatua ndoo kichwani kuliko ilivyokuwa sasa hali ni m baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, pia niende kwenye suala la kujenga mabwawa. Kama walivyosema, Lushoto ni ya milima milima lakini laiti Serikali ingekuja na mpango wa kujenga mabwawa naamini tusingepata taabu ya maji. Lushoto kuna maji ya mserereko, kwa hiyo, niombe Serikali sasa itenge fedha kwa ajili ya kujenga mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, waati tunasubiri miradi mikubwa, hebu sasa tupatieni fedha za kuchimba visima virefu ili wananchi wale waanze kupata maji, wananchi wale wasipate taabu san a na ukizingatia sasa hivi wananchi wetu wanatoka asubuhi hususan akina mama. Wanatoka asubuhi saa kumi na mbili wanarudi saa saba. Hivi hawa watoto watawahudumiaje kwenda shule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri na timu yake ili angalie ili kwa jicho la huruma. Nimeongea sana kwa muda mrefu hususan katika Bunge hili kuhusu mambo ya maji. Kwa kweli kama tumedhamiri akumtua mama ndoo kichwani basi kweli tumtue mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, watumishi Wizara ya maji mpaka kule chini kwenye idara hawatoshi ni wachache sana ndiyo maana unakuta mambo yanazorota. Pamoja na hayo, kuna hii sheria ya manunuzi, hii sheria inakandamiza sana na ndiyo inapelekea miradi inakuwa miradi inatengwa kwa gharama kubwa sana. Mfano unaweza ukaona *get valve* ya inchi sita inauzwa 1,000,000...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wetu ndiyo huo.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Kahigi ajiandae.

**MHE. MENRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni suala la kipaumbele, bila maji hatuwezi kuifanya kitu chochote. Kwanza kabisa namshukuru sana Waziri pamoja na Naibu kwa kazi nzuri mnayoifanya. Na sisi Wabunge inabidi tukusaidie kwa kutoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inahitaji kupata fedha nyingi sana. Sisi Wabunge tuliangalia tozo ya mafuta ile shilingi 50 lakini tunaona kuna ugumu wake na ili Wizara ipate fedha nyingi, nilikuwa napendekeza kwa sababu kila Mbunge akisimama tunaomba maji, kuna vijiji, kata, kuna sehemu nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa mapendekezo kwamba mnaonaje kwenye Wizara hii vitu vyote vinavyohusiana na maji tufute kodi, tufute kodi vyote. Kwa mfano, vifaa vya maji tufute kodi, watu wanaochimba visima tufute kodi, miradi mikubwa ya maji, tufute kodi ili Wizara iweze kupata fedha za kutosha na watu wengi sana wanajitolea. Kuna mashirika mengi sana yanajitolea kuleta maji katika nchi yetu. Mtu yeyote anayeleta maji hafanyi biashara, hii ni huduma ya jamii. Sasa ili tuweke kipaumbele na wananchi wapate maji ya kutosha, basi vifaa vya maji inabidi viwe vya bei ya chini sana, hii itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya maji ambayo tumewapa wakandarasi wazawa, kuna uzembe mkubwa sana. Serikali inatoa fedha lakini miradi haiishi kwanini? Kuna miradi mingine imetengenezwa lakini haitoi maji. Ukienda kuangalia mabomba yanakaa siku mbili/tatu yameharibika. Hili ni tatizo kubwa sana. Unaweza ukaona fedha nyingi sana imekwenda lakini ukaenda kuangalia utekelezaji wake sio imara! Hilo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwenye usimamizi wa miradi ya maji inabidi uongezeke mara tano, tusimamie vizuri sana kwenye miradi hii. Kwenye jimbo langu kuna miradi mikubwa ya maji Serikali ilitoa fedha, nataka nikuambie kuna mradi wa Mtwango ule, wa Sawala Mheshimiwa Waziri aliyepita alikuja na akasaini mkataba mbele ya wananchi. Naibu Waziri umekuja wewe ni shahidi, umeona pale mradi mpaka Serikali imeshatoa zaidi ya milioni 700. Mpaka leo tunavyoongea hivi, maji bado hayajatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mtiririko wa fedha, zinakwenda lakini mkandarasi hafanyi kazi na Serikali bado tunaangalia tu. Mkandarasi yule hafanyi kazi mpaka leo wananchi wa Kata ya Mtwango, vijiji karibu sita havina maji na Serikali imepeleka pesa. Zaidi ya miaka miwili, mradi unakwenda, mkandarasi yuko *site*. Ni tatizo! Tutafanyaje kulitoa hilo tatizo na tumesema wazawa, wakandarasi lazima wapewe kazi hii lakini hawafanyi kazi ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwingine kwenye Kata ya Itandula pale Kiliminzowo Serikali ilipeleka milioni 800, milioni 800 zilikwenda pale, mradi ule mpaka leo unatoa maji ya kusua sua tu ya wasi wasi. Serikali imepeleka pesa, wakandarasi wako pale wananunua vifaa sijui vifaa gani vile, vinakaa siku mbili vimeharibika. Tunafanyaje hilo, ni tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jimbo langu nina matenki karibu saba yalishachakaa, miundombinu imechakaa. Kwa mfano ukienda pale Nyololo, Waziri siku ile umekuja na uliniahidi kwamba watoe tenda pale mkandarasi aingie *site*. Nakupongeza sana Waziri, ulitoa bilioni 1.4 kwa Kata ya Nyololo lakini mpaka leo hii hawajatangaza tenda ile na wewe kibali ulishatoa. Wewe umetoa kibali tarehe 15 lakini tenda haijatangazwa mpaka leo na fedha zipo watu wanasuasua, tunafanyaje hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni 1.4 iko Nyololo kwenye Jimbo langu, Waziri umetoa kibali, watu hawafanyi kazi wako ofisini. Hili ni tatizo kubwa sana hili. Kata ya Igowole ni kata kubwa sana, pale ni mjini, tenki la maji liko pale, lina miaka zaidi ya 10. Wananchi wanakunywa maji Mbunge nilichimba visima pale ambavyo mimi nilisaidia lakini na tenki la maji liko pale, kwenye bajeti tulitenga milioni 400, mpaka leo hakuna mradi pale, wananchi wanahangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vyanzo vya maji Mufindi vimejaa, ni vingi! Sisi tuna vyanzo vya maji vingi sana, ile ya kuchimbachimba visima mimi Mbunge, nimechimba visima

vingi pale kwenye jimbo langu lakini kuna vyanzo vingi vya maji ambavyo tunaweza tukatengeneza maji ya *gravity system*. Naiomba Serikali tusimamie vizuri sana kwenye miradi hii ya maji. Sasa hivi Serikali inafanya vizuri kwa kutoa fedha, naishukuru sana, Serikali ya Awamu ya Tano fedha inapeleka lakini usimamizi sio wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hatuwezi kuilaumu Serikali jinsi ya kupeleka fedha kwenye majimbo, inapeleka! Lakini usimamizi mbovu sana na hii haitakubalika Serikali iwe inapeleka fedha halafu kuna watu wengine wanafanya mchezo hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ampongeza Mkuu wa Mkoa wa Iringa. Yule huwa anawaweka ndani wazembe wa kazi, safi kabisa! Mkuu wa Mkoa wa Iringa, uendelea na mtindo huo. Weka wengi tu ili wajifunze kwa sababu sisi tunataka watu wafanye kazi inavyotakiwa na katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tunatekeleza vizuri na hakuna mtu anaweza akabishana na Ilani, imekaa vizuri lakini watendaji wanatudondosha hasa wakandarasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba kwenye Jimbo o langu la Mufindi Kusini, Kata ya Mtambula, Itandula, Idunda, Mbalamaziwa, Malangali, Mtambula, Igowole, Mninga, Mtwango, Luhunga, sehemu zote zipewe maji. Bahati nzuri nawapongeza na wafadhili wangu *RDO* walipeleka mradi mkubwa sana Kata ya Luhunga, nawapongeza sana walifanya vizuri. Nawapongeza sana watu wa *UNICEF* wako vizuri, wametengeza mradi pale lhowanza umekaa vizuri sana. Nalipongeza Shirika la *Water for Africa* ambalo tulianzisha pamoja na ninyi, wanafanya kazi nzuri sana nawaombe tuwapunguzie kodi ili wafanye kazi vizuri. Wafadhili wanaojitolea kwanini umtoze kodi na anatoa maji bure yeye hafanyi biashara. Kuna mashirika mengine ya dini yanatoa msaada wa maji, kwanini tuwatoze kodi? Wale hawafanyi biashara ni kwa wananchi. Hili lazima tuliangalie vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji tukiwekea unafuu wa vifaa itakuwa vizuri, wala hakuna *inflation*, wengine wanasema labda *inflation* itaharibu, hakuna hiyo! Na kipaumbele cha kwanza kwa wananchi ni maji. Maji ni uhai, hakuna kitu kingine. Hapa hata tukipiga kelele ni kipaumbele cha kwanza cha wananchi ni maji vijijini. Mijini sasa hivi Serikali imejitahidi sana hata hapa Dodoma naona watu tunapata maji. Lakini vijijini tatizo ni kubwa, kuna watu bado wanatembea kilometa nne kilometa tatu wanatafuta maji. Kuna watu wengine wanachota maji na punda. Ukipita hii njia ya Iringa, ukitoka hapa kwenda Iringa utakutana na punda humo njiani wanatafuta maji huko na huko. Hili tatizo lazima tulifute kabisa lisiwepo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigola. Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Alfredina, halafu Mheshimiwa Aisharose Matembe.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza natumia fursa hii kutoa pole kwa jumuiya nzima ya wafanyabiasha, wadau wa habari, wadau wa viwanda na familia ya mzee wetu, Mheshimiwa Reginald Mengi. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kimya toka Wizara hii imeanza kuchangiwa, nilikuwa nasikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu na nilikuwa napitia kumbukumbu za Bunge kuangalia michango ya mwaka 2018, nimekuta kwa sehemu kubwa malalamiko yetu Wabunge ni yale yale yanajirudiarudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mwaka 2018 tulilalamikia juu ya ubadhirifu kwenye miradi ya maji, kuwepo na miradi ya maji isiyotoa maji na mambo kama hayo; na Serikali ikaahidi yafuatayo, naomba kunukuu maneno ya Mheshimiwa Waziri aliyoyasema: "Kuna haja ya kuunda timu

ya wataalamu watakaopitia miradi yote iliyotekelezwa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnapendekeza. Mlipendekeza kwamba iingie Kamati ya Bunge, lakini kabla hamjafika hapo, sisi tayari tumeshaunda na kamati hii itasimamiwa na Profesa Mbwete wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iliacha au ilikataa Wabunge tusiunde kamati ya kuchunguza ubadhirifu na miradi ya maji ambayo haitoi maji kwa kisingizio cha kwamba Serikali imeunda Kamati ya Profesa Mbwete, lakini Mheshimiwa Waziri alipokuja kutoa hotuba yake Bungeni, hajaeleza hiyo Kamati ya Profesa Mbwete imebaini yapi, watu gani wamechukuliwa hatua mpaka sasa na nini kinaendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, naomba baada ya kuhitimishwa hoja hii nitoe *notice* kabisa ya kupendekeza kuundwe Kamati Teule ya Bunge ili ipitite taarifa ya Profesa Mbwete lakini iende mbali zaidi kushughulikia ubadhirifu na ufisadi wote ulioko kwenye miradi ya maji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo la kwanza. Niliomba nianze nalo. La pili ni juu ya takwimu zinazotolewa na Serikali hapa Bungeni kuhusiana na hali ya upatikanaji wa maji. Serikali inasema, kwa wastani hivi sasa, vijijini maji yanapatikana kwa asilimia 65 na mijini kwa asilimia 80. Sasa nawaomba Wabunge wenzangu, hizi takwimu za Serikali zisikubalike kwa sababu hazilingani na hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushuhuda tu wa majibu ambayo yametolewa na Serikali hapa Bungeni na Mheshimiwa Naibu Waziri, mwezi Aprili, 2019, Naibu Waziri, juu ya upatikanaji wa maji Jimbo la Kibamba ambapo alisema upatikanaji wa maji ni asilimia hii hii 80, lakini alitoa majibu ya uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuingia kwa undani katika hili kwa sababu ya muda, naipa nafasi Serikali pengine

wakati wa majumuisho, irekebishe hii kauli. Kwa sababu Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye hotuba yake ukurasa wa nane, sehemu ya tano, wameeleza kiunagaubaga kuanzia aya ya 27 mpaka aya ya 35 ushahidi wa namna ambavyo maelezo ya Serikali hayakuwa ya kweli kwa kueleza kata kwa kata, mtaa kwa mtaa, hali halisi ya upatikanaji wa maji. Nami nafahamu kwa takwimu za ukweli, upatikanaji wa maji kwa Jimbo la Kibamba haujavuka asilimia 65 mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ije ieleze ukweli na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wafike Jimbo la Kibamba washughulikie hayo matatizo ili upatikanaji ufike hizo asilimia ambazo wanazieleza hapa Bungeni. Hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sababu hali hii siyo ya Kibamba peke yake, ni maeneo mengi nchini takwimu zinatolewa siyo za kweli, hiyo Kamati Teule ya Bunge itakapoundwa, pamoja na mambo mengine ikachunguze ili zipatikane takwimu sahihi za hali ya upatikanaji wa maji hapa nchini, Bunge liweze kuchukua hatua kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, tunaitwisha hii Wizara mzigo mkubwa ambao kwa kweli ni mzigo wa Wizara ya Fedha. Mzigo wa fedha kutokutolewa kwa wakati kwa ajili ya miradi ya maji. Tunavyozungumza hivi sasa, mpaka mwezi Aprili, ukilinganisha kiwango tulichopitisha kwenye bajeti na kiwango cha fedha kilichotolewa, fedha ambazo Serikali haijatoa bado kwa ajili ya Wizara ya Maji, kwa miradi ya maendeleo peke yake ni shilingi bilioni 329. Kati ya hizo, fedha za ndani ambazo Serikali haijatoa mpaka hivi sasa ni shilingi bilioni 288. Sasa kama Serikali hii ina uwezo wa kujigamba inalipa fedha taslimu kwa ajili ya kununua ndege, kwa nini haitoi fedha kwa ajili ya miradi ya maji? *(Makofi)*

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.



**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Mnyika, tulia kidogo. Taarifa Mheshimiwa Mlinga.

## T A A R I F A

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na heshima kubwa ya Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu mchangiaji Mbunge makini, nataka nimpe taarifa ya kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshasaini fedha na Serikali ya Ujerumani shilingi bilioni 330 ambazo yeye anasema kilichopungua hapo ni shilingi bilioni 229. Zinakuja kulipwa, hilo tatizo halipo. La pili, Serikali tarehe 14 mwezi huu...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Taarifa ni moja tu, ahsante.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Haya ahsante.

**MWENYEKITI:** Samahani nilikuita Mlinga, kumbe Mtulia. Samahani sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusainiwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo hakujibu haja na hoja ya fedha za ndani ambazo Bunge lilipitisha ambazo Serikali inapaswa ilieleze Bunge, kwa nini fedha hizi hazijatoka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja kuchangia hii hoja hatatoa maelezo ya kuridhisha, nitaomba nafasi kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1) ili bajeti hii isogezwe mbele mpaka kwanza Serikali itimize matakwa ya kutekeleza bajeti ambayo imekusudiwa na Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye hizi fedha za wahisani, mwaka 2018 tuliambiwa maneno kama haya haya juu ya fedha za India. Tuliambia Serikali imesaini mkataba wa dola milioni 500. Ninao ushahidi hapa wa *Hansard* wa kiwango kilichosainiwa. Hata kwenye hizo fedha za wahisani vilevile, kwa mujibu wa utekelezaji wa bajeti, kiwango cha

fedha kilichotolewa hakijakamilika kwa idadi ya kiwango cha fedha ambacho kilipitishwa na Bunge. Kwa hiyo, hapa napo ipo hoja ya kujadili na Bunge lifanye kazi ya kuisimamia Serikali ili hatua ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haiwezi kutekeleza Bajeti, ni kwa nini mwaka huu vilevile Serikali imeleta hoja, ikitaka fedha nyingi zitengwe, mabilioni yale yale, safari hii imepunguza kidogo; fedha za maendeleo zimepungua kutoka shilingi bilioni 673 mpaka 610, pungufu ya shilingi bilioni 63, lakini bado fedha ziko kule kule juu. Kama Serikali inajijua haina uwezo wa kupeleka fedha, basi ilete bajeti inayolingana na mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu, Serikali hii ingeamua kipaumbele kiwe maji badala ya ndege fedha zingetengwa kwa ajili ya maji na wananchi wangekombinelewa; na kwa sababu Serikali hii inajigamba wazi wazi kabisa kuleta maendeleo ya vitu, kama ndege, badala ya maendeleo ya watu kwenye miradi kama ya maji, tiba siyo ninyi kwa sababu hamsikii tena, tiba ni Watanzania, kujiandaa kuiondoa Serikali ya CCM madarakani kuanzia kwenye uchaguzi wa mitaa, kwenye vijiji, kwenye vitongoji, kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ili kuingiza kwenye uongozi wa nchi Serikali ambayo itajali maslahi ya watu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa!

## TAARIFA

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie kaka yangu kwamba unapozungumzia maendeleo ya watu, huwezi kutenganisha maendeleo ya watu na kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati ambayo ndiyo yatazalisha fedha za kutosha kwa ajili ya kuendesha kuleta maendeleo. Ukizungumzia maji,

unahitaji biashara ya ndege, unahitaji utalii ili uweze kuongeza kipato kiweze kuingia kwenye maji.

**MWENYEKITI:** Usichangie.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Haya mvuvuzela...

**MWENYEKITI:** Usichangie Mheshimiwa, toa taarifa tu. Ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo maeneo ya kimkakati ndiyo biashara ya ndege ambayo Shirika la Ndege linaendesha kwa hasara, kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kushindwa tu kujua namna ambavyo maji ni kipaumbele. Maji ni kipaumbele, siyo kwa sababu tu ni huduma kwa wananchi, maji ni kipaumbele vilevile kwa sababu ni huduma ya kiuchumi ambayo ingewezesha uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni kipaumbele. Naomba vilevile Wizara itakapokuja kwenye majumuisho, ieleze ni kwa nini fedha za kujenga mradi wa Kidunda mpaka sasa hazijapatikana? Kwa mujibu wa kumbukumbu za Bunge, ninazo kumbukumbu za Bunge hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu Bungeni kuhusiana na hoja ya Kidunda, kwa sababu ya muda naomba nisiende kwenye ukurasa, lakini alilieleza Bunge kwamba Serikali iko kwenye majadiliano na NASSSF kwa ajili ya kutoa fedha za ujenzi wa mradi wa Kidunda na kwamba akaahidi ifikapo mwezi Julai, 2018 zabuni ya Bwawa la Kidunda ingetangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sasa hivi Serikali hii isiyowekea kipaumbele miradi ya maji, inasema kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ndiyo kwanza fedha za Mradi wa Maji wa Kidunda, zinatafutwa, mradi ambao ukitekelezwa, siyo tu utanusuru watu wa Dar es Salaam na Pwani; kwa sababu pamoja na kupanua Ruvu Juu na Ruvu Chini, kwa sababu ya mabadiliko ya nchi, wakati wa kiangazi,

maji Dar es Salaam hayatakuwa yanapatikana ya kutosha, ndiyo maana tunahitaji fedha kwa ajili ya mradi wa Kidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu mradi huu utasaidia kwenye maji ya viwanda na majumbani, mradi huu ungeweza kuzalisha *megawatts...* (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ahsante sana.

**MHE. JOHN J.MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, lakini suluhu ni kuiondoa Serikali madarakani. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Alfredina Kahigi, Mheshimiwa Matembe na Mheshimiwa Edwin Sannda wajandae.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara ya Maji, hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mchango wangu, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mbarawa; Naibu wake, Mheshimiwa Aweso kijana wangu, kwa kazi ambayo wanaifanya, tunaiona. Nisiwe mwizi wa fadhila, wanafanya kazi usiku na mchana, tunaona wanakimbizana, Mungu awabariki sana na Mungu azidi kuwatia nguvu. Ni lazima nimsifie (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge ninayetoka Mkoa wa Kagera, Kanda ya Ziwa. Mkoa wa Kagera tuna Majimbo mengi ambayo yanapakana na Ziwa Victoria. Ziwa Victoria tuna Wilaya nyingi ambazo zina upungufu wa maji. Kwa mfano, Wilaya ya Bukoba Vijijini, Wilaya ya Muleba Kaskazini na Kusini, Wilaya ya Misenyi; kuna baadhi ya kata ambazo zina matatizo ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha kiangazi ambacho tunaelekea mito inakauka, wanawake wanapata shida kubwa sana ya kupata maji. Pamoja na kwamba Ziwa Victoria, liko sehemu nyingi sana limetambaa Mkoa wa Kagera, lakini kijiografia tuko juu ya Ziwa Victoria. Kata nyingine ziko juu ya Victoria. Naiomba Serikali iwasaidie wananchi wa Kagera ambao wako juu ya milima waweze kuwapatia maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, ninaomba Serikali iweke mkazo, wananchi ambao wanalima kwenye vyanzo vya mito, wanaokata miti ovyo ovyo na kuchoma miti, wakatazwe kabisa wasifanye vitu hivyo, ndivyo vinavyopelekea tukakosa maji kwa wingi. Zamani mito ilikuwa inatiririsha maji vizuri, lakini sasa hivi inakauka, ni kwa sababu ya matatizo hayo. Serikali iwekee mkazo jambo hilo kusudi waache kukata miti na kulima kwenye vyanzo vya mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, naiomba Serikali, kwa wale ambao wamejaliwa kujenga nyumba ambazo zina mabati, ni vizuri wakavuna maji ya mvua, wajenge matanki ya saruji madogo madogo, kwa watu wale ambao wanajiweza ili maji yale ambayo yanapotea kwenye ardhi yaweze kuwasaidia wakati wa kiangazi, itakuwa ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile na maji yale ambayo yanapotelea kwenye ardhi, kama watu wangukuwa wanayavuna, mito mingine kipindi cha mvua isingekuwa inafurika na madaraja kuvunjika. Huenda ingekuwa inasaidia na yenyewe kwa ajili ya kuyavuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine naomba, kuna mradi wa Wilaya ya Karagwe, huo mradi ulianza mwaka 2005, ndipo ulipozinduliwa, mradi wa Lwakajunju. Mwaka 2010 upembuzi yakinifu ulikamilisha jambo hilo, mwaka 2018, Mheshimiwa Rais alipokuja kufungua barabara ya Kyaka Bugene, alisema kwamba shilingi bilioni 70 tayari zimeshatoka kwa wafadhili, huo mradi unapaswa kuanzishwa. Mpaka leo

hii ninaposema, hakuna kitu ambacho kimeshafanyika. Mheshimiwa Waziri ninaongea na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema kwamba huo mradi uanze, maana shilingi bilioni 70 tayari zimeshatoka kwa wafadhili India, lakini mpaka leo hii huo mradi haujaanzishwa na wananchi wa Karagwe, wanapata shida sana ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Karagwe wana milima mirefu, wanawake wanafuata maji kwenye mabonde, wanapata shida sana. Naomba Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind-up* atuambie huo mradi unaanza lini? Maana umekuwa mradi, mradi, ngonjera, ngonjera, wananchi wa Karagwe wanawake wameota vipara wanapata shida. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu ambalo liko sahihi, maana wamenituma nije nisemee hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kusema, ni kuhusu..., aah, yameniishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kahigi kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea. Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mheshimiwa Edwin Sannda, Mheshimiwa Flatei Massay ajiandae.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii muhimu ya maji kwa maendeleo ya Watanzania. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya chama changu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwaletea Watanzania maendeleo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, amekuwa na ziara ndefu akihamasisha

maendeleo, hakika tunamwombea heri, baraka na nguvu katika kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji Profesa Mbarawa, Naibu wake Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu, Kitilya Mkumbo, pamoja na watendaji wote kwa hotuba nzuri, hotuba ambayo inatoa mwelekeo wa kumtua ndoo mwanamke kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ndiyo kila kitu. Maji ni uhai, maji ni maendeleo, maji ni uchumi, lakini maji haya yamekuwa yakileta madhara makubwa, mfarakano na kusababisha ndoa nyingi kuvunjika na kuwafanya wanawake wengi kutokushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu wa Singida unakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa maji safi na salama, hususan maeneo ya vijijini na hii ni kutokana na jioografia yake. Jambo kubwa la kusikitisha ni kwamba, hata miradi mikubwa inayopangwa kutekelezwa katika Mkoa wa Singida imekuwa ikisuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mradi wa Maji Kitinku, Lusilile katika Wilaya ya Manyoni, uliibiliwa chini ya mpango wa Matokeo Makubwa Sasa na ulianza kutekelezwa mwaka 2013, lakini hadi leo ni miaka sita mradi huu haujakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuambie, ni lini fedha za kutosha zitapelekwa kwa wananchi wa Manyoni ambao wanausbiri mradi huu kwa hamu kubwa na ni vijiji kumi vitakavyonufaika. Vijiji hivi ni Kintinku, Lusilile, Maweni, Chikuyu, pamoja na vijiji vingine ambavyo vipo karibu katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutupa miradi mikubwa miwili ya maji ya mtandao wa bomba katika Jimbo la Ikungi Magharibi. Miradi hii ni ya Ighuka na

Mtunduru, lakini niombe sana, sana Serikali ipeleke fedha za kutosha ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati kwa sababu wananchi wa Jimbo la Ikungi Magharibi wanapata tabu sana ya ukosefu wa maji safi na salama. Pia naishukuru Serikali kwa kutupa vibali vya kuchimba visiwa 20 kwenye Jimbo la Ikungi Magharibi pamoja na Ikungi Mashariki. Naomba vibali hivi viende sambamba na kutupa fedha za kutosha ili wananchi waondokane na adha ya ukosefu wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji katika Mkoa wangu wa Singida hususan maeneo ya vijijini bado ni duni sana na vijiji vingi bado havina huduma ya maji safi na salama. Mfano Jimbo la Singida Kaskazini Vijiji vya Mitula, Migugu, Ughandi B, Misinko, Mwishanji havina kabisa mtandao wa maji, maji wanayotumia ni maji ya malambo na unapofika wakati wa kiangazi, maji haya yanakauka na wananchi wanapata tabu kubwa sana ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuchangia ni ukosefu mkubwa wa vitendea kazi yakiwemo magari, pamoja na watumishi wa Idara za Maji. Naishauri Serikali iangalie jambo hili kwa jicho la tatu; Wilaya zangu zote za Singida ikiwepo Mkalama, Manyoni, Ikungi, Iramba na Singida Vijijini wapate watumishi pamoja na magari na vitendea kazi vya kutosha. Naipongeza na kuishukuru Serikali kwa kutupa Mamlaka za Maji katika Miji Midogo ya Ikungi, Mkalama na Itigi. Tayari Bodi zimeshaundwa na mapendekezo yameshapelekwa Wizarani. Naiomba Serikali basi iharakishe upatikanaji wa bibali hivi, naamini kwamba Mamlaka hizi za Maji zitaweza kusaidia sana upatikanaji wa maji katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala lingine ambalo ningependa kulichangia; kuna changamoto kubwa sana ya ukosefu wa maji katika Taasisi za Elimu na Afya. Watoto wetu wa shule wamekuwa wakitumia muda mrefu sana kuhangaika kutafuta maji na unategemea jambo gani la ufaulu iwapo watoto hao wanatumia muda mwingi kutafuta



maji. Pia watoto wanapofika siku za hedhi, watoto wa kike wanataabika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa la kusikitisha ni kwamba wanawake wajawazito wanapokwenda kujifungua wanaambiwa waende na maji ni kwa sababu kwamba Taasisi hizi za Afya zinakuwa hazina miundombinu ya maji. Niombe sana pia Serikali iangalie jambo hili kwa jicho la tatu, iweke miundombinu katika shule zetu pamoja na Taasisi za Afya ili kuweza kuwapatia wananchi huduma ya maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii na nakushuru kwa muda ulionipatia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Edwin Sannda, dakika nane, Mheshimiwa Flatei dakika nane na Mheshimiwa Leah Komanya dakika nane.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Maji, Wizara muhimu kabisa. Kwanza niwapongeze Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wengine wote kwenye Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya na ukiona kama kilio ni kikubwa hapa si kwamba kazi hawafanyi, kazi wanafanya lakini bado uhitaji ni mkubwa kweli kweli, tunawashukuru sana na tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambazo anaendelea nazo na usimamizi mkubwa wa hata Wizara hii iliyo chini yake na Wizara nyingine zote, mambo mazuri yanaendelea na nchi naona kabisa kwamba sasa mwelekeo tunaokwenda ni mwelekeo umenyooka, mwanga unaonekana kule mbele kwamba Tanzania mpya sasa inaonekana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Wizara yetu hii ya Maji na mahitaji na changamoto ambazo tunazipata pale Jimbo letu la Kondoa Mjini. Toka nimeanza 2015 au tuzungumzie 2016 mwanzoni mpaka leo tunavyozungumza tulikwishaidhinishiwa fedha kiasi cha bilioni 3.7 na mpaka sasa ambazo zimekwishaingia, zimelipwa kabisa ni bilioni 2.5, hizo tayari kabisa zilishapokelewa, bado kuna kiasi kidogo cha kuwalipa makandarasi. Hapa tumechimba visima 10 ambavyo kati ya hivyo vingine vilikwenda Kata za Mjini ambazo ziko kama tatu, kata ambazo ziko pembezoni ni kama nane hivi na kwenyewe tumesambaza kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katikati Mji kwenye kata tatu, mwanzo tulikuwa tunategema maji ya chemchem ya asili, kulikuwa na tatizo kubwa sana, tukaamini na fedha hizi zote ambazo zimeingia kule kwetu basi tatizo la maji litapungua kweli kweli kwa sababu pale katika kwenye hizi kata tatu tumechimba visima vitano ambavyo vimeenda kuongezea upatikanaji wa maji ambavyo vinaenda ku-*compliment* ile chemchem. Hata hivyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, leo tunavyozungumza bado kilio ni kikubwa kweli kweli cha tatizo la maji pamoja na kwamba tuna visima vipya vitano na vimesambazwa pale Kwapakacha, Kilimani, Tura, Tumbelo na maji yamesambazwa Wisikwantisi lakini bado huu mzigo wote tulitegemea sasa ule mzigo uliokuwa ukienda chemchem ungepunguza uhitaji basi hii mitaa mingine ibaki ina maji ya kutosha lakini sivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni nini? Inaonekana liko tatizo la wazi kabisa katika utekelezaji wa hii miradi kwamba labda zile *design* zinazofanywa za usambazaji, idadi ya matenki, urefu wa mabomba, idadi ya vizimba, huenda kuna tatizo wakati wa *design*, wasanifu wetu wanapofanya kazi inabidi Wizara isimamie kwa karibu sana kuona *design* hizi ni *efficient* na zitakuwa *effective*, sasa hebu fikiria bilioni 2.7 imeingia na bado kilio cha maji kipo kikubwa Mitaa ya Mnarani, Miningani, Ubembeni, Maji ya Shamba ambapo ndio mjini katikati, kilio ni kikubwa kweli kweli. Hapa nimwombe Mheshimiwa Waziri hebu tufanye utaratibu, turudi

tufanye kazi na timu labda Mainjinia wa Mkoa lakini na kule halmashauri kwetu tuone tatizo liko wapi? Kwa nini tulishatoa hela nyingi halafu tatizo la maji bado ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea, tulikuwa tumeomba pia fedha kiasi cha shilingi bilioni nne kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji pale mjini katikati, ilifanywa *design* nzuri tu sijui sasa kama Wizara na yenyewe imeihakiki ile *design*, tumepeleka andiko pale Wizarani, mpaka dakika hii niki-*compliment* yale niliyokuwa nikiongea mwanzo, inawezekana hata haya maji ambayo tayari tumeshakuwa tukiyasambaza kupitia hivi visima vipya na ile chemchem, chanzo cha maji cha chemchem inawezekana yasiweze kukidhi au kusambaa vizuri kama fedha hizi za ukarabati wa miundombinu zisipopatikana. Tunaomba, tutakuwa tumefanya kazi kubwa sana huku nyuma kama tumekula ng'ombe mzima tumebakiza mkia, hela imeshalipwa lakini wananchi hawanywi maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize kwenye hili kwamba kuna umuhimu mkubwa kupata zile fedha za ukarabati wa miundombinu ya maji. Miundombinu hii ilijengwa mwaka 1972, wakati Mji wetu wa Kondoana una *population* ambayo ilikuwa labda haizidi watu 20,000, leo hii tuna *population* ya watu 50,000, haiwezekani ikawa inatosha, lakini pili imeshakuwa chakavu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Edwin Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** ... kwa kiwango hiki hela ile tui pate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei, dakika nane atafuatiwa na Mheshimiwa Komanya dakika nane.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami siku ya leo nichangie hoja hii. Kwanza naomba uniruhusu niwapongeze kwa kweli Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Watendaji Wakuu kama Katibu Mkuu wanavyofanya kazi kwenye Wizara hii ya Maji, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mdogo naomba tu nijielekeze moja kwa moja kwenye maeneo ya wakandarasi. Jimboni kwangu kwa kweli kuna miradi mitano, miradi hii yote kwa kweli mpaka sasa haifanyi kazi mmoja walau una afadhali. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri amefika kwenye Jimbo langu na ametembelea miradi hii ameona mwenyewe kwa macho yake. Kwa hiyo ninapozungumza nina hakika anajua nazungumzia nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Harsha, umesanifiwa 2012, hadi leo haujakamilika, wamejenga matenki, wameweka maeneo ya kujichotea maji lakini kwa kweli wananchi sasa wameduwaa, wanazidi kusubiri, hakuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mradi wa Tumati - Mongahay uko palepale. Nimesoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri aliyoiandika humu na nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakika nachelea kusema tuna hali mbaya kweli kweli. Nimeleta maswali si chini ya 13 humu ndani ya Bunge, nimepata majibu, lakini miradi hii bado haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa sababu kinachoonekana hapa tunalo tatizo kubwa la fedha na ukiangalia sasa kwa muda huu ambao mkandarasi amefanya kazi na hakulipwa, tumeshavunja mkataba maana yake mkandarasi huyu amekwishaondoka *site*, hayuko tena *site*. Nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Wakuu wake wa vitengo waangalie jinsi ambavyo wakandarasi hawa wamepewa hizi *tender* na hawa wanaopewa *tender* waangalie basi, nakumbuka kwenye hotuba ya mwaka jana alituhidi hapa kwamba wataunda

tume ambayo wao wenyewe kama wataalm watakwenda kuhakiki na kuangalia miradi nchi nzima na nilitegemea basi watakuwa wamefika Jimboni kwangu Mbulu Vijijini, lakini hilo sidhani kama limetokea na kama limetokea basi Waziri atakuja kuniambia wakati anahitimisha bajeti yake hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ukiangalia tatizo lilloko katika maeneo yetu pamoja na wakandarsi kuwa na matatizo lakini shida ya ulipwaji wa *certificate* ambazo kimsingi zinakaa sana Wizarani, kama kuna Wizara nimetembea, nimeenda ofisini, nimetembea mno, nimeonana na wataalam wote, nimejitahidi kweli kweli, mara nyingi pia nimejaribu kwenda na Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya kwenye Ofisi ya Katibu Mkuu na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na kusumbuka kote huku miradi hiyo bado haina namna ya kumsaidia mwananchi. Kwa hali hii katika jimbo langu lazima niseme ukweli, ni ngumu kusema kwamba unaweza kumtua mama ndoo kichwani, kwa kweli hili halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba amekuja na ameona pale Haidom, ameagiza kisima kichimbwe na juzi tarehe ya 25 nimeuliza swali la nyongeza hapa na akaagiza *DDCA* wachimbe visima, hali ni mbaya naomba kabisa waone namna ya Wizara watakavyosaidia Jimbo la Mbulu Vijijini kutokana miradi hii ambayo imekuwa viporo, wameshaacha *certificate*, zimeshakaa kwenye Wizara, lakini kubwa zaidi miradi mingine miwili wakandarasi wameshatengua mikataba, kwa hiyo hawafanyi kazi tena na tumetangaza *tender*. Naomba basi katika bajeti ya mwaka huu apeleke fedha ili hawa wakandarasi wanaoomba tena miradi hii waweze kuendelea kwa sababu bila fedha hakuna kinachotendeka. Kubwa zaidi niombe pia hawa Wahandisi Washauri wanaokuja katika miradi hii, nishauri tu watumie tena utaalam wao ili waweze kushauri miradi hii iishe vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo hali hii ya hao Wahandisi Washauri inawezekana huenda taaluma zao siyo

sawa, waangalie kwa wana-*design* miradi ambayo haiishi na shida ni nini? Tujue, lakini kubwa zaidi nashauri kwa mfano Mradi wetu wa Haydom umekaribia kumalizika, tumepeleka maombi Wizarani tuumalizie sisi kama halmashauri kwa kutumia *Force Account* kwa sababu sheria inaruhusu na inasema mradi unaweza kutumia *Force Account* yaani bei ya soko na sisi tukajenga tukaumalizia kuliko kuweka tena mkandarasi kwa sababu tuna uwezo wa kufanya hivyo. Mabomba yako tayari, maeneo mengi yamekwishamalizika, watuache sisi tumalizie, tumepeleka Hadidu Rejea na iko Wizarani kwa Waziri aangalie namna yoyote, nafikiri wananisikiliza, ni hela kidogo tu ni milioni isiyopungua 70, tunaweza kumaliza sisi wenyewe watuachie na mimi nina Injiniya ambaye kimsingi amekuja, watuachie tumalize kwa kutumia *Force Account*...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKIITI:** Ahsante sana.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba tu niunge hoja mkono, lakini kwa masikitiko makubwa sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri na maombi yako. Tunaendelea na Mheshimiwa Leah Komanya, dakika nane na Mheshimiwa Maulid Mtulia dakika tano, halafu Mheshimiwa Ramo Makani Injiniya dakika tano.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii, nikianza na kuunga mkono kwa asilimia mia moja hoja iliyoletwa mbele yetu na Wizara ya Maji.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi nzuri anazozifanya katika Wizara hii, Mheshimiwa Waziri nampongeza amekuwa akitembelea mazingira yetu na kuona hali halisi ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kufanya masahihisho katika ukurasa wa 56 wa hotuba. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imesema kwamba, nishukuru kwanza kwa Serikali kutoa shilingi bilioni 1.7 ili kukamilisha Bwawa la Mwanjolo, lakini nataka kusema kwamba maelezo yalitolewa katika kitabu kwamba tayari wananchi wa Mwanjolo, Jinamo, Mbushi Wilayani Meatu wanapata huduma ya maji wananchi 13, 859 siyo sahihi. Kilichopo hapa ni mabirika ya maji kwa ajili ya mifugo, ndiyo wanaokunywa maji. Usambazaji wa maji katika vijiji vilivyotajwa hapa haujafanyika. Ninachoomba fedha kwa ajili ya kufanya usanifu kwa ili kusambaza maji kwa wananchi katika vijiji tajwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali na kuishukuru kwa kusaini mkataba wa shilingi bilioni 330 kwa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya Mkoa wa Simiyu na kuyapeleka Nyashimo, Bariadi pamoja na Itilima ambao utekelezaji wake utakamilika mwaka 2022. Nataka nitoe maoni yangu machache; toka mwaka 2016, Wabunge wa Mkoa wa Simiyu tumekuwa tukiomba mradi huu yajengwe mabomba mawili, lakini fununu niliyoisikia kwamba linajengwa bomba moja. Kama litajengwa bomba moja dhana nzima ya kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi haitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilitafutwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa lengo kuu la kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Simiyu ambao umekumbwa na ukame wa muda mrefu, endapo kama litajengwa bomba moja wananchi hawataweza kumudu maji haya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Lengo kuu lilikuwa ni kukabiliana kwa kilimo cha umwagiliaji, kama litajengwa bomba moja maji haya yakitibiwa gharama yake itakuwa juu wananchi hawataweza kuyanunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri mawazo ya Wabunge yasikilizwe kuwe na mabomba mawili ambayo litakuwa na maji ghafi ambayo hayajatibiwa ambayo hayatakuwa na gharama kubwa ili wananchi waweze

kuyamudu kwa ajili ya kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa kuwa mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili na Wilaya ya Meatu na Maswa ni Wilaya zilizo na ukame mkubwa...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana kwa mchango wako mzuri sana, sababu ya muda tu najua una mengi. Mheshimiwa Mtulia, atafuatiwa na Mheshimiwa Injia Ramo Makani dakika tano tano, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, dakika tano na Mheshimiwa Shanif Mansoor, dakika tano.

**MHE. MAULID S.A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima na mimi kupata fursa ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Pili, nikushukuru wewe Mwenyekiti wetu. Tatu, niwashukuru Watendaji wote Wizara ya Maji nikiianza na Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Maji ni nyeti sana kama Wabunge wengi walivyosema lakini vilevile tujikumbushe Wizara hii katika Awamu hii ya Tano tu wamepita Mawaziri wengi na wamefanya kazi kubwa. Ameanza Mzee wetu Mheshimiwa Maghembe, Mheshimiwa Eng. Lwenge, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe na sasa tunaye Mheshimiwa Profesa Mbarawa. Kwa kweli wote wamefanya kazi nzuri lakini sasa hapa kwa Profesa kwa kweli mambo yanakwenda kweli kweli. Wakati mwingine Profesa unamkuta ananing'inia kwenye ngazi unapata raha kabisa, mzigo unapigwa kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine matatizo yetu yanaonekana kwa sababu ya uzito wa jambo lenyewe na umuhimu katika jamii yetu. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuwaunge mkono



wenzetu hawa kuhakikisha kwamba tunawapa nguvu, tunawatia moyo hili jambo liende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu Kinondoni maji tunapata, yako mengi na ukichukua Mradi wa Ruvu Chini na Ruvu Juu hatuna shida sana ya maji, shida yetu ni mtandao wa maji tena kwa baadhi ya kata. Niiombe Wizara ishirikiane na watu wetu wa Dar es Salaam kwa ajili ya Kata zetu za Tandale, Mwananyamala, Makumbusho, Kigogo, Hananasifu na Mzimuni. Hizi ndiyo kata ambazo tunaamini mtandao wa maji ukiwekwa itakuwa ni vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nishukuru tu kwamba bajeti ya mwaka huu inakwenda nzuri na itatekelezeka. Kama nilivyosema pesa zimesainiwa lakini zile shilingi trilioni 1.2 ambazo hata kaka yangu Mheshimiwa Mnyika amezisema asiwe na wasiwasi mwaka huu ndiyo mwaka wa mavuno, mihela itakuwa inashuka kwenye Wizara ya Maji kwa maana shilingi bilioni 330 ipo, shilingi trilioni 1.2 zipo, wasimamizi wapo, *RUWASA* inakwenda kuanzishwa mwezi Julai, tuhakikishe mapanya wote wanaokula pesa za maji wanakwenda kudhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni wakati wetu sasa, hakuna wakati mzuri ambao tunatakiwa tuungane, tushikamane kuwasaidia wenzetu hawa kwa sababu wameonyesha dhamira ya kweli. Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi kila Mbunge ametembelewa na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri au na Katibu Mkuu au na kiongozi yoyote. Hili jambo kwa kweli siyo dogo, ni jambo ambalo sisi kama viongozi na wawakilishi wa wananchi lazima tuwape moyo; mnyonge, mnyongeni, haki yake mpeni.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, unga mkono hoja.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Ramo Makani.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa fursa hii. Kwa muda wa dakika tano nachoweza kusema ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, pongezi kwa ujumla kwa Serikali lakini mahsusi kabisa kwa Wizara ambayo hoja yake iko mezani, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na timu yake nzima, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Profesa Kitila Mkumbo - Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu – Eng. Kalobelo, Wakurugenzi wote pamoja na wataalam kwa ujumla pamoja na wafanyakazi wengine wa kada saidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nashukuru Serikali kwa sababu katika Jimbo la Tunduru na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa ujumla tulipata fedha kwenye bajeti hii jumla ya shilingi bilioni 1.27; shilingi milioni 300 mjini na milioni 974 vijijini. Siwezi kutumia muda mrefu sana kurudia kusema kwamba fedha hizi hazitoshi lakini ieleweke tu kama ujumbe kwa Wizara kwamba hasa kwa mradi wa mjini ambao unahitaji fedha karibu shilingi bilioni 16, bajeti ya shilingi milioni 300 kwa mwaka maana yake mradi huu utachukua karibu miaka zaidi ya 50. Kwa hiyo, tutafutiwe fedha kwa kutoka vyanzo vingine na kwa *style* nyingine tuweze kukamilisha mradi wa Tunduru Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Tunduru uko mahali pa kimkakati hata kitaifa. Ni mji ambao uko katikati ya umbali wa kutoka Bandari ya Mtwara mpaka Bandari ya Mbambabay. Pia kule tuna zoezi maalum la kimkakati Kitaifa la *Mtwara Corridor*, maendeleo ya kitaifa yatakavyoweza kuchangiwa na maendeleo ya Kusini kupitia Miradi ya Ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri yenyewe ilishamaliza mjadala hapa Bungeni na hasa pale ilipokuwa inazungumzia changamoto. Imetaja

changamoto tano lakini kila changamoto Wizara imetoa mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza upungufu wa fedha kwa ujumla katika kutekeleza miradi ya maji nchini. Wao wamesema Serikali inaendelea kutafuta fedha na mimi narudia Serikali iendeleo kujipanga kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi yote muhimu kwa ajili ya kuwapatia wananchi huduma hii ya maji ambayo ni muhimu na kila Mbunge akisimama anaeleza namna gani mahitaji ya maji ni muhimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ya pili muhimu kabisa kupita hata hiyo ya kutafuta fedha, wamesema hivi na hii nitaisoma kabisa, 5.2, ukurasa wa 108, anasema: “Uwezo mdogo katika utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji”. Kitaalam hii wanaita *low absorption capacity*, uwezo mdogo wa kutumia fedha ulizonazo kwa tija na kutumia fedha kwa tija maana yake utekeleze mradi ufanikiwe. Mafanikio ya mradi yanatafsiriwa kitaalam kwamba ujenge mradi kwa wakati, uwe na ubora, kwa gharama zile ambazo zimekadiriwa na uwe endelevu (*sustainability*) utakaozingatia mazingira lakini pia uhakikishe wale walengwa (*stakeholders*) wanapata yale matarajio yao, ndiyo maana ya mradi uliofanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji ukisikiliza michango ya Wabunge wote haikidhi haya niliyoyaeleza, mambo karibu matano. Sababu kubwa ni nini? Sababu kubwa ipo muda hautoshi ningeweza kuieleza iko kwenye utaalam.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante *Engineer* Makani.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Jacqueline Msongozi dakika tano.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadhirifu katika miradi ya maji. Kwenye miradi ya maji kuna ubadhirifu mkubwa sana. Hii inasikitisha sana pale ambapo Serikali inatoa pesa na pesa zile haziendi kufanya kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Litola kuna mradi wa maji wa zaidi ya shilingi milioni 200 lakini mradi ule haufanyi kazi una zaidi ya miaka mitatu. Kata ya Mkako kuna mradi wa shilingi milioni 718, mradi huu maji hayatoki lakini pesa asilimia karibu 90 imeshalipwa kwa mkandarasi. Sasa mimi nashindwa kuelewa hili jambo linakuwaje na wakati huo huo, katika utekelezaji huu huwa kunakuwa na Mhandishi Mshauri, Mhandishi Mshauri ambaye anashauri miradi kama hii hapa ambayo mwisho wa siku inagharimu pesa nyingi na haiwezi kutoa maji na kufikia malengo tunayokusudia amechukuliwa hatua gani?

Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aseme katika miradi hii iliyofanyiwa ubadhirifu ni watu gani ambao wamechukuliwa hatua ili tuweze kujua vinginevyo Mheshimiwa Waziri nashindwa kukuelewa pale ambao upo hapo lakini pia hatusikii chochote kinafanyika kuhusiana na hawa watu waliofanya ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mbarawa kwamba kuna dhambi ambayo hawezi kuikwepa hata ikawaje. Mkoa wa Ruvuma katika Kata nilizozitaja, Kata za Litola, Mkako, Nandembo ndoa za watu zimevunjika kwa sababu ya kukosa maji. Akina mama wanafuata maji umbali mrefu, kwa hiyo, kuna ndoa ambazo zimevunjika, Kata ya Litola ndoa tatu zimevunjika, Mheshimiwa Waziri atajibu. Kata ya Mkako ndoa tisa zimevunjika, wanawake wanafuata maji umbali mrefu. Kata ya Nandembo hali kadhalika ndoa nne zimevunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hawatendei haki Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa sababu sasa wanaondoka kwenye hali ya kuwa na ndoa zao wanaanza kuwa ma-*bachelor*. Niombe sana utakapokuja unijibu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mbarawa nisaidie katika hili kuhakikisha kwamba miradi hii niliyoitaja iliyogharimu pesa nyingi, nijue ni nini ambacho kimefanywa kwa sababu katika Mradi wa Mkako, shilingi milioni 718 zinaendelea tu mradi haufanyi kazi, umeacha tafrani katika maeneo husika. Naomba tafadhali sana sana, wanawake wa Mkoa wa Ruvuma tunakullia ndoa zetu zinavunjika kwa sababu ya kufuata maji umbali mrefu, waume zetu wanakosa imani, tunashindwa kuwahudumia waume zetu, kwa hiyo, tunakosa sifa ya kuwa wanawake bora wa kuhudumia familia zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Waziri naomba ajibu kwa nini miradi hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hujasema ndoa yako wewe ikoje, haya Bwana. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mansoor dakika tano.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umenipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema niweze kusimama mbele yako kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba kuzungumza kuhusiana na suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la maji naomba niseme mambo matatu. La kwanza, kuna Mradi wa Shirima; ulianza mwaka 2013, mwaka jana ulipofanya ziara

kwenye Jimbo la Kwimba nilienda na wewe tulikupeleka mpaka kwenye mradi huo wa Shirima, Kata ya kukibizi, ulitoa ahadi kwamba mradi ule utakamilika ndani ya miezi mitatu. Mheshimiwa Waziri mradi bado haujakamilika, nashukuru mkandarasi huyo mkataba wake ulikuwa ume-*expire*, tarehe 28.03.2019 Serikali imekataa ku-*extend* mkataba huo na imekabidhi ule mradi kwa MWAUWASA ili waweze kuumaliza.

Naomba Mheshimiwa Waziri uwaambie MWAUWASA waumalize mradi huo mapema sana kwa sababu wananchi wana shida sana ya maji kwenye Kata hii ya Kikubizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kwamba kuna maombi ya mradi wa tenki la kutunza maji Ngudu. Wilaya ya Ngudu ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba lakini tuna matatizo ya maji, wakati KASHWASA wanapofanya matengenezo kwenye tenki ya Mhalo wananchi wa Ngudu wanakosa maji. Tumepeleka maombi Wizara ya Maji kupata tenki ya lita milioni tatu. Mheshimiwa Waziri maombi yako kwenye Wizara yako naomba utusaidie ili wananchi waweze kupata maji ya uhakika Wilayani Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuna mradi wa tenki ya Kizida. Tunaomba pesa kutoka Mfuko wa *PBR* na maombi yameenda siku nyingi yako Wizarani yanasubiri majibu. Tunaomba mradi huo ukamilike kwa sababu ukikamilika Vijiji vya Shikangama, Shilembo, Nguliku, Mwamakelemo, Ilula, Kibitilwa, Mwamapalala vyote vitapata maji. Naomba Mheshimiwa Waziri usikie kilio chetu cha maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Wilaya ya Kwimba ni Wilaya ambayo tabianchi imetuathiri sana, hatuna ziwa wala mito ambayo ina maji ya kudumu tunatemegea visima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mansoor. Tunaendelea na Mheshimiwa Cecil Mwambe dakika 10 atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Bungara dakika 10.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyopo hapa mbele yetu, hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye masuala ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali unavyoiona kama ambavyo Mheshimiwa Mnyika alianza kuongea toka mwanzo kwamba kimsingi kuna hali mbaya sana kwenye suala la maji na Wabunge wote waliosimama hapa wamekuwa wakilalamikia suala hili. Niungane na Mheshimiwa Mnyika lakini pia niungane na hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuitaka Serikali irudi na kufanya marejeo kwenye hii miradi yote ya maji kwa ajili ya kupata *value for money* kwa sababu kuna miradi mingi imesimama na tunaamua kufanya hii kazi kisiasa, tunapeleka pesa kidogo kidogo kwenye maeneo mengi ambayo hayawezi kuleta tija kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru sana wa-*missionary* wa Ndanda kwa sababu bila wao eneo kubwa sana la Mji wa Masasi pamoja na maeneo ya Ndanda tungekuwa na kiu kuu. Kutokana na uvumbuzi wao uliofanywa miaka ya 1960 na marehemu Bruda Lucas, Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi, wametuwezesha kupata maji eneo kubwa, kata nane za mwanzo ambazo ni Ndanda, Mwena, Chikundi mpaka kufikia Kata ya Chigugu pamoja na Kata ya Chikukwe. Tatizo kubwa tulilionalo hapa ni ucheleweshwaji wa uanzishwaji wa mradi huu. Mradi ule umeendelea kutengenezwa pale, tumepokea mabomba tunashukuru lakini pia matenki yameendelea kujengwa kwenye lile eneo pamoja na vizimba kwenye maeneo mengi sana, sasa tatizo mkandarasi anashindwa kuendeleza ile kazi yake kwa sababu hapati pesa kwa wakati kiasi kwamba wananchi wanaanza kukata tamaa na hawajui

kwamba maji wataanza kupata lini kwenye eneo hili. Kwa hiyo, bado mpaka sasa hivi wanahangaika na visima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukumbuke sisi watu wa Ndanda tuna maji mengi tu na nilishwahi kusema hapa hata siku ya kwanza kabisa naanza kuchangia nilisema kwamba tatizo kubwa tulinalo watu wa maeneo ya Ndanda kwenye hizo kata nilizotaja ni miundombinu. Sasa miundombinu imetufikia lakini kazi hii inashindwa kukamilika zaidi ya mwaka wa pili sasa hivi kwa sababu pesa zinapelekwa taratibu. Ni bora hizi pesa zikapelekwa kwa haraka ili ikiwezekana mradi huu ukamilike tuwaondolee kero wale wananchi wa hayo maeneo niliyoyataja ikiwemo pamoja na Maparagwe na Vijiji vya Mbemba na Mbaju. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilisema hapa, Jimbo la Ndanda limegawanyika kwenye jioografia mbili; kuna upande wa Mashariki pamoja na upande wa Magharibi. Upande wa Magharibi miaka ya zamani kama mtakumbuka tulikuwa tuna miradi iliyokuwa inafadhiliwa na JICA na DANIDA. Kwa bahati mbaya sana ukienda Kata za Mlingura, Namajani na Msikisi, maeneo haya yote yalikuwa na miradi mikubwa sana ya maji na maji haya yalikuwa yanatokea kwenye Kata ya Namajani. Pale kuna visima, kwenye vile visima vinatakiwa visafishwe na kuboresha miundombinu kwa sababu mpaka *pump house* ziko pale mpaka sasa hivi, matenki nayo yako pale, kwa hiyo, tunahitaji kuboresha ile miundombinu pamoja na kusafisha visima kwa gharama ya karibia shilingi milioni 300. Nilivyoongea na yule mtaalam wa maji mara ya mwisho alisema hivyo lakini Serikali haijatekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa hapa wanatuletea mipango mikubwa sana wakati sisi tunahitaji maji kwa haraka tuweze kuwasaidia watu wetu. Serikali inawaza kutengeneza mabwawa na niliongea hapa wakati fulani na Mheshimiwa Waziri na nimeona kwenye kitabu hapa, ukurasa wa 79, wametaja na kijiji pekee ambacho tumepata maji siku za karibuni kwa gharama isiyozidi shilingi



milioni 60. Sasa tunawaza kurekebisha mabwawa, kuna Bwawa la Lukuledi na Mihima, tunawaza kutengeneza Mabwawa maeneo ya Chingulungulu, kimsingi maji ya Mbwinji yaliyokwenda Jimbo la Ruangwa, Nachingewa yanatoka Jimbo la Ndanda, Milima ya Nangoo, kwa hiyo, tuna maji mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiomba sisi, badala ya ninyi kufikiria kuhusu kutengeneza mabwawa tupeleke miundombinu ili haya maji yanatopelekwa maeneo hayo niliyoyataja yaweze kufikia eneo kubwa la Jimbo la Ndanda tena kwa gharama nafuu sana tofauti na gharama mnazozifikiria ninyi. Tuwaombe kabisa Serikali kwamba mtakapokuwa mnafanyia kazi miradi hii mtushirikishe sisi wenyeji wa haya maeneo, tunaweza tukawafahamisha, tukawaonyesha vyanzo vizuri zaidi kuliko vile ambavyo ninyi mnafikiria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine liko kwenye Kata yangu moja ya Chiwata. Kata hii kijiografia iko juu kabisa ya mlima ambako tunapaka kati ya Makonde *plateau* pamoja na milima ya upande wa Masasi. Bahati mbaya sana Kata ya Chiwata ndiko ambako iko shule kubwa kabisa ya sekondari na sasa hivi imekuwa *A-level*, shule ya Tija lakini kuna shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati tulifikiri kwa sababu mradi wa madini ulikuwa unaendelea pale na wale wawekezaji walikuwa tayari kusaidia maji kwenye lile eneo, inahitajika kama shilingi milioni 300 mpaka shilingi milioni 400 na Waziri tumeshaliongea jambo hili. Naomba nikusisitize tena, ili tuweze kupata maji safi na salama Chiwata yanayotoka kwenye vyanzo vya maji vya Kambona ambavyo mimi navijua, wewe haujawahi kufika pale, tunahitaji kupata *pump*, tunahitaji pia kutengeneza tenki kwenye maeneo ya Chibya Sekondari ili tuweze kusambaza kwenye haya maeneo yote na hivi ndivyo inatakiwa ifanyike mtushirikishe. Sasa mnawaza kupeleka pale maji sijui kutoka kwenye *source* gani wakati kuna chanzo cha gharama nafuu sana cha maji

ambacho kitasaidia haya Serikali kuweza kubana matumizi kwenye eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mwingine ni wa kupeleka maji kwenye hizo kata nilizokwambia. Kwa mfano, ukisoma kwenye hii taarifa ambayo iko kwenye ukurasa huu wa 29 nilivyoitaja hapa mwanzoni wanaelezea kuhusu Mradi mkubwa sana wa maji ya Mbwinji lakini naomba tu nikutaarifu kwamba huu Mradi wa Maji ya Mbwinji ulikuwa na andiko lake toka mwanzoni kabisa na walisema wataanza kuhudumia wenyeji wa maeneo husika. Sasa hivi naongea na wewe lakini ukienda kwenye Kata za Nanganga pamoja na mradi ambao ulifanyika kwenye eneo hilo kupeleka maji vijiji vyote, mradi uliofanywa chini ya kiwango na mkandarasi yule bado yupo amefanya ubadhirifu mkubwa lakini amekuwa akilindwa na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana hii miradi tumeigeuza kuwa ya kisiasa. Viongozi wa kisiasa kwenye maeneo yetu ndiyo wanaopewa kusimamia miradi hii. Makusanyo yanayopatikana kwenye miradi hii watakapotumia vibaya hakuna mtu anayekwenda kuwahoji hasa wanaotokea kwenye chama tawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mradi wa maji uliopo kwenye Kata ya Nanganga haufanyi kazi kwa sababu tu yule mkandarasi alijenga chini ya kiwango, lile chujio la maji pale limeharibika, halijakarabatiwa na mpaka sasa hivi mradi huo haujapokelewa ambapo tunashindwa kupeleka maji kwenye Kata ya Nanganga kwenye vijiji vya Mkwera, Chipite, Nangoo, Lumumburu pamoja na vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri mnapopata nafasi na nakumbuka Mheshimiwa Waziri Kamwele alipokuja alisema kabisa kwamba Bodi ya Maji inayosimami ile ambayo iliundwa na wananchi kwenye hii Kata ya Nanganga ivunjwe kwa sababu imekuwa ikifanya ubadhilifu na watu wanapohoji viongozi wetu wa Serikali za Mitaa na wengine wanawachukulia hatua ambazo sio stahiki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kweli tuklamua kwa mfano Mheshimiwa Mbunge alietoka sasa hivi anaongea habari ya shida ya maji Kwimba. Kwimba ipo karibu na Ziwa la Victoria wala sio mbali kutoka huko, sasa kama mtu aliyeko Kwimba analalamika kuhusu maji sishangai na watu wa Shinyanga na kwingine wakalalamika kwa sababu kidogo wako mbali na hili ziwa. Kwa hiyo, maeneo yenye vyanzo vya maji tuache kufikiria miradi mikubwa sana twende tukaboreshe ile miradi midogo iliyopo kwenye haya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini tuna tatizo kubwa sana la maji pia kwenye Jimbo letu la Masasi na Masasi ni nyumbani kwangu nina wajibu wa kuwasemea watu wa Masasi. Tuna shida moja tu Masasi wanapewa maji kutoka kwenye watu wa MANAWASA. MANAWASA ndio wanaosimamia chanzo cha maji cha Mbwinji, mpaka sasa hivi ninaongea na wewe ukiangalia kwenye bajeti iliyopangwa huku ndani wanasema watawapelekea maji wote huo mradi unakaribia kukamilika na najua Katibu yuko hapa anasikiliza naweza nikampa maelezo ya ziada baadaye kutokana na muda tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu wazi kwamba mkandarasi ambaye alipelekwa kwenda kufanya tathimini kwa ajili ya kutaka kuanza ule mradi ambao wanasema unakamilika mwezi Juni mwaka huu anashindwa kuendelea na kazi kwa sababu hana pesa ya kufanya hiyo kazi ambayo nyinyi mnasema mlishamfanyia *commission* ili aweze kuanza. Na hii itasaidia kupata maji safi, hata maji tuliyopeleka huko Nachingwea, Maji tuliyopeleka Rwangwa na ndio maji hayo yanayokwenda Masasi. Lakini yanazidi kuwa machache kwa sababu chujio lile sio zuri tena ni dogo liliwekwa kwa ajili ya kuzalisha maji machache pale, sasa tunahitaji kupata chujio kubwa ili tuweze kupata maji safi na salama Masasi na maeneo mengine yote yanayozunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema tuwashukuru sana Wamisionari bila wao huu mtandao mzima wa maji tunaongelea hili eneo la Kata ya Mwena mpaka kufika Kata ya Chikukwe basi kungekuwa kuna shida kubwa

sana. Na maji tunayotumia eneo hili ni safi na salama kwa sababu ndio chanzo cha mwanzo kabisa kabla ya chanzo cha Mbwinji kupeleka maji Masasi, kilikuwa kinatumika chanzo cha Mwena ambako ndiko yanakotoka...ahsante ninaiomba wizara pamoja na kazi nzuri wanayofanya waongeze...

**MWENYEKITI:** Unga mkono Mheshimiwa, mmh maji yatafikaje kama huungi mkono .

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Kambi Rasmi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii leo tarehe 6 Mei. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika katika Bunge hili na afya tele. Tatu natoa pole kwa mfanyabiashara Dkt. Reginald Mengi Mungu amuweke mahala pema peponi huyu Mheshimiwa miaka ya 80 huko tulimuita Kilwa akawa mgeni rasmi ni katika kuchangia elimu Wilaya ya Kilwa alitoa shilingi milioni 20, enzi hizo milioni 20 nyingi sana, kwa hiyo, tunatoa pole za dhati watu wa Kilwa na Ishallah Mwenyezi Mungu amuweke mahali anapostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu 1961 tunapata uhuru mpaka leo miaka 58 Bunge linazungumzia habari ya maji, kila Mbunge anayesimama hapa anasema kwake hakuna maji sio Mbunge wa CCM wala sio Mbunge wa CUF, wala wa CHADEMA. Naomba sana ombi langu kubwa sana katika mfuko wa maji tuongeze shilingi 50 ili yapatikane maji, naona tatizo kubwa ni fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri shilingi 50 iongezwe katika mfuko wa maji ili watu tupate maji. Waheshimiwa maji ndio maisha bila maji kila kitu hakifanayiki kwa hiyo, naomba mheshimiwa Waziri tunawasaidia wafadhili kwamba tutoe shilingi 50 tuingoze

katika mfuko wa maji tafadhali, hilo jambo la kwanza.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili sisi Kilwa kuna miradi ya DCA miradi 17 lakini mpaka sasa hivi vimechimbwa visima vitatu tu tunaipongeza Serikali kwa mfano hivyo visima vitatu vyote vimechimbwa katika Jimbo langu. Lakini katika visima vitatu kisima ambacho kina maji safi na salama ni kisima kimoja tu cha Pande lakini kule Kisongo na Limaliyao visima vyote viwili maji yake ya chumvi na tulisema siku nyingi sana kwamba mazingira ya Limaliyao na Pande tunapenda tuletewe mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema kwamba kule mazingira yake ukichimba maji lazima yawe maji ya chumvi, tunaipongeza sana Serikali Limaliyao wamechimba visima si chini ya sita lakini vyote ni maji ya chumvi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali mabwawa yajengwe katika maeneo hayo ya Limaliyao tunaiomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tunashukuru hiki kisima cha Pande kina maji mengi na mazuri hakina mataatizo kabisa kwa saa moja inatoa lita 14,000. Kwa hiyo, tunachoomba sasa miundombinu yanaweza yakapelekwa maji katika vijiji vitatu katika eneo hilo kwa hiyo tunamuomba Mheshimiwa Waziri Ustadhi Mheshimiwa Profesa Mbarawa oneshwa ujasiri wako ili tupate maji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumepata hela tumeona katika kitabu tumepata hela milioni 300 kwa ajili ya Mji wa mdogo wa Masoko. Lakini Mheshimiwa Profesa kuna Mji mdogo wa Kivinje hakuna bajeti katika mradi wowote wa maji katika Mji mdogo wa Kivinje na Mji mdogo wa Kivinje kuna hospitali ya Wilaya na siku nyingi nasema hiyo hospitali ya Wilaya ina upungufu mkubwa wa maji. Naomba sana Mheshimiwa Profesa uangalieni Mji wa Kivinje ambao una wakati si chini watu 15,000 lakini maji hamna kabisa na hakuna mpango wowote wa maji niliouna katika kitabu hiki ambapo umepangwa mji mdogo wa Kilwa Kivinje isipokuwa Mji wa Kilwa Masoko Alhamdulillah maji yapo na kuna mradi

vile vile unakwenda huko, lakini tunaomba sana Mji wa Kilwa Kivinje upatikane maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna vijiji havina maji machache sana kwa mfano Kata ya Kikole kuna Luwate, kuna Kikole yenyewe, kuna kijiji cha Kisange mbalambala , maji nayo hakuna. Pia kata ya Likawage kuna kijiji kimoja kinaitwa Nainokwe kilikuwa katika mradi wa visima 10 kisima kimechimbwa hakina maji hata kidogo tunaomba nacho kijiji hiko kipatiwe maji, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kijiji cha Mavuji, kijiji cha Mchakama, Kijiji cha Mkondaji katika Kata ya Mandawa navyo maji hakuna lakini nasisitiza sana kuna mradi wa Mavuji ambao mradi huo ulikuwa chini ya Wabeligiji lakini ikaonekana hela ziko nyingi sana, sasa hivi umeingia katika mpango wa msaada wa India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Profesa sana tena sana mradi huo wa Mavuji kama hautafanikiwa matatizo ya maji katika Mji mdogo wa Kivinje, Mji mdogo wa Masoko utamalizika nakuomba sana na kwa kuwa Serikali hii ni sikivu Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni sikivu naamini kabisa kwamba mradi huu wa Mavuji huu tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa Mheshimiwa Dkt. Magufuli sikivu kuna mradi wangu mmoja wa barabara kwa Nkocho Kivinje paka nikaitwa mimi jina langu Nkocho kwa Kivinje, nikamuomba siku moja tu sasa hivi lami ilishakwisha iko moto imekwisha lami, ilishajengwa ni sikivu Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni msikivu. Lakini msimuangushe nakuombe Mheshimiwa Prof. Mbarawa usimuangushe hebu fanya mpango wa maji yawe safi haya ili Mheshimiwa Dkt. Magufuli apate sifa yake hiyo inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo namuomba Mheshimiwa Magufuli kila kizuri kidogo kutakuwa na kasoro kidogo hawa watu wanaotekwa aseme na yeye

kauli aseme kina Mdude hawa nao kukaa kwake kimya kuna...

**MWENYEKITI:** wewe ongelea hoja iliyo mbele yako tu hapa wewe na muda wako.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naendelea na maji.

**MWENYEKITI:** Muda wako ndio huo unga mkono upate maji, Mheshimiwa Bungara unga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli upate maji.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kambi naunga mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge tumejitahidi sana mniwie radhi Waheshimiwa wale ambao hamkuweza kupata dakika zenu 10 kwa sababu ya muda wetu lakini tumejitahidi sana tumewamaliza wote kwenye orodha zetu za vyama.

Tunaporejea hapa saa 11 tutaanza na Waheshimiwa Manaibu Waziri wa Kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI kwa kadri watakavyokuwa wamejipanga kwa dakika 10, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi upande wa barabara dakika 10. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na baadae atakuja Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara yenyewe ya Maji kwa muda usiozidi dakika 20 na baadaye sasa mtoa hoja ahitimishe hoja yake kwa muda usiozidi saa moja, baadaye tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi kwenye shughuli pevu.

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni leo.

*(Saa 6.53 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa niliwataja wachangiaji wetu. Naibu Waziri Ujenzi, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mungu kwa nafasi hii, lakini nawapongeza Wizara ya Maji. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa, nampongeza Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya, pia nawapongeza watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Kwa kweli, maji ni uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu sisi katika Wizara ya Ujenzi tunapokuwa na miradi ya ujenzi wa barabara, tunahitaji kutumia maji kwa wingi. Kwanza sisi wenyewe kama sehemu ya kukamilisha miradi tunatumia maji, tunahitaji maji ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojenga barabara, madaraja makubwa, madaraja madogo, ma-*calavat*; pia tunapotengeneza madaraja haya ili kuweza kupitisha maji, maana iko mito midogo, mikubwa na iko mito ya msimu na ambayo inapitisha maji muda wote, tunahitaji maji katika kazi ya ujenzi kwa wingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ili kushindilia barabara zetu zikae vizuri, maji yanatumika; ili kuweka zege katika maeneo mbalimbali, maji yanatumika; ili kuhakikisha kwamba barabara inakuwa *stable*, tunafanya *curing* kwa maana kwamba tunamwagilia maji na maji yanatumika kwa wingi sana. Kwa hiyo, upatikanaji wa maji huwa ni kigezo cha kupunguza au ku-*control* gharama za ujenzi wa barabara. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukifanya shughuli za ujenzi wa barabara huwa tunawaelekeza makandarasi waweze kutengeneza au kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji ili kukidhi mahitaji ya shughuli za ujenzi. Kazi hii ikikamilika, mabwawa haya hubaki na maeneo mengi tunatumia mabwawa haya yaliyobaki baada ya shughuli za ujenzi kwa shughuli mbalimbali za maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, muda wote tunahitaji ku-*manage* maji ili tuweze pia kupunguza shida kubwa ya maji ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo ambayo pia tunachimba vifusi, tunachimba udongo ili kuweza kukamilisha shughuli za ujenzi wa barabara na baada ya ujenzi kukamilika na sisi kama Wizara hutoa mchango mkubwa wa kuhakikisha kwamba maeneo haya, hizi *ball pits* tunazifanyia marekebisho makubwa, tunazichonga vizuri ili ziweze kutumika kwa maeneo ambayo mahitaji ya maji ni makubwa sana. Kwa hiyo, huu utaratibu tunaufanya ili na sisi kutoa mchango katika kuhakikisha kwamba maji haya na hizi *pits* zinazobakia zinaweza kutumika kwa ajili ya kutoa huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mbele ya Bunge lako hili kwamba uko uwezekano mkubwa wa kwamba sisi kama Wizara pale tunapotambua kuna mahitaji ya maji kwa wingi kiasi gani katika maeneo miradi ya barabara inapita tunazingatia kuanzia kwenye hatua ile ya usanifu tunaweka *provision* ili nasi tuweze kutoa mchango kwenye maeneo ambayo miradi ya barabara inapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kwamba sehemu ambayo tutakuwa na miradi kuanzia kwenye hatua ya usanifu watoe ushirikiano, watupe taarifa, lakini ninajua pia wako wadau wengine katika maeneo yetu, wakurugenzi na wananchi wenyewe wakitupa taarifa ili na hii fursa tuweze kuitumia na sisi kuendelea kupunguza adha ya maji ambayo yanahitajika kwa ajili ya shughuli za kibinadamu mbalimbali, shughuli za kilimo na pia kwa ajili ya kunyweshea wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mifano ya miradi ambayo kwa ufupi tu niitaje. Baada ya miradi ya barabara kukamilika tumeacha huduma za maji kwa ajili ya kumbukumbu. Ukiangalia barabara ya kutoka Tabora – Puge kwenda Nzega yako maeneo mengi ambayo tumeacha mabwawa na sehemu nyingine tumeweka huduma ya maji. Barabara hii kutoka Nzega – Tinde kwenda Shinyanga kadhalika tunayo mabwawa ambayo yamebakia kandokando ya barabara, tunaendelea kuhudumia maji; barabara hii kutoka Nzega – Igunga – Shelui na penyewe yako maeneo ambayo tumeweka huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa maeneo pia ambayo yanazunguka kwenye Mji huu wa Dodoma kwa Barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida, yako maeneo ambayo yanahudumia wakazi wa Dodoma na wakazi wengine wa Singida, tumeacha mabwawa ya maji. Ukiangalia pia, hata barabara kuu kutoka hapa Dodoma kwenda Morogoro, Dodoma – Kondoa – Babati, Dodoma – Iringa yako maeneo ambayo tumeweka huduma za maji. Kwa hiyo, nilitaka niseme tu kwamba fursa zipo kila wakati tupate hizi taarifa kuhusu mahitaji sahihi ya watu na sisi tutaendelea kutoa msaada wa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunachimba visima kama sehemu ya *social responsibility*. Uko mfano, ukienda Kaliua kule kuna visima vitano tumechimba. Pia viko visima vingi kwa sababu, miradi ya barabara ni mingi, yako maeneo mbalimbali ambayo kama sehemu ya *social responsibility* tunatoa huduma kupitia wakandarasi wanaofanya shughuli hizi ili kuweza kutoa mchango mkubwa kwenye huduma za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilitolewa hapa kwamba maji yanapotea katika maeneo mbalimbali. Hii ni kweli, tunapokuwa tumetengeneza ma-*calavat* na madaraja madogo, madaraja makubwa na pia kwenye hizi *ball pit* kuna maji yanapotea, kwa sababu, hatujajipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunayatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kutumia maji haya, siyo kazi ya Serikali peke yake, ni kazi yetu sisi wote. Wote tunao wajibu wa kushirikiana kuhakikisha kwamba tunayazuia maji haya yanayopotea kwa kiasi kikubwa kuliko maji yapotee halafu wananchi wana shida ya maji. Tukishirikiana kwa pamoja tutawahudumia vizuri wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwasihi na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na kwa sababu pia, ziko mamlaka, *TANROADS* inajenga barabara, *TARURA* tunajenga barabara, lakini pia iko fursa ambayo tumepewa kupitia Bodi zetu za Barabara katika mikoa ambapo Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe; Wakuu wa Wilaya ni Wajumbe; wako pia Wenyeviti wa Halmashauri zetu za Manispaa na Majiji nao ni Wajumbe kwenye bodi hizi za barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa tunashiriki kwenye vikao hivi, basi mahitaji yetu, mipango yetu tuiweke kwenye bodi hizi ili nasi tuwe na sehemu nzuri ya kuchukua mahitaji haya. Kwa sababu kama nilivyosema, fursa ya kuendelea kutengeneza mabwawa haya yawe makubwa kulingana na mahitaji, nasi kama Wizara, uwezekano wa kutoa huduma hii ya maji upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane ili sasa tukishatambua mahitaji yetu, kuliko kuyaacha maji yapotee, tunaweza sasa tukayatumia haya maji ili kuweza kuwahudumua wananchi sehemu mbalimbali. Kwa sababu tukiacha maji yakaenda, kwanza yanapotea bure, lakini tusipoya-*manage* pia yanaharibu makazi ya watu, yanaharibu mashamba na hata barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiona kama kuna vitu ambavyo vinahitaji na sisi tuvijue tuweze kuyatumia vizuri haya maji, nawaomba wote tushirikiane na wananchi, Waheshimiwa Wabunge na viongozi mbalimbali kwenye maeneo yetu tuweze kupata taarifa hizi ili sasa maji haya yaweze kutusaidia kuendesha shughuli mbalimbali za

kibinadamu, yatumike kwa ajili ya mifugo na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa na hayo kwa ufupi. Naomba sana katika hatua zote, kuanzia hatua za usanifu, pale tunaposanifu barabara huwa tuna-*involve* watu walio kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, hata tukiona kuna mradi wa usanifu unaendelea na kama tuna mahitaji ya maji, ni hapo naomba sasa tushirikiane ili mtuletee sasa mahitaji haya kwa pamoja tuyaingize kuanzia kwenye hatua za mwanzo ili saa hizi *facility* za mabwawa na sehemu ambazo maji yanapita na sisi mchango wetu uwe mkubwa kuhakikisha kwamba tatizo hili kubwa ambalo Mheshimiwa Profesa Mbarawa hapa anapambana nalo kupunguza shida ya maji, nasi kama Wizara ya Ujenzi tuko tayari kushirikiana na Wizara ya Maji ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuko tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge ili maeneo yetu ambayo yana-*demand* kubwa ya maji na sisi kama Wizara ya Ujenzi tuendeleo kutoa mchango wetu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja iliyo mbele yetu asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako na ushauri wako mzuri. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI. Mheshimiwa Kandege, una muda usiozidi dakika 10.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kuunga mkono hoja. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao walipata fursa ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango imetolewa na Waheshikiwa Wabunge, mingi ikiwa ni ya kujenga. Nasi sote ni mashuhuda kwamba maji ni uhai, tuna uhitaji wa maji na tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba maji yanawafikia Watanzania wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambapo ukienda huko ndiyo unakutana na wananchi ambao wanahitaji maji, hakika tunaamini katika jitihada ambazo zimewekwa na Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kwamba tunaenda kumtua ndoo mwanamama, ni ahadi ambayo tumeahidi kwa llani yetu, nasi tukiahidi huwa tunatekeleza. Kwa hiyo, naamini kwa siku ya leo tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba tunaunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, kuna maneno yamesemwa mengi kwamba kiasi cha fedha ambacho kinatolewa hakitoshi. Ni vizuri pia tukajiridhisha kwamba katika hicho ambacho kinatolewa kiende kikafanye kazi iliyokusudiwa. Kwa sababu hajalishi kiasi cha wingi wa fedha kama *management* yake isipokuwa nzuri; hakika hata kingekuwa kingi namna gani hakiwezi kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu na hasa katika utaratibu wa uanzishwaji wa mamlaka ya maji; hapa katikati na wewe ni shuhuda, wakati mwingine ilikuwa tunatupiana mpira, inaonekana hili liko TAMISEMI, hili liko Wizarani, kiasi kwamba sasa ukitaka kufuatilia kujua *exactly* ni nani ambaye amesababisha wananchi wetu wasipate maji wakati mwingine ilikuwa inatuwia ugumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wetu huu wa kuanzisha mamlaka hii, nawe ni shuhuda, pale ambapo tumeanzisha *agency* kama *TARURA* inakuwa ni rahisi kujua *exactly* nani awe *responsible* na awe *answerable* na kila mtu abebe msalaba wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini na kwa bahati nzuri sisi kama TAMISEMI tuna utawala mpaka kijini na kwa sababu Serikali hii ni Serikali moja, kinachofanyika ni kuhakikisha tu kwamba tuna-*mainstream* ili ijulikane nani anafanya nini, lakini kwa sababu lengo ni kumfikishia mwananchi wa kawaida huduma ya maji, naamini na fedha hizi ambazo zimepatikana na hii *agency* ndiyo imeanza hivi karibuni, naomba tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla na Uongozi wa Wizara ya Maji ili tukasimamie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu naamini mbele ya safari baada ya hiki ambacho kitakuwa kimetolewa, kikionekana kimesimamiwa vizuri hakijatoshwa, sasa hoja itakuwa ina mashiko kwamba sasa tuongezee fedha zaidi kwa sababu tuna uhakika juu ya usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami na wewe mwenyewe ni shuhuda, hatuna wasiwasi juu ya uongozi na bahati nzuri kuna mamlaka za maji kila mji. Naamini hakika fedha hii ambayo itaenda kutolewa itaenda kukidhi haja ya kuhakikisha kwamba maji yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shuhuda, wakati fulani ilikuwa ukianza kutafuta fedha unaambiwa nyingine zimeenda Wizara ya Elimu, nyingine zimeenda TAMISEMI, kiasi kwamba unashindwa kuzi-*trace* kwa ujumla wake, lakini sasa hivi kwa utaratibu huu ambao umeanzishwa hakika Profesa atakuwa na uhakika wa kusimamia kila shilingi na itakuwa ni rahisi kwake yeye kuweza kuwawajibisha wale wote ambao watakuwa hawatimizi malengo ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba niendeleo kuunga tena mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Tunaendelea na

Mheshimiwa Sima, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini pia niungane na Wabunge wenzangu kwamba sasa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. Pia, nampongeza kaka yangu Katibu Mkuu wa Wizara hii, Profesa Kitila Mkumbo na watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza mazingira bila kutaja uhifadhi wa vyanzo vya maji, maana yake mazingira yatakuwa hayajatimia. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge na ni ukweli usiopingika kwamba wameongea kwa hisia kubwa sana juu ya uhitaji wa maji na hili ni jambo jema sana. Mjadala huu unatuonesha picha ni nini ambacho Serikali tunapaswa kukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna vita itatokea duniani leo itakuwa ni vita ya kugombania maji. Kwa bahati mbaya sana Tanzania inaweza ikawa nchi ya kwanza ya kuathirika na vita hii. Kwa nini? Asilimia 35 ya maji safi na salama duniani yanapatikana Tanzania. Tunayo maziwa makubwa, tunalo Ziwa Viktoria, Ziwa Tanganyika na maziwa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayojitokeza hapa ni namna ya kuhifadhi vyanzo vya maji na hili ndiyo jukumu letu. Hata kwenye mjadala ukiuskiliza, wote tunazungumzia *water supply*. Sasa una-*supply water* wakati unajua kabisa hujahifadhi vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niliseme hili kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba jukumu la kuhifadhi vyanzo vya maji ni jukumu la kila Mtanzania, siyo jukumu la Serikali peke yake. Eneo hili linahitaji tushirikiane

kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunahifadhi vyanzo vya maji ili tuweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejitahidi sana kupeleka fedha za kutosha, inapeleka fedha za mradi, lakini mradi kwenye maeneo mengine hata kwangu kule Singida wanaenda kluchimba wanakosa maji na *geological physical survey* imefanyika inaonesha kwamba hapa kuna maji. Watakapochimba tu wakaenda hata mita 200 wanakosa maji. Hapo ndiyo kwenye changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayojitokeza hapa ni uhifadhi wa vyanzo vya maji ambalo hili ni jukumu letu kuwaelimisha watu wetu, tukirudi kuitaka Serikali itupatie fedha za miradi, tuwe tumetoa elimu ya kuhakikisha watu wetu wanajua namna ya kuhifadhi vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi nyuma mwaka 1961 Watanzania walikuwa takribani milioni 10, ukiweza kugawa unapata mita za mraba kama 7,862, lakini leo milioni 55 Watanzania mita za mraba unapata kama 2,300. Vyanzo vya maji ni vilevile na vingine toka mwaka 1961 vimeshakufa na leo vyanzo vinaendela kufa. Maana yake tunakoelekea ni kwenye vita kubwa ambayo tutashindwa kukabiliananayo. Vita hii inatuhitaji sisi wote Watanzania tuungane kwa pamoja, tusiachie Serikali peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya ziara kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuangalia vyanzo vya maji vya mito mikuu mitatu; Mto Luengo nimeenda kule Namtumbo, nimepanda ile milima zaidi ya kilometa 10, nimeenda kuona chanzo cha maji. Kwenye chanzo cha maji pale hakuna tatizo, lakini inapoanzia pale kwenda maeneo mengine, maji kote njiani Watanzania wanafanya shughuli za kibinadamu na eneo hilo lote wame-*tap* maji wanayatumia kwa wingi kiasi kwamba maji yale kule yanakotoka mpaka yanakofika, yamepungua kwa kiasi kikubwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mto Ruaha Mkuu kuna shida kubwa sana. Watu wamevamia kwa kiwango kikubwa. Hili ni eneo ambalo tunahitaji sisi Watanzania tushirikiane kwa pamoja kulisimamia. Hivi vyanzo vya maji tusipovisimamia hapa tutakuja kudanganyana. Tukizungumza lugha ya *water supply* peke yake na Serikali kweli ikawa na fedha ikapeleka, unapeleka fedha unaenda kuchimba maji wakati hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la mazingira nilitaka niwaombe Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kwa pamoja. Tunayo fursa na tunayo nafasi kwenye mikutano yetu ya Majimbo ya kuwaeleza Watanzania kwamba tunahitaji kutunza vyanzo vya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna fedha ya miradi mbalimbali inayopelekwa na Serikali kwenye Halmashauri zetu. Tusiposimamia kuanzia hatua ya kwanza mpaka ya mwisho na baadaye tunaenda; hapa umesikiliza mjadala wa Waheshimiwa Wabunge, mijadala mingi inasema mradi umeenda umeisha, shilingi milioni 500 zimeenda, lakini hakuna maji. Jukumu ni la nani? Wizara imepeleka fedha. Fedha tunatakiwa tuzisimamie sisi, ndiyo wajibu wetu na kuwaelimisha watu wetu. Kamati za Maji zishirikishwe kuanzia *initial stage*. Hili ni jukumu letu kule chini. Hili eneo nilitaka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tusibaki tu kulalamika na tukaiachia Serikali ikasimamia mpaka kule chini. Huu ni wajibu wetu na hatuwezi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine Serikali imeweka mkakati mzuri sana. Yako maeneo iko miradi ya nyuma ambayo tayari miradi ile ime-*collapse* kwa uzembe wa watendaji na kwa uzembe wa kutokushirikisha jamii. Mkakati huu uliowekwa uwe mkakati ambao unahitaji na sisi kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la mita 60, mita 500 limezungumzwa; eneo hili sisi kwenye Sheria yetu ya Mazingira mwaka 2004 kifungu cha 57(1) kimezungumza mita 60, lakini kifungu cha 57(2) kimeeleza ufafanuzi kwamba Waziri

anayo dhamana ya kutengeneza kanuni za mita 60 itumikeje. Nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba kanuni tayari zipo na hazielekezi moja kwa moja, kila mazingira yana tofauti yake; kuna eneo ambalo halihitaji mita 60, mengine yanahitaji mita 10 tu, tukapanda miti mita 10 kuhifadhi kile chanzo cha maji lakini mita zingine wakaweza kuzitumia ama mita 20. Kanuni tumeziweka wazi na hatuna muda mrefu kanuni hizi zitafika mpaka kwenye *Local Government* kuhakikisha kwamba suala hili linaweza kusimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengi tunaweza kuzungumza juu ya uhifadhi wa maji, maeneo haya yote hasa visima ukizingatia visima hivi ambavyo vimechimbwa na wadau mbalimbali; mdau akishachimba kisima watu wanaamua kuacha kiendeleo. Jukumu la kutunza visima na jukumu la kutunza vyanzo vya maji ni jukumu letu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na haya ya kuweza kushauri/kuwashauri wenzangu na kuunga mkono bajeti. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa na Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sima. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso, una muda usiozidi dakika ishirini.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kushiriki katika Bunge lako Tukufu. Kwa namna ya kipekee nimshukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu na Waziri Mkuu kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa sisi Wizara ya Maji katika kuhakikisha tunatimiza majukumu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nimshukuru mke wangu mpenzi Kauthar Francis na mama yangu kwa malezi na matunzo wanayonipa, Waswahili wanasema, usione vyaelea ujue vimetunzwa. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wifu yenu yupo vizuri na ndiyo maana nami nipo vizuri katika utendaji wangu wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nimpungeze sana Mheshimiwa Waziri wangu Profesa Makame Mbarawa, huyu ni jembe wembe. Ukiachana na Uwaziri wake lakini amekuwa mlezi katika kuhakikisha maagizo na maelekezo anayotupa katika Wizara yetu ili yawe na tija na kuleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Maji. Mheshimiwa Waziri ahsante sana, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, sisi hatuwezi kufanya kazi peke yetu, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu Eng. Kalebelo, Wakurugenzi wote na watendaji wa Wizara ya Maji; tumekuwa tukifanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana. Pamoja na changamoto tunazopitia lakini bahari kubwa ndiyo inayovukwa, tutaivuka katika kuhakikisha tunawaletea maendeleo makubwa sana Watanzania katika sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii sana kumpongeza Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kazi nzuri, mapendekezo na ushauri wao lakini pia Waheshimiwa Wabunge wote na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa michango yao, tumeipokea na tutaifanyia kazi. Tumepata bahati ya kipekee kuona Wabunge kila aliyesimama ametoa mawazo, amezungumzia suala la maji na namna gani tunaweza kuboresha Wizara yetu katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Nataka niwahakikishie Wabunge sisi kama viongozi wa Wizara hatutokuwa kikwazo katika kuhakikisha Watanzania waishio mijini na vijijini wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kujibu hoja; moja ya michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni suala zima la ubadhirifu wa fedha za miradi na usimamizi wa miradi ya maji. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alivyoniteua nikiwa kama Naibu Waziri wa Maji tulipeana mikakati pamoja na watendaji wote, Katibu Mkuu na Waziri kwamba tupite maeneo yote ambayo tumepeleka fedha za miradi ya maji hususani maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupa sisi viongozi wa Wizara ya Maji kubaini changamoto kwenye eneo la maji vijijini. Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakijua miradi ya maji kuliko hata Wahandisi wetu wa Maji, lakini wamekuwa wakitoa *solutions* za kutosha. Niseme tu itoshe kwamba Waheshimiwa Wabunge wametusaidea kuokoa miradi mingi ya maji katika eneo la vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya ziara Mbeya Vijijini kwa Mheshimiwa Oran Njeza, tulivyofika pale Mhandisi wa Maji alitupa taarifa ya miradi iliyotekelezwa katika miradi ya maji, lakini nami nikawa na taarifa yangu, baada ya kutupa taarifa nikamwambia nipeleke Mradi wa Galijembe ingawa hakutupa katika taarifa yake. Mhandisi yule wa Maji ananiambia Mheshimiwa Waziri kule eneo unapotaka twende kuna miinuko mikubwa utachoka, nikamwambia hapa sisi tumekuja kufanya kazi, tupeleke Mradi wa Galijembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mvutano mkubwa sana, tulivyofika katika eneo la Mradi ule wa Galijembe, mradi zaidi ya milioni 290 Mkandarasi amelipwa 260 hayupo *site* zaidi ya miaka mitatu. Unamuuliza Mhandisi wa Maji, mkandarasi yupo wapi, anasema Mheshimiwa huyu ni msumbufu huu mwaka wa tatu tukimwandika barua haji. Nikatoa agizo kwamba kesho lazima aje katika eneo la mradi. Kweli alivyokuja tukamuuliza mkandarasi nikiwa na Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, unawezaje kulipwa fedha za miradi ya maji ilhali hujatekeleza? Mkandarasi ananiambia

Mheshimiwa Naibu Waziri tusipoteze muda, mimi nataka kikao chako kiwe kifupi, fedha tumelipwa lakini hizi fedha tulizopewa tumegawana na Mhandisi wako wa Maji; kama nalipwa *certificate* ya milioni 20, milioni 10 yangu na 10 yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuishia hapo, nilikwenda Shinyanga Vijijini katika Mradi wa Mwakitolyo, zaidi ya 1.4 billion, fedha zote zimelipwa za mradi huu wa maji, lakini unafika pale katika eneo la mradi wa maji unakagua, unakuta maji hayajapanda hata katika tenki, unamuuliza Mhandisi wa Maji fedha zimekamilika zote mkandarasi amelipwa, kwa nini maji hayapandi? Ananiambia Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nikunong'oneze; nikamwambia hapana toa taarifa kwa wananchi watuelewe. Ananiambia Mheshimiwa Naibu Waziri sijawahi kuona kijiji wachawi kama hawa, tumetandika mabomba usiku yanapaa kama *bombardier*, hatuwezi tukawa na Wahandisi wa Maji kama hawa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo ya ajabu, hii siyo stori, lakini kutokana na changamoto hizi tulizoziona, sisi kama Wizara ya Maji tukakumbuka maneno ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli pale Ikulu alituambia sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji, anatupa Wizara ya Maji wananchi wa Tanzania waishio mijini na vijijini wapate maji safi na salama, tukishindwa kuifanya hiyo kazi atatutumbua. Sisi kama Viongozi wa Wizara ya Maji hatupo tayari kutumbuliwa, hawa wahandisi wa namna hii hawana nafasi katika Wizara yetu ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtatusamehe hawa wahandisi baada ya maelezo haya, tuliwabeba wazima wazima, mpaka hivi sasa wanaendelea na kesi mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la utekelezaji wa miradi ya maji ukiachana na fedha, wataalam wetu baadhi yao walikuwa siyo wazalendo. Sisi tulikaa na viongozi wa Wizara tukaona haja ya kuunda Kamati Maalum ya watu 10 ambayo inaongozwa na Profesa Mbwete, kukagua miradi

yote ya vijijini na kuona changamoto yake ili tuje na mapendekezo ambayo tutaweza kutatua changamoto hii. Profesa Mbwete alifanya kazi hii kubwa, lakini akabaini kuna changamoto 17 ambazo zinatukabili sisi katika Sekta ya Maji Vijijini. Alikuwa na mapendekezo 50 katika kuhakikisha sisi tunayatatia ili mwisho wa siku sekta hii ya eneo la vijijini liwe linafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mapendekezo ambayo amekuja nayo Profesa Mbwete ilikuwa kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini na ndiyo maana sisi kama Wizara ya Maji tukaja katika Bunge lako Tukufu na tukawaomba Waheshimiwa Wabunge ili waweze kutupitishia Muswada ule ili wale Wahandisi wa Maji waje katika Wizara yetu ya Maji. Nataka niwaambie Wahandisi wa Maji nchini popote walipo, kuna Mheshimiwa Mbunge hapa alichangia katupa stori ya *movie* Fulani, akasema kwamba *we will meet again*, nataka niwaambie Wahandisi wa Maji *we will meet again*. Sisi tutakutana nao, lakini kwa kuwa wametupa rungu, sisi kama viongozi wa maji hatuna kisingizio kingine tena, tutawashughulikia katika kuhakikisha tunaleta nidhamu katika Wizara yetu ya Maji na tuweze kuleta matokeo chanya kabisa katika sekta yetu ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha msingi, pamoja na changamoto hizo zote ambazo tumezibaini, tumefanya kazi kubwa na kazi nzuri ya baadhi ya wataalam wetu. Leo ukienda kwa Mheshimiwa Mwakajoka pale Tunduma tuna mradi mkubwa na ndiyo maana Mheshimiwa Mwakajoka anakubali kazi tunayoifanya. Ukienda kwa Mheshimiwa Haonga kwake pale Mlowo, tuna mradi mkubwa tumeutekeleza na wananchi wake wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ukienda Chunya na maeneo mengine yote miradi ambayo tumeianza, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge, hakuna *single cent* itakayopotea, sisi kama viongozi kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge tutasimamia miradi hii ili iweze kuleta tija na maana kubwa kwa wananchi wetu. Maji hayana mbadala, maji siyo kama wali, ukikosa wali

utakula ugali, ukikosa ugali utakula makande; ukikosa maji utapata maradhi. Sisi ni Wizara ya Maji siyo Wizara ya ukame, tutahakikisha Watanzania waishio mijini na vijini wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ililetwa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa suala zima la madai ya wakandarasi. Tunajua kabisa kwamba kulikuwa na kusuasua kukubwa sana wa baadhi ya miradi, kwamba wakandarasi wamefanya kazi lakini hawajalipwa. Nikiri tulikuwa na madai zaidi ya bilioni 88 ambayo tunadaiwa na wakandarasi, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ya Fedha, mpaka ninavyozungumza tumeshapata zote bilioni 88 na tumeshawalipa wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumewalipa wakandarasi wao, *certificates* zipo na tutawapa orodha ya wale watu tuliowalipa. Sisi jukumu letu ni kusimamia na miradi iendelee kufanya kazi na sisi kama Viongozi wa Wizara ya Maji tunaomba bajeti yetu watupitishie ili twende tukasimamie fedha zile na zilete miradi mikubwa kabisa katika kutatua changamoto hii ya suala zima la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imeletwa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa manung'uniko ya suala zima la ulipaji wa vibali, kwa maana ya umilikaji wa visima, kwamba mtu amechimba kisima kwa fedha zake mwenyewe na pale kulikuwa na changamoto ya maji, lakini anatakiwa alipe kibali lakini alipe ada kila mwaka. Hii ni changamoto, sisi kama viongozi wa Wizara tumeiona, tunakwenda kubadilisha kanuni zetu na tunaziwasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge ili tuondokane na changamoto hii katika kuhakikisha Watanzania hawapati tabu katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maneno mengi sana, Mheshimiwa Profesa yupo hapa, atazungumza kwa kina. Sisi tunachotaka kusema Mheshimiwa Profesa anafanya kazi

nzuri, sisi tutakupa ushirikiano wa dhati kabisa katika kuhakikisha tutatatua tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyokuja, kuona kwamba kuna baadhi ya wananchi wanaishi katika vyanzo vya maji. Leo kuna Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, lakini wananchi wa maeneo yale hawapati maji. Sisi kama Wizara tumeliona na tumeagiza tufanye usanifu unaendelea katika kuhakikisha tunabuni miradi ili wananchi wale wa pembezoni waweze kupata maji na kutumia rasilimali muhimu iliyokuwepo. Nataka nimhakikishie Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Mzee Ndassa ukisoma Tenzi za Rohoni zinasema unapotembea na kuzuru wengine naomba usinipite Mwokozi, hatutokupita pale Sumve katika kuhakikisha unapata maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba nimalizie kwa kuzungumza na kaka yangu Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, Mheshimiwa Mnyika. Miaka ya nyuma kabla mimi sijaja Bungeni nilikuwa mwanafunzi, alikuwa unajenga hoja kuhusu suala zima la uboreshaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, hali ilikuwa mbaya sana Dar es Salaam. Kulikuwa na mabomba ya Mchina yalikuwa hayatoi maji, nilimfahamu kwa kusimamia hoja yake, namheshimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya kazi kubwa sana, *Quran* inasema *waamma biniimati rabbikka fahaddith*, zielezeeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru. Serikali imefanya kazi kubwa sana, leo eneo la Kibamba zaidi ya kilometa 360 tumezitandika katika kuhakikisha wananchi wa Kibamba wanapata maji. Leo hii ninavyozungumza wananchi wa Kibamba walikuwa wanapata maji kwa saa nane, lakini sasa hivi kwa saa 24. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na hayo, Mheshimiwa Mbunge ni shahidi kwa kuwa ana macho; tuna mradi tunautekeleza Matosa, Hondogo, King'azi A na Mbezi Makabe. Mheshimiwa Mnyika nini au tukupe donda ufukuze nzi? Tunatambua kabisa Mheshimiwa Mnyika maji yamekuwa



na uhitaji mkubwa sana lakini sisi kama viongozi wa Wizara tunaendelea kuwaagiza DAWASA kutenga asilimia 35 kwa mapato ya ndani kuhakikisha tunayafikia maeneo ambayo hayajafikiwa na maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Aweso kwa mchango wako. Sasa nimwite mtoa hoja mwenyewe ahitimishe hoja yake, Profesa Makame Mbarawa, una muda usiozidi dakika 60.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele yenu tena na kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe mwenyewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaoonesha katika kuliendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali.

Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia hoja yetu iliyowasilishwa hapa Bungeni. Kwa kweli michango ni mizuri na imejaa hekima kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango na changamoto nyingi zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu Sekta ya Maji. Hii ni kwa sababu Sekta ya Maji kama tunavyofahamu maji ni uhai, maji ni afya, maji ni kilimo, maji ni uchumi, maji ni viwanda, maji ni ustaarabu na maji ni kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imechangiwa na wachangiaji 173 ambapo wachangiaji 59 wamechangia kwa maandishi na wachangiaji 88 wamechangia kwa kuzungumza. Kama nilivyosema hapo mwanzoni, michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa ni mizuri sana na ilivyosheheni mapendekezo, ushauri, busara na namna bora ya kuendeleza Sekta ya Maji.

Aidha, siyo rahisi kujibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa kina na kutosheleza kwa muda huu mfupi nilionao. Naahidi kwamba hoja zote tutazichukua, tutazifanyia na tutazijibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo nitaanza kujikita ni usimamizi wa miradi. Naamini kwamba changamoto namba moja sasa hivi ya Wizara ya Maji ni usimamizi wa miradi. Tumekuwa na changamoto kubwa ya usimamizi wa miradi ya maji na changamoto hii imeanzia Halmashauri kwa *Engineer* wa maji, ikaja kwa *Engineer* wa Mkoa mpaka ikafika Wizarani, ni changamoto kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii kuna maeneo mawili; eneo la mwanzo la usimamizi linahusiana na viwango na ubora wa miradi. Changamoto hii ni kihistoria, ilianza toka mwaka 2010; miradi mingi iliyojengwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ilijengwa kwa viwango vya chini. Miradi hiyo ilitekelezwa kati ya mwaka 2010 – 2015, tume nyingi zimeenda kuchunguza miradi hii na imethibitisha kwamba miradi hiyo ilijengwa chini ya viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya kipindi hicho ndiyo yenye changamoto ambazo sasa tunapambana nazo na ni lazima tuna jukumu na tumepewa jukumu la Tanzania lazima tutatue tatizo hili na tuwapelekee Watanzania maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyoanza kujengwa mwaka 2017 kwa kiasi kikubwa changamoto hizi zimepungua. Hii imetokana na ufuatiliaji wa karibu sana wa viongozi wa Wizara ya Maji, ninyi nyote mmekuwa mashahidi, kila leo mnaona viongozi wa Wizara ya Maji wanatembelea maeneo mbalimbali ya nchi yetu kuangalia miradi ya maji. Nawashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote kwa kufanya kazi hii ya kuhakikisha kwamba miradi ya maji tunayojenga inaenda kwa viwango vinavyokubaliwa ili Watanzania waweze kupata maji safi na salama, hilo eneo la mwanzo ambalo kwa kiasi kikubwa sasa hivi wakandarasi wameanza kuogopa na tumeweza kwenda nao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ni tatizo na bado ilikuwa ni changamoto ni gharama halisi ya miradi ya maji. Gharama ya miradi ya maji iko juu sana, huku ndiko wakandarasi wengi wanakojificha na kupiga pesa za Serikali. Hii inafanywa kwa ushirikiano mkubwa kati ya wakandarasi wetu, Halmashauri, Wakurugenzi, Wahandisi wa Maji Mikoani, Wahandisi wa Maji wa Wizara ya Maji yenyewe, Idara ya Manunuzi, Wizara ya Maji pamoja na Mfuko wa Maji. Kumekuwa na mtandao mkubwa sana ambao unaanzia kule kwenye Halmashauri, Mkoani hadi Wizarani, hili jambo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mtandao huu, Wahandisi wetu wa Maji wa Wilaya wanatengeneza *engineering estimation* au makisio ya kihandisi ambayo si sahihi, wanaweka gharama za juu. Ubaya zaidi wanajaribu kuwapa wakandarasi wazijue kabla ya tenda. Hili ni jambo baya, siyo uadilifu na halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano miwili ambayo ipo ambayo inaonesha jinsi gani pesa za Serikali zinaliwa kwa mtindo huu. Sitataja jina la mradi lakini kuna *Project A (Mradi A)*, mradi huu ulitangazwa, mkandarasi akaomba na akatoa bei yake ni shilingi bilioni 4.5. Sisi baada ya kupitia mradi huu vizuri tukaona unaweza kujengwa kwa bilioni shilingi 2.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchambua vizuri, nikiwaonyesha hapa, hii ndiyo bei ya mkandarasi nah ii ndiyo bei tuliyofanya uchambuzi wetu, baada ya kupitia tuliona kwanza kwenye mabomba alisema bei ya mabomba ni shilingi bilioni 2.77, sisi baada ya kufanya utafiti tukaona bei ya bomba ni shilingi bilioni 1.13, karibuni mara mbili. La pili, tumeenda tena tukaangalia baadhi ya maeneo kwa mfano ujenzi wa tenki yeye ame-*quote* milioni 488, sisi tuka-*quote* milioni 771. Sasa huku ndiko wakandarasi wengi wanakopiga pesa na mtandao huu unaanzia Halmashauri mpaka Wizarani. Watu wengi wanapiga hela kwa kutumia utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza hapo mkandarasi huyu tukasema hatufai. Tulilofanya tukasema sasa pesa ile ambayo tulikuwa tumpe mkandarasi huyu tutumie utaratibu wetu sisi tukajenge kazi hiyo hiyo kwa shilingi bilioni 2.5 ama 2.6 lakini pesa nyingine tupeleke kwenye miradi mingine, kwa mfano tujenge mradi wa Kamwanda kule kwa Mheshimiwa Serukamba ambao ni shilingi milioni 811. Pesa iliyobaki tunaweza pia kujenga mradi wa Horohoro ambao ni takribani shilingi milioni 350. Pesa ambayo tume-*save* kwenye mradi huu kwa kutokumpa kazi mkandarasi yule tunaweza kujenga mradi wa Tunduma kwa shilingi milioni 500. Kwa kweli watu wengi wanapiga pesa kwenye miradi ya maji kwa njia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukusimama hapo, tulikwenda kuchukua mradi wa pili, mkandarasi huyu aliomba kazi hii kwa shilingi bilioni 1.6, baada ya kufanya mahesabu vizuri tukaona kazi ile inaweza kujengwa kwa shilingi takribani milioni 800 mpaka bilioni 1, hapa kuna takribani shilingi milioni 600 zingeliwa na mkandarasi. Pesa hizo tukizitumia tunaweza kuchimba takribani visima virefu 30 ambapo Wabunge wengi hapa wana shida ya visima hivyo. Kwa kweli kuna changamoto kubwa Wizara ya Maji na tumejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona tatizo hilo, tukaenda tena mbali tukaangalia miradi kama mitatu, minne tukaona tatizo ndiyo hilohilo. Sasa tulifanya nini kama Wizara.

Kuna mambo ya msingi tulifanya, hatua ya mwanzo tuliyochukua, tulifuta vibali vya miradi yote husika na tukaja na utaratibu mpya wa kutafuta mkandarasi na mkandarasi huyu tutatumia Mamlaka yetu ya Maji ambayo itafanya kazi nzuri na kwa bei nafuu na kwa muda mfupi kuliko mkandarasi yule aliyekuwa amependekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili tuliyochukua ni kuondoa watumishi 14 ndani ya Wizara ya Maji kwa muda wa wiki mbili. Watumishi watano (5) tumewaondoa Idara ya Maji Vijijini; watumishi watatu (3) Idara ya Manunuzi au Sekta ya Manunuzi; tumemuondoa Mkurugenzi wa Manunuzi, Msaidizi wake na mtumishi mmoja; tumeondoa watumishi watatu kwenye Mfuko wa Maji na Bodi yote ya Mfuko wa Maji tumeiondoa kwa sababu hivi ndivyo vilikuwa vichocho vya kupigia pesa za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa tumejipanga kusafisha. Ni lazima wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji wabadilike, lazima wafanye kazi kwa uadilifu na weledi mkubwa. Wakati wa kupiga Serikali sasa imetoshwa, haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumefanya ni kuimarisha idara mbalimbali za Wizara ya Maji. Tumeimarisha Idara ya Maji yenyewe kwa kuunganisha maji vijijini na mjini; tumeboresha Kitengo cha Manunuzi, tunaboresha Mfuko wa Maji na tunaboresha Kitengo cha Usanifu ambapo penyewe pana matatizo makubwa. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuwa Wizara ya Maji itabadilika, lazima ibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kila siku watu wanakaa ofisini wanapiga pesa lakini Watanzania wetu wanapata taabu ya maji safi na salama, hii haiwezekani. Imetoshwa, lazima tujipange, aliyekuwa hawezi kufanya kazi hii anaondoka. Kama ni Mkurugenzi, kama ni nani, wote wanaondoka, lazima Wizara ya Maji inyooke. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha hilo, tumesema sasa Wizara ya Maji lazima tuje na mpango wa kujua gharama za miradi ya maji. Kwa mfano, tunalofanya sasa hivi tunataka kujua *unit cost* kwa kila mradi, ukijenga tenki pengine la lita milioni mia moja itatumia shilingi ngapi, tunataka kuleta kitabu ambacho kitaonesha bei halisi za mradi wa maji ambapo Wahandisi wetu wa *RUWASA* na wengine wote watatumia kitabu hicho kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata thamani ya pesa tunayoingiza kwenye miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunafanya maboresho makubwa ni uanzishwaji wa *RUWASA* (Wakala wa Maji Vijijini. Kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema, kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema kwamba Wahandisi wa Halmashauri ni tatizo, sasa tunakuja na *RUWASA*, wafanye kazi pale, tuhakikishe kwamba tunapata thamani ya miradi tunayotekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo kila Mhandisi anayetoka Halmashauri tutampeleka *RUWASA*. Kazi tutakayoifanya tutahakikisha tunafanya upekuzi wa kina kwa Wahandisi wote wanaotoka Halmashauri, hatutaki kupeleka watu wapigaji kwenye *RUWASA* hii mpya tunayoianzisha. Naomba niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge, tatizo la maji litamalizika na tumejipanga kuhakikisha kwamba tatizo la maji linakwisha na wananchi wetu wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nalotaka kuchangia ni kuhusu upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Fungu Na.49 - Wizara ya Maji, iliidhinishiwa bajeti ya maendeleo shilingi bilioni 673.214. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi bilioni 343.486 zilipokelewa. Tarehe 30 Aprili, 2019, Wizara ilipokea tena shilingi bilioni 56.26 ambapo shilingi bilioni 12 ni za Mfuko wa Maji na shilingi bilioni 44 ni pesa kutoka Serikali Kuu ama Hazina. Mpaka kufikia tarehe 30 Aprili, 2019, Wizara ilipokea shilingi takribani bilioni 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa madeni ya wakandarasi. Kama alivyoongea Naibu Waziri, hadi kufikia mwezi Aprili, Wizara ilikuwa na *certificates* za miradi mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 78.67. Baada ya kupokea fedha hizo, shilingi bilioni 56.256 ambazo kwa sasa tunaendelea kuwalipa wakandarasi hao, deni la *certificates* limepungua kwa asilimia kubwa sana na *certificates* tunazozipata sasa hivi tunazifanyia uhakiki ili tuhakikishe nazo zimeenda sawa baadaye tuanze kuzilipa mwezi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuhakikishia wewe na Bunge lako Tukufu itakapofika mwezi Juni wakandarasi wote watakuwa hawatudai. Hata hivyo, naomba muelewe kwamba kila siku wakandarasi wanazalisha *certificates* kwa sababu kazi zinaendelea *site*, lakini tumejipanga tuhakikishe kwamba kila *certificate* inayokuja tunailipa lakini baada ya kuhakiki kwa sababu Wizara ya Maji kuna historia ya upigaji, lazima tujipange tuhakikishe kwamba tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nalotaka kulizungumza, Mheshimiwa Naibu Waziri ameligusia kidogo, ni tozo kwa watumiaji maji chini ya ardhi (tozo ya uchimbaji visima). Kupitia Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Na. 11 ya mwaka 2003, kifungu cha 96 na Kanuni zake kinanipa mamlaka ya kusimamia tozo za uchimbaji visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Spika alizungumza hili kwa masikitiko makubwa na sisi kama Serikali tulilisikia. Waheshimiwa Wabunge mlilizungumza jambo hili la tozo ya uchimbaji wa visima kwa masikitiko makubwa, tulilisikia. Watanzania wanyonge wamelalamikia jambo hili tumelisikia. Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, imesikia kilio cha wanyonge, cha Watanzania kuhusu tozo ya watumiaji wa visima vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia leo Serikali imefuta tozo ya visima vya maji kwa watumiaji binafsi kwa matumizi ya nyumbani. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena; kuanzia leo Serikali imefuta tozo ya visima vya maji kwa watumiaji binafsi kwa matumizi ya nyumbani. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa lazima wapate maji safi na salama. Hhatuwezi kuona Watanzania wetu wanalalamika na wanapata shida, Serikali tunafanya kila tunaloweza kuhakikisha kwamba matatizo haya tunayaondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni huduma za usambazaji wa maji vijijini. Sera ya Taifa ya 2002 inasema waziwazi Watanzania wapate huduma ya maji si zaidi ya mita 500 kutoka maeneo wanayoishi. Vilevile Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba itakapofika mwaka 2020, Watanzania waishio vijijini wapate maji asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumejipanga, tunaendelea kutekeleza miradi mbalimbali. Hadi hivi sasa jumla ya miradi 1,659 yenye vituo vya kuchotea maji 131,370 imejengwa. Kati ya vituo hivyo, vituo 86,780 vinafanya kazi na vina uwezo wa kuwahudumia wananchi milioni 25.359. Aidha, miradi 653 yenye gharama ya takribani shilingi bilioni 501 inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujipanga hivyo, Serikali inatekeleza miradi mingine kwa mfano tuna mradi wa maji vijijini ambao unagharimu takribani shilingi bilioni 46.47 ambapo mradi huu tunaita *payment by result*. Tuna mradi mwingine ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo gharama yake ni takribani shilingi bilioni 806 na kazi yake kubwa ni kupeleka huduma ya maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya miradi ya vijijini ni kama ifuatavyo. Kama nilivyosema mwanzo, miradi mingi iliyojengwa kati ya 2010 - 2015 imejengwa chini ya viwango. Kazi yetu sisi kama Serikali na kama Wizara ni kuendelea kuhakikisha kwamba miradi hii tunaisawazisha ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.



Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo lina changamoto ni uharibifu wa mazingira. Hali ya tabianchi inabadilika kila siku na baadhi ya maeneo yana changamoto sana. Tunachimba kisima leo baada ya miaka kumi kisima hicho kimekauka. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba Watanzania wenzangu tupambane na hali hii ili kuhakikisha kwamba miundombinu tunayojenga hii inakuwa endelevu ili tuweze kutumia sisi wenyewe pamoja na vizazi vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine iko kwenye usimamizi wa Jumuiya za Maji. Utakumbuka Bunge lako Tukufu hapa lilipitisha Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira, Na. 5 ya mwaka 2019, ambayo yenyewe imeeleza kwa kina uboreshaji wa jumuiya hizi za watumia maji. Tunaamini tukiweka mambo haya vizuri, miradi ya maji kwa kiasi kikubwa itafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye eneo la huduma ya maji mijini. Kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeeleza waziwazi ifikapo mwaka 2020 wananchi watakaopata maji kwenye miji mikuu ya mikoa lazima iwe asilimia 95. Hali ikoje leo hii? Hivi tunavyozungumza kuna baadhi ya maeneo watu wanapata maji asilimia 97, 90, 86, lakini kwa wastani watu wanaopata maji kwenye miji mikuu ya mikoa ni asilimia 87. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga kuhakikisha kwamba tutafikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2020. Katika kujipanga huko kazi ya mwanzo tuliyoifanya ni kuhakikisha tunaboresha utendaji kazi wa Mamlaka zetu za Maji, hilo la kwanza, kwa sababu kama mamlaka za maji zitalegalega hatutaweza kufikia malengo tuliyojiwekea. Kwa hiyo, kazi ya kwanza tuliyojiwekea ni uboreshaji wa utendaji kazi wa Mamlaka zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo jambo la kwanza tulilofanya ni kuweka *performance contract* (mikataba ya kazi) baina ya Waziri na Mwenyekiti wa Bodi, baina ya Katibu Mkuu na Mtendaji wa Mamlaka, lazima tuwapime kutokana na utendaji wao wa kazi. Hatuwezi kuendelea biashara kama

kawaida, watu wanafanya wanavyotaka, watu wanakaa hawafanyi kazi, hili tutalisimamia na mimi ntalisimamia kwa nguvu zangu zote. Mtendaji Mkuu yeyote ambaye hatafanya kazi kama tulivyokubaliana, tutamuondoa. Lazima Mamlaka za Maji zibadilike, lazima Wizara ya Maji ibadilike, lazima Watanzania sasa waone matokeo makubwa ya Serikali yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumefanya maboresho kwenye ulipaji wa bili za maji. Kuna changamoto kubwa kwa baadhi ya maeneo ya watu kutokulipa bili za maji. Tumeamua sasa tulete *prepaid meters*, mita za kielektroniki ambazo tumezifunga watu waweze kupata huduma nzuri na walipe maji kutokana na matumizi wanayotumia. Kwa sababu kulikuwa na mchezo kwa baadhi ya Mamlaka kuibia wananchi lakini ukitumia *prepaid meter* sasa utalipa kutokana na matumizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tutalisimamia na tutahakikisha kwamba tunafunga *prepaid meters* maeneo mengi. Bado *prepaid meter* bei yake iko juu lakini tutajitahidi kama tunavyoweza tuhakikishe kwamba tunawafungia wananchi wengi ili waweze kupata huduma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeamua kwenye Mamlaka hizi kuboresha miundombinu ili kupunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa maji. Kuna upotevu wa maji kwenye maeneo mengi sana na tumeamua kujipanga kuhakikisha kwamba upotevu wa maji unapungua kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumekubaliana na Mamlaka za Maji, kwenye mapato yao lazima kila mwezi watenge asilimia 35 ili waende kujenga miundombinu ya maji. Utaratibu uliokuwepo zamani Mamlaka zote za Maji zikitaka kujenga mradi zinakuja Wizarani kuomba pesa kwenye Mfuko wa Maji. Baada ya kuingia Wizarani nikawaambia hii haiwezekani, ninyi mnafanya biashara, mnauza maji, lazima muanze kujenga miundombinu ya maji na tumejipanga na hii tunaisimamia kwelikweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano, DAWASA (Mamlaka ya Maji ya Dar es Salaam) tayari wanajenga miradi mbalimbali kwa kutumia pesa zao za ndani. Mradi wa kwanza ni ule wa Chalinze – Mboga – Bagamoyo ambao unatumia takribani shilingi bilioni 10.7. Mradi wa pili ni Kibamba – Kisarawe ambao vilevile unajengwa kwa pesa za ndani za Mamlaka ya Maji DAWASA na tunatumia takribani shilingi bilioni 10.67. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingine kwa mfano usambazaji wa maji maeneo ya Kiwalani, Madale, Usukumani na mengine mengi, kote huko tunapeleka huduma ya maji kwa kutumia pesa za Mamlaka zenyewe. Pia tuna mradi ule wa visima Kimbiji, tayari tumeshatangaza tenda ambapo tutatoa maji kutoka visima vyetu vya Kimbiji kuleta pale Kigamboni na tunajenga matenki na kazi hii itafanywa kwa kutumia pesa za ndani za DAWASA. Hatuwezi kuendelea tena kuanza kuzibeba Mamlaka hizi za maji wakati zinafanya biashara, zinafanya kazi, lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ambalo nataka kulizungumzia ni miradi ambayo tunaitekeleza ili kufikia malengo tuliyopewa na ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hivi ninavyozungumza, tunatekeleza mradi wa maji kutoka ziwa Victoria kwenda Nzega Igunga, Tabora, Uyuwi, ambao unagharimu takribani shilingi bilioni 605. Tunatekeleza vile vile, mradi wa maji wa Arusha ambao unagharimu takribani shilingi bilioni 525.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti Bariadi, Busega, Itilima, ambao utagharimu takribani shilingi bilioni 300 na mkataba ulisainiwa hivi juzi. Tuna changamoto kwenye miji mingi hapa Tanzania Serikali kwa kulitambua hilo, Serikali kwa mapenzi makubwa yaliyonayo kwa wananchi wake inatekeleza mradi wa miji 29 ambao unafadhiliwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Indi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utagharimu takribani shilingi tirion moja nukta mbili, miji ambayo itanufaika na mradi huu kwanza ni muheza, Wanging'ombe, Makambako, Kianga, Songea, HTM, Korongwe na handeni, Njombe Mugumu Kilwa Masoko, Geita, Chunya, Makonde, Manyoni, Sikonge, Kasulu, Lujewa, Chato, Singida Mjini, Kiamboi, Mpanda, Chemba, Mafinga, Urambo, Kaliuwa, Pangani, Ifakara Rorya, Tarime, Chamwino na Nanyumbu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inaendelea vizuri na tunategemea wiki inayokuja tutasaini na mkandarasi ambaye atapitia usanifu na kutayarisha makabrasha ya zabuni nitawaalika Wabunge wote ambao wanapitiwa na mradi huu waje washuhudie sherehe hii kwa sababu ni jambo muhimu katika maisha ya watanzania wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulifuatilia hili, tutampa mkandarasi huyu au mtaalam mshauri huyu miezi miwili aweze kumaliza usanifu na kutupatia makabrasha ya zabuni na tunategemea mambo yote yatakwenda vizuri mkandarasi atakuwa kwenye *site* bayana ya mwezi Septemba na mwezi Oktoba ili aanze kazi ya kujenga miundombinu kwenye maeneo mbalimbali hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunao mradi wa kupeleka maji miji sita ambayo ni Mwanza, Musoma, Bukoba, Misungwi na Lamadi ambao unagharibu takribani shilingi bilioni 276. Tunao mradi wa kiistoria, mradi wa Mugango Kiabakari Butiama, ambao utagharibu takribani shilingi bilioni 30.69. Mradi huu umezungumzwa kwa muda mrefu, lakini sasa tulishafikia mahala pazuri tulishapata mkandarasi tumeshaandika BADEA kwa *no objection* BADEA imeshatoa *un objection* Kuwait fund imeshatoa *un objection* sasa tuna subiri *no objection* kutoka Saudi fund na tunategemea hivi karibuni watatuletea na mkandarasi ataanza kufanya mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie ndugu zangu wa Mugango, Kiabakari, Butiama, na Musoma

kwa ujumla kwamba itakapofika mwisho wa mwezi wa sita tunategemea mkandarasi awekwe *site* tutatuwe tatizo la maji ambalo linawakabili. Pia tunayo miradi mingi sana tuna mradi pale Dar es Salaam, mradi wa wasambaji maji ambao unagharimu takribani shilingi bilioni 197.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite kidogo na eneo ambalo ya miradi ambayo imejengwa kutoka mwaka 2010 mpaka 2015 lakini hayatoi maji. Kuna miradi takribani 88 ambayo ilijengwa mwaka 2010 mpaka 2015 lakini haitoi maji miradi hiyo kwa mfano; kuanzia mradi wa masoko kule Rungwe Mbeya, mradi wa Mwanza Shirima kule Kwimba, mradi wa Tunduru kuna mradi wa Mbesa, kuna mradi wa maji kule Matimira, kuna mradi wa maji kule Singida ambayo ni Ikole Migingi, Kuna mradi wa maji kule maeneo Kigoma Kankoko, ambayo kuna miradi sita haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuja na mpango wa kuhakikisha kwamba miradi hii yote inafanya kazi na wala hatutaleta mkandarasi tutatumia wataalam wetu wa Mamlaka za Maji, hivi tunavyozungumza mradi wa masoko wako watu tumenunua mabomba na wako vibarua takribani 80 wanachimba mtaro kuhakikisha kwamba kazi ya mradi huo inamalizika mara moja. Vilevile, kwa mradi wa Kakonko huko Kigoma tumepeleka wataalamu wetu kutoka Moshi, Mamlaka ya Maji Moshi ambayo wanauwezo mzuri wa kujenga vyazo vya maji kwenda kufanya kazi hiyo huko Kakonko Kigoma ili kutatua matatizo ya maji ya huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi kwa mfano ya kule Kwimba tumepeleka Mamlaka ya Maji ya Mwanza kuhakikisha pia wanamaliza tatizo la mradi huu naomba niwahakikishie ndugu zangu watanzania, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wengine wametuona kule Mbeya vijijini matatizo ya maji kwenye maeneo mengi tutayamaliza ili kuhakikisha watanzania watapata maji safi na salama. Kama mradi umejengwa 2010 mpaka 2015 lazima tuukarabati kwa sababu wataanzania wanalotaka wao ni kusikia habari ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mazungumzo kuhusu wataalam wa maji ni kweli wataalam wa maji wengine wanachangamoto kubwa, wataalam wa maji wengine weledi wao ni mdogo, wataalam maji wengine hasa wa halmashauri uwezo wao ni mdogo, wataalamu wengine wa halmashauri siyo waadilifu, lakini pia nina amini wapo baadhi ya wataalamu ni wazuri sana na wataalam hawa wanategemea kuangalia kiongozi wao kama kiongozi wao anaonyesha njia kama kiongozi wao unasimamia vizuri na wao watajifunza kutoka kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba niwahakikishie kwamba tutafanya kila tutakaloweza tuchukuwe wataalam ambao ni waadilifu na tutasimamia kwa uwadilifu mkubwa. Kama nilivyosema mwanzo mtaalam yoyote kama yupo halmashauri, kama yupo kwenye mkoa, kama yupo wizarani, akifanya uzembe kama si mhadilifu nitamfukuza hapo hapo bila kupoteza hata muda. Nia yetu lazima tujenge Wizara ya maji mpya, Wizara ya maji ambayo itakwenda kujibu matatizo ya watanzania watanzania wamechoka wanahitaji maji Safi na Salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *issue* nyingine wa uvunaji wa maji tumesikia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili tumelichukuwa na tulizielekeza halmashauri zitengeneze sheria ndogo ndogo kwa ajili ya kuvuna maji hasa kwenye majengo na taasisi za Serikali kwa vile hili naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kulisimamia kuhakikisha kwamba tutafanya kazi hiyo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa vyanzo vya maji, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira amelizungumza sana hili kwa kweli utunzaji wa vyanzo vya maji ni muhimu sana kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka, tunazungumzia mwaka 1962 wakati watanzania wapo milioni 10 upatikanaji wa maji kwa mto mmoja ilikuwa mita za ujazo 7862, leo hii tuko watu karibuni milioni 54 upatikanaji wa maji takribani au upatikanaji kwa maji kwa mtu mmoja ni lita za ujazo 2300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujipange kwa sababu tulipoangalia vizuri tunaelekea chini ambako baadaye nchi yetu itakuwa na shida kubwa ya maji hili, jambo linaweza kutokea popote nyote Waheshimiwa Wabunge mlikuwa mashahidi *South Africa Cap town* siku zake zilizopita kulikuwa na changamoto kubwa ya maji, sisi tumejipanga kuhakikisha kwamba tunatunza vyanzo vya maji tunapanda miti na tunafanya kilimo ambacho kinaenda na vyanzo vya maji hasa kwenye maeneo ya vyanzo vya maji, hiyo ni muhimu sana kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji hivi tulivyonavyo vinakuwa endelevu tuvutumie sisi pamoja na watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunajaribu kuweka mipaka tunapima mipaka kwenye vyanzo vya maji ili visianze kuvamiwa vamiwa, tumejipanga vizuri tukishirikiana na wadau wote kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vyote tunavilinda na vinakuwa salama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge Wabunge wengi wamezungumza kwenye michango yao kwamba na mahitaji ya visima, na Waheshimiwa Wabunge tutatoa karatasi kila Mbunge aandike mahitaji yake ya visima ili tuanze kuhifanya kazi hiyo kwa uharaka sana kwa sababu wananchi wetu hatutaki wapate tabu hii ni muhimu sana tutatumia *resources* zetu zote, tutatumia nguvu zetu zote, tutatumia utaalam wetu tuhakikishe visima hivyo vimechimbwa haraka iwezekanavyo. Yule ambaye atashindwa kwenda na *speed* yetu tutamwambia imetoshwa kaa pembeni, tumejipanga kuhakikisha kwamba nchi yetu sasa kwenye sekta ya maji tunaenda mbele tumechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Bwawa la Kidunda ni kweli imekuwa muda mrefu lakini tunajipanga sasa Serikali kuanza kufanya kazi ya ujenzi wa Bwawa hilo ili tuwe na maji ya uhakika kwa ajili ya Dar es Salaam, Bagamoyo na Kibaha, tutafanya kazi hiyo hiyo kwa bwawa la Farkwa, ambalo linategemiea sana na chemba na hapa Wilaya ya Chemba pamoja na jiji hili la Dodoma ambalo Serikali iko

hapa makao Makuu yake, tumejipanga kwa ufupi kuhakikisha kwamba sekta ya maji matatizo yote tunamaliza ili watanzania wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa sasa ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa imeungwa mkono na Bunge zima, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi, Waheshimiwa tukae, Katibu.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 - Wizara ya Maji**

Kif. 1001 - *Administration and HRM*..... Sh. 3,417,225,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nina orodha hapa, orodha ndefu aya tunaanza na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nilitarajia kushika shilingi kwenye mshahara wa Waziri kuhusiana na lile suala la kuongeza shilingi hamsini, lakini kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri Profesa na mikakati aliyoiweka naondoa hoja yangu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana, naomba nipate *commitment* ya Serikali kwenye suala



la kuondoa kodi katika mitambo ya kuchimbia maji, lakini pia mitambo ya kutengenezea mabwawa na pia *pump* zile za sola ambayo itafanya urahisi wa kupeleka maji hasa huko vijijini maji yawafikie mpaka mlangoni, nilikuwa naomba *commitment* ya Serikali kwamba iweze kutusaidia kufanya jambo hili na kama hatutapata *commitment* ya uhakika basi ningepomba na Wabunge wenzangu, nijenge hoja ili tuweze kujadili ili tuweze kupata uhakika kwamba jambo hili sasa ni muda wa kufanikiwa ili mitambo yote hiyo iondolewe kodi, upatikanaji wa mabwawa lakini pia na visima iweze kushika bei *private sector* iweze kuunga mkono juhudi za Serikali. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Jitu Soni hoja yake hii na Serikali tuna tambua umuhimu wa mitambo hii ya kuchimbia maji na Mheshimiwa Jitu Soni naamini anafahamu kabisa kwamba Serikali kwa sasa ipo kwenye mchakato wa kubadilisha kodi mbalimbali na tozo mbalimbali, kikosi kazi kipo kazini na tayari tumeshakaa kikao cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Mheshimiwa Jitu soni kwamba, kwanza nimshukuru yeye kwa kuliona hili na kuendelea kuwatetea wananchi kwa ajili ya jambo hili maji tunayaitaji sana. Namshukuru kwa sababu nimeona amewasilisha hiki anachokiongea ndani ya Bunge lako Tukufu na Serikali tunaendelea kuyachambua maombi haya yote na tunapokamilisha tunapokuja na *finance bill*, naomba nimuambie Mheshimiwa Jitu Soni kwamba anafahamu utaratibu ulivyo basi jambo hili asiliwahishe Bunge ni hili hili tutaonge hapa hapa kwenye ukumbi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Jitu Soni asikamate shilingi ya Mheshimiwa Waziri wa maji ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini wazo aliotoa Mheshimiwa Naibu Waziri na tayari kwa sababu ipo ofisini kwake na iko *task force* yake naamini mwaka huu itafanyiwa kazi nashukuru naunga mkono. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante tuna, tutasubiri siyo mbali Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, hoja yangu ni suala la mpangilio wa kibajeti ambalo mahususi linausisha halmashauri ambazo ziko chini ya asilimia hamsini kwa wananchi wanaopata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajuwa sera ya maji ya Mwaka 2002 wanatakiwa wananchi wapate maji ndani ya mita 400, lakini halmashauri nyingi zinapata fedha dongo ya kibajeti ambapo haiwezi kukidhi kufikisha wastani wa kitaifa wa 2020 wa asilimia 85. Sasa kama maelezo yatakuwa ni mazuri sitakuwa na kusudio la kushika shilingi; je, Serikali ipo tayari kuboresha hii ramandama ili zile halmashauri ambazo zinapata chini ya asilimia 50 wananchi wanapata maji safi na salama waweze kuongezewa mgao na ili malengo ya kufika asilimia 85, 2020 yaweze kufikia hata kwa uchache nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahasnte, Mheshimiwa Waziri wa maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na imesema wazi wazi kwamba itapofika mwaka 2020 Watanzania wanaopata maji vijini lazima wawe asilimia 85. Sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba tunafikia malengo hayo. Zile Halmashauri ambao ziko chini kabisa, tutatumia nguvu kubwa tuweze kupeleka maji zaidi au tupeleke miradi ili tuweze kufikia asilimia hiyo kwa sababu hii tumewekeana ahadi na wananchi, lazima tuitekeleze.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* ya Serikali, nimemsikia Mheshimiwa Waziri, lakini lengo ni kwamba kuna Halmashauri ambazo ziko chini ya asilimia 50, sasa je, anatoa-*commitment* ipi ya kuzisaidia kibajeti ziweze kupanda angalau kusogea hata kwa asilimia 60?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama maelezo ya Mheshimiwa Waziri hayatajikita zaidi, nitatoa hoja tuweze kulijadili.

**MWENYEKITI:** Katika hatua hii Mheshimiwa toa hoja tu.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hujaungwa mkono. Tunaendelea Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa hoja yangu kwa Mheshimiwa Waziri. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji. Naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo imekuwa kifanya katika miradi ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna miradi mikubwa ya maji kupitia mabonde, mito, maziwa na hii miradi mikubwa huwa inachukua muda mrefu sana kukamilika, inaweza kuchukua miaka mitatu, miaka minne, mitano, mpaka sita na sasa hivi tunavyovisima, karibu nchi nzima kuna visima vidogo vidogo vingi sana ambavyo vimekuwa vikiwasaidia wananchi, lakini hivi visima kuna visima ambavyo ni vibovu havifanyi kazi kuna visima vingine vinafanya kazi lakini ni virefu na vifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua, wakati tunasubiri hii miradi mikubwa, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha, kwanza kabisa tunajua kwamba vitakavyokuwa vinakarabatiwa hivi visima vitamtua ndoo mwanamke

kichwani na ndiyo nia yetu na hata wakati wa kujadili, akina mama wengi na akina baba wengi wamekuwa wakilalamika kuhusiana na maji, lakini kuna maji yamesababisha hata ndoa za akina mama, kuna mwenzetu mmoja...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta, unataka...

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni nini mkakati wa muda mfupi wa ukarabati wa hivi visima wakati tunasubiri miradi hii mikubwa ya maji? Serikali labda ituambie ili kusaidia hili tatizo la maji nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hoja yangu hapa nilisema kwamba tutatoa karatasi ambapo kila Mbunge mwenye mahitaji ya visima ama kuna visima ambavyo havifanyi kazi watuandikie Serikali tuweze kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyosema mara nyingi, nia ya Serikali ni kuwapelekea Watanzania maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Naomba Wabunge wote tulete hizo orodha na tuombe Serikali haya majibu yawe ya uhakika ili kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika nchi nzima na wanawake na akina mama wote tupate hii miradi ya maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na hoja zangu za msingi zimejibiwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** ...lakini nina moja ambalo...

**MWENYEKITI:** Alah!

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna moja naomba kuongezea kuhusu mabwawa. Amesema atapitisha karatasi ili watu wote wenye shida ya visima virefu waweze kuorodhesha. Naomba atoe *commitment* kwamba mabwawa ambayo ndiyo tegemeo la nyanda kame za nchi yetu kwa sababu ya kukamata au kuteka maji ya mvua inaponyesha, pia apitishie karatasi tumweleze maana tuna mabwawa mengi yaliyopasuka au kujaa udongo katika sehemu mbalimbali za nyanda kame za nchi yetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya hivyo kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge, tutaleta *list* halafu tutafanya hivyo kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikusudia kushika shilingi juu ya ucheleweshwaji wa *finance agreement* ambayo ingesaidia ujenzi wa chanzo kipya cha maji ambayo kiukweli yangepeleka maji maeneo ya Wilaya za Illemela kule Busweru, Buhongwa Nyamagana, Kisesa kule Magu pamoja na Usagara kule Misungwi, lakini maelezo ya Mheshimiwa Waziri ya awali yamejitosheleza na hivyo naondoa hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kuhusiana na suala la ubadhirifu kwenye miradi ya maji maeneo mbalimbali ya nchi na uwepo wa

miradi mingi ambayo haitoi maji. Iwapo majibu ya Mheshimiwa Waziri hayataridhisha, nitaomba nitoe hoja ya kuondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwaka jana alieleza kwamba iliundwa kamati ya wataalamu chini ya Prof.r Mbwete kupitia miradi nchi nzima; na leo katika majumuisho ameeleza kwamba kamati ile ilibaini kuna changamoto 17 na imetoa mapendekezo 50 ya kufanyiwa kazi, lakini sisi kama Wabunge hatujapewa fursa ya kuiona hiyo ripoti ya Kamati ya Prof. Mbwete tuone je, walipita kwenye Halmashauri zote? Nini hasa walibaini katika Halmashauri mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiomba kwa Serikali ni Serikali kuiwasilisha hiyo ripoti Bungeni ijadiliwe na Bunge, Bunge lipitishie maazimio na iwapo Bunge halitaridhika, Bunge liweze kuunda kamati yake ya kuchunguza na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali ya kuiwasilisha hiyo ripoti Bungeni, ijadiliwe na Bunge, huo ufisadi uliobainika, ubadhirifu na kila kitu, viweze kuchukuliwa hatua na Wabunge tuweze kuipitia kwa umoja wetu, tuone je, kwenye Halmashauri zetu huko walikopitia, wameona kile ambacho si tumeona? Wameona kile ambacho tumelalamikia hapa Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya Serikali iwapo Serikali iko tayari kuileta hiyo ripoti Bungeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, wewe ni Mbunge wa siku nyingi sasa. Ripoti ni za Mheshimiwa Waziri. Zipo ripoti ambazo ni za sera ambazo ndiyo Bunge linaweza likaletewa. Hizi za utekelezaji, za utendaji, ni za Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Ndiyo maana mnaweza mkaja mkamwajibisha yeye. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ilikuwa ni Azimio la Bunge, ulikuwa ni uamuzi wa

Wabunge walio wengi, lakini pili, nikinukuu maneno ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe, naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe anasema: "Kuna haja ya kuunda timu ya wataalam watakaopitia miradi yote iliyotekelezwa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnapendekeza. Mlipendekeza kwamba iingie Kamati ya Bunge lakini kama hamjafika hapo, naomba...

**MWENYEKITI:** Haukufika huko.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleweke. Naomba unielewe Mwenyekiti. Mheshimiwa Waziri alichokitaka ni kwamba kabla ya Bunge kuunda kamati, Kamati ya Wataalam ichunguze ili ripoti ya wataalam ije. Ni nini kinazuia ripoti ya wataalam ije? Kama Serikali haitaki kuwasilisha ripoti yake ya wataalamu, imefanya kuwa siri, basi Bunge sasa tuunde kamati yetu, tuende tukachunguze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha kazi mara mbili, Serikali ina uwezo wa kuleta ripoti. Mheshimiwa Mtemi Chenge, wewe ni Mbunge wa muda mrefu, nikupe mfano. Mheshimiwa Rais wakati huo Mheshimiwa Dkt. Kikwete, aliunda ripoti ya kuchunguza masuala ya madini Kamati ya Bomani, lakini Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa Bunge kwenye kuamua, akaamua pamoja na kuwa ni Kamati ya Rais, ripoti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote labda nitoe ufafanuzi kutokana na changamoto hizi za ubadhirifu wa miradi ya maji, sisi tukaona haja ya kuunda kamati ya watu 10 inayoongozwa na Prof. Mbwete. Moja ya changamoto kubwa alizokuja nazo na mapendekezo ni kuhusu suala zima la uanzishaji Wakala wa Maji Vijijini na pia kuanzishwa kwa Kitengo cha Kusanifu

Miradi Wizarani kwa maana *Design Unit* na kuimarishwa kwa Kitengo cha Ufuatiliaji wa Miradi ya Maji na kutolewa mafunzo (*contract management*) katika kuhakikisha tunakwenda kutatua changamoto hizi na wananchi waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza.

**MBUNGE FULANI:** Hajaelewa swali huyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu tuelewane kidogo. Masuala ya kuisimamia Wizara au Serikali kwa ujumla kupitia Wizara, tunazo Kamati za Kisekta na ndiyo huko sasa haya mambo huwa yanapelekwa yanajadiliwa kama ilivyokuwa kwenye taarifa ile ambayo umesema ilifika hata hatua ya kupendekeza kufanya hivyo. Sasa katika hatua hii ambapo Serikali imeshafanya kazi ile ambayo ilikuwa na upungufu huo; na kwa vile Kamati ya Kisekta itakuja tena kuwa *ceased*, yaani itaipokea tena katika mwaka ujao wa fedha na moja ya eneo ambalo itakuwepo, itakuwepo ni utekelezaji wa ahadi za Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa miradi ambayo ilikuwa na upungufu mkubwa wakati huo.

Sasa nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Mnyika, hili ndiyo unataka kufanya Serikali tuchukue muda kujadili? Nisaidie tu kwanza nielewane na wewe.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza huu uchunguzi ni wa toka mwaka uliopita wa fedha na kamati ya kisekta, Kamati ya Maji imefichwa kuhusu huu uchunguzi, haijapewa kuhusu uchunguzi, mpaka Wajumbe wengine wanaisikia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utoe fursa ili Bunge lako lijadili. Hii hoja ya ubadhirifu wa miradi ya maji na kuwa na miradi mingi hewa ni hoja kubwa sana. Hii ni hoja ambayo ilifanya mpaka Mheshimiwa Rais amwambie Mheshimiwa Waziri avute bangi kisirisiri aache upole ili kushughulikia mambo ya maji. Ni jambo kubwa. Bunge hatujajadili hili jambo. Fursa ya Bunge kujadili ni sasa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, turuhusiwe Wabunge tujadili, kama Serikali itaji-*commit* baada ya hapo kupeleka kwa Kamati ya Kisekta au utaratibu mwingine, ifuate baada ya Bunge kwanza kujadili jambo hili kwamba haturidhiki na hii hali kwamba huo uchunguzi umefanyika, ripoti imekaa kwa Serikali yenyewe, Bunge halijahusishwa mpaka sasa.

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba jambo hili lijadiliwe na Wabunge wote.

**MWENYEKITI:** Hamna hiyo, hamna hicho.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Nasema hivi, hapa tunaongelea Sera. Eeh, katika hatua hii tunaongelea sera na ndiyo maana kanuni niliyokuruhusu kusimama ni ya sera.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia Sera ya Serikali kuhusu kushughulikia ubadhirifu kwenye miradi ya maji. Kwa hiyo, tujadili kuhusiana na ambavyo Serikali haishughulikii vya kutosha ubadhirifu kwenye miradi ya maji na hii miradi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusiwe nitoe hoja tujadili hili jambo. Taarifa ya Serikali imeanzia 2010 wakati ambapo mwaka 2018 alituahidi angeanzia 2006 wakati programu ya maji ilipoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linahitaji mjadala wa Bunge, liko wazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba jambo hili lijadiliwe na Wabunge

**MWENYEKITI:** Nimelikataa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MBUNGE FULANI:** Ufisadi huu.

**MWENYEKITI:** Sera.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Sera gani? Mna sera ya kulinda ufisadi? Ina maana mna sera ya kulinda ubadhirifu na ufisadi kwenye miradi ya maji?

**MWENYEKITI:** Hebu mkae Waheshimiwa Wabunge, mkae tu. Mkae tu Waheshimiwa Wabunge. Bado narudia, katika hatua hii unasimama kwa suala la sera. Sasa kama kuna ubadhirifu katika utekelezaji wa mradi au miradi, hilo sasa mtakujakuliibua tu katika hatua inayofata. Maana sasa hivi hiyo ripoti ambayo Mheshimiwa Waziri ameletewa na timu yake ya wataalam ni ya kwake na mapendekezo yale ni ya kwake. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi Bunge tujadili tuunde kamati yetu basi. Kama ya kwake ni ya siri, ni ya kwake, sisi Bunge tujadili tuunde kamati yetu.

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu hata kusimama, nitakutoa nje. Sijakuruhusu kusimama, tusifanye mambo hayo, *please*. Tunaendelea.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Wakati nachangia nilieleza namna ambavyo miradi mingi ya maji hapa nchini inakwama kutekelezeka kwa muda kutokana na fedha kutokutolewa kwa wakati na pia kutolewa kidogo; na namna ambavyo Watanzania wengi bado wameendelea kuteseka kwa kukosa maji kwa sababu katika maeneo yao hakuna miradi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa ni kutokuwepo kwa fedha ya kutosha; na hata fedha ambayo imetolewa mwaka jana kwenye bajeti 2018/2019, ni asilimia 51 tu. Kwa hiyo, shida kubwa kwamba hakuna fedha ya kutosha kuweza kutekeleza miradi kwa wakati na ili pia kusambaza maji kwa wakati kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mfuko wa Maji uongezwe ili tuwe na hela ya kutosha kwa sababu mfuko ule utakuwa *ring fenced*, utakuwa umelindwa na fedha yake itakuwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji tu kama ilivyo kwa REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea, pamoja na mikakati mizuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza ya kuleta maji, hajatupa mkakati wa kuongeza fedha ambayo ni tatizo sugu, tatizo kubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, nini mkakati wa kuhakikisha kwamba tunaongeza Mfuko wa Maji uwe na fedha ya kutosha kuweza kutekeleza miradi kwa wakati lakini pia Watanzania wengi wanaoteseka wapate maji kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kukamata shilingi kama sitapata majibu ya uhakika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaongea pale nimesema changamoto kubwa ya miradi ya miradi ya maji ni usimamizi. Unaweza kuwa na mabilioni ya pesa, lakini kama usimamizi siyo mzuri matokeo yake watu wajanja wajanja wanapiga pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tulivyo sasa hivi tunaloimarisha ni usimamizi ndani ya Wizara ya Maji. Nimetoa mfano pale kwamba kuna Mkandarasi alikuwa anatengeneza *project* mahali fulani, gharama ya mradi ni shilingi bilioni 4.7 alioleta yeye, lakini mradi wenyewe unaweza kutengenezwa na shilingi bilioni 2.6 nukta saba. Unaona sasa. Asilimia 50 yule jamaa anapiga tu. Sasa kitu muhimu kwetu

sisi sasa hivi kwanza ni kuimarisha mifumo yetu, kuhakikisha kwamba pesa inayokwenda inakwenda kujibu changamoto ya maji. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hivi tunavyozungumza tumepata takriban shilingi bilioni 400. Sasa hivi tunawalipa Makandarasi wote. Ina maana mpaka ikifika mwezi Juni tutakuwa hatuna *certificate* yoyote. Kama nilivyosema pale, *certificate* kila siku zinazaliwa kwa sababu Makandarasi wako kwenye *site* na wanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Sakaya kwamba Makandarasi wote tutawalipa kwa muda na kuhakikisha kwamba miradi yote inatekelezwa kwa mpango tulioweka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba hii hoja Waheshimi Wabunge wachangie tuone *point* ni nini? *Point* ni kwamba naomba, naomba nikamate shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa toa hoja tu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ili Wabunge wachangie hoja hii ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Watanzania.

**MWENYEKITI:** Haijaungwa mkono.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kuunga mkono hoja)*

**MWENYEKITI:** Sawa, imeungwa mkono. Waheshimiwa sasa wale ambao mmeunga mkono mnaotaka kuchangia msimame tuwachukue majina. Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Sonia mbona umekaa, Mheshimiwa Rukia

nimekuandika hapa. Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Katani.

Haya Waheshimiwa tumewabeba wengi ili tuone. Waheshimwa Wabunge alichouliza, anachotaka Mheshimiwa Sakaya hiyo ndiyo ya sera. Kwa hiyo tukienda hivyo tutakwenda vizuri tu. Tunaanza Mheshimiwa Silinde fungua dimba.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya nikiwa na sababu ya msingi kabisa. Fedha tunayoomba iongezwe kwa maana ya shilingi hamsini kwenye tozo ya maji itasaidia moja kupeleka miradi mingi kwa wakati mmoja ambapo tatizo la maji nchi hii litaondelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nataka Wabunge wote muunge mkono suala la maji ambalo ndilo limekuwa kero kubwa kwenye Bunge letu. Sasa hivi mmeona nchi imekuwa na mradi mkubwa ikiwemo mradi wa reli ambayo kwa taarifa za uhakika kabisa Serikali itakuja kuomba tozo ya karibu Sh.112 iongezwe kwa ajili ya kugharamikia Mradi ya SGR. Sasa tatizo la maji ambalo ni kubwa naomba tuanze kuongeza shilingi hamsini kwenye maji ambayo inahusu Watanzania wote ikiwemo wale wa Momba kule vijiji ambao hiyo reli haiwezi kuwafikia. Kwa hiyo tunaomba hii shilingi hamsini iongezwe ili kutatua tatizo la maji kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga hoja upande wa Serikali kutokana na maelezo mazuri na mipango mizuri ambayo imeoneshwa wakati Mheshimiwa Waziri akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Namwomba Mheshimiwa dada yangu Sakaya kutokana na majibu mazuri yalitolewa na Serikali, hoja hapa sio kuongeza shilingi. Hoja tumekwishashuhudia na kuona ni jinsi gani ubadhirifu mkubwa wa miradi ya maji umekuwa ukifanywa na baadhi ya wakandarasi na hata wakati

mwingine baadhi ya watumishi wa Serikali wasio waaminifu. Kwa hiyo hata kama tunaongeza shilingi kama bado hatujaweza kudhibiti wizi unaofanywa na watu wasio waaminifu hatutakuwa tume-*solve* kitu chochote na tumekwishaona tayari Serikali imechukua mkakati wa kuona kwamba ni kwa jinsi gani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Massay Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya hata leo nilichangia hoja hii, lakini kwa sababu Waziri ameshaji-*commit* mwenyewe kwamba kuna fedha na amejieleza vizuri, tatizo hapa sio kuongeza fedha bali ni usimamizi wa fedha zenyewe. Nimwombe tumwachie nafasi wakati huu kwa sababu ni mara yake ya kwanza, ndio ameingia kwenye Wizara hii ili tuone sasa, amesema Juni, Juni sio mbali nimwombe Mheshimiwa Sakaya hebu amrudishie shilingi hiyo ili afanye kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napinga kabisa wazo la Mheshimiwa Sakaya la kutafuta hela, naunga mkono Serikali ameshasema Waziri pesa ipo, ni kusimamia na alizungumza mapema kabisa pesa imeharibiwa na Waziri hajasema ukweli, hawa walioharibu pesa ndio nataka kujua walioharibu miradi ya nyumba, wamejenga majumba, wamenunua magari ndio warudishe hela tupate maji vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hajajibu hoja kabisa, walioharibu miradi hiyo amewakamata kabisa na hela anajua wamechezea hizo hela za Serikali. Lazima walipe hizo hela za Serikali, zirudi ili watu wapate maji vijijini, hamna kuongeza tozo popote, fedha za Idara ya Maji zinatoshwa, tusimamie kwa ukweli ili mambo yaishe.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Sonia .

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya kwa sababu tumeshuhudia miradi mingi imekuwa ikisuasua na inachukua muda mrefu sana kutekelezeka. Hii ni ishara tosha kwamba hakuna fedha za kutosha katika eneo hili. Pia tunaposema kwamba tunataka kuongeza usimamizi bado na yenyewe hiyo ni gharama nyingine inaongezeka, hivyo bado pesa inahitajika katika Mfuko huu wa Maji. Hivyo, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jirani yako Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami pia namuunga mkono Mheshimiwa Sakaya kwa hoja yake. Tatizo kubwa lililopo ni kwamba hakuna fedha. Wabunge wengi hapa walichangia wakasema kama iongezwe hii hamsini, lakini kwa nini Serikali inakataa? Kwa sababu tatizo siyo Kaliua peke yake, tatizo wanaoteseka ni wanawake wa Tanzania nzima. Hili tatizo la maji limekuwa ni sugu, ingelikuwa kuna fedha huu Mradi wa Ziwa Victoria kuja Tabora, huu ni mwaka wa tano haujakamilika, angalau kama kungekuwa kuna fedha ukafika Tabora Mjini kwenda Kaliua ni kilometa 190 tu. Kwa hiyo nasema Serikali itafute fedha popote ikiwa hiyo hamsini hamkubaliani na sisi ili mradi ipatikane, tatizo la maji liondoke, wanawake wanaumia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya, suala la upungufu wa bajeti ya maji dhahiri shahiri Wabunge humu ndani sote tumeshuhudia. Kungekuwa na fedha za kutosha miradi mingi ya maji ingekuwa imetekelezeka. Fedha anazosisema leo Mheshimiwa Waziri ni fedha unasema unakwenda kulipa wakandarasi ambao

wako wanaendeleza miradi iliyoko huko *site*. Chemba nina vijiji 114, vijiji saba tu ndiyo vina maji, hivi ukiwalipa hao wakandarasi hivi vijiji vingine vinabaki na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Sh.50 iongezwe iwe Sh.100 tupate fedha ya kutosha, tukiambatanisha na usimamizi madhubuti Watanzania wengi watapata maji na hatimaye tutakuwa tumepunguza asilimia kubwa kwa ajili ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI AHMAD KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya ya kuongeza fedha kwenye maji kwa sababu za msingi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ukisikiliza hoja ya Serikali ambayo inasema kwamba na baadhi ya Wabunge wanasema kwamba kuna fedha zimeibwa na wakandarasi na nini, hii haiteti maana. Tumeona wakati hatujawa Wabunge hapa kulikuwa na miradi fedha zimepigwa, kulikuwa na miradi ya *Richmond* hapa lakini hatukuacha kujadili suala la umeme, hatukuacha kujadili maslahi ya Watanzania. Maji tunayozungumza, tunazungumza maji ambayo yatawatosha Watanzania wote, sasa hatuwezi kushindwa kuongeza fedha eti kwa sababu kuna ukaguzi wanatafutwa watu walioiba fedha. Hao walioiba fedha...  
*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunayo mifano mingi ya maeneo ambako



wakandarasi wamelipwa fedha zote lakini miradi haijakamilika. Kwa hiyo hicho peke yake kinaonesha kwamba tatizo siyo fedha, lakini pia tunayo mifano ya miradi ambayo fedha zimelipwa lakini maji hayatoki, hata kilio cha wananchi maeneo mengi wameonesha hivyo. La tatu, hiki wanachosema kwamba fedha iongezwe na chanzo wanachopendekeza, sote tunatambua mwaka huu mvua hazikunyeshwa vizuri kwenye nchi yetu kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa ukatokea upungufu wa chakula ambao unaweza ukasababisha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mwaka huu siyo muda muafaka sana wa kugusa viashiria vya kiuchumi kwa kuweka tozo ambayo inaweza ikasababisha mfumuko wa bei na kuongeza ugumu wa maisha kwa wananchi ambayo inaweza ikatuletea matatizo na... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Kwa hiyo naunga mkono hoja ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya. Ukiangalia kuna tatizo kama la asilimia tano tu ya usimamizi, lakini asilimia 95 ni *issue* ya fedha. Hili liliombwa mwaka jana Serikali ikakataa, lakini mwaka huu wameona kwamba hakuna chochote kimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo ambalo Serikali ya CCM imeshindwa kabisa ni katika eneo la maji. Tuongeze hii fedha ili tuwasaidie wananchi, wana wasiwasi ya *inflation*, *inflation* inaweza kutokea, mishahara haijaongezwa, kuna wasiwasi gani? Tuwaongezee watu maji ili mambo yaweze kwenda sawa. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashungwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumwomba Mheshimiwa Sakaya amrudishie Waziri shilingi yake kwa sababu ukiisikiliza Serikali, *concern* ya Wabunge kwamba mkakati wa kuongeza fedha tumeutambua lakini kuna haja ya kufanya maandalizi ili Mfuko huu utakapongezewa fedha, basi zisipotee kama zinavyopotea kwenye baadhi ya miradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimwombe Mheshimiwa Sakaya Serikali imemsikia lakini amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili aweze kwenda kwenye utekelezaji wa miradi na huko mbele Serikali itaongeza Mfuko wa fedha kama ilivyosikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nimwombe Mheshimiwa Dada yangu Magdalena arejeshe shilingi ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameonesha *commitment* kubwa ya kwamba anakwenda kuzisimamia fedha ambazo zimekuwa zikipelekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, mwaka huu tayari tumeshatoa shilingi bilioni 435 kwa ajili ya maji ambayo ni zaidi ya asilimia 59 ya bajeti ya maendeleo ya maji. Hii ni ya mwaka huu kwa miezi hii kumi tu ambayo tayari Serikali imeshafanya kazi. Mwaka jana tulitoa, ukiacha Mfuko wa Maji ambako tumepeleka fedha zote, tumepeleka bajeti ya shilingi bilioni 425, nina taarifa hapa ya ripoti ambayo inaonesha fedha hizi zilikwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili ili tumwelewe Mheshimiwa Waziri wa Maji, fedha hizi bilioni 425 zilikwenda

katika halmashauri zote 185, lakini tukijiuliza athari ya bilioni 425 za mwaka jana tunaiona kwa wananchi? Hilo ndiyo jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Waziri wa Maji anasisitiza. Tumpe nafasi ameanza kuisafisha Wizara yake ili fedha hizo zote zinazopelekwa, tuweze kuona maana ya fedha inayopelekwa, tatizo hapa siyo fedha, fedha ipo, ndiyo maana ndani ya mwezi huu mmoja tumelipa zaidi ya bilioni 88 kwa ajili ya miradi ya maji. Fedha ipo Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli mnamuona, anaeleza katika uhakiki ambao ...*(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Huo ndiyo mkakati wa Serikali kwenda kusimamia fedha hizi.

Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana. Dada yangu Mheshimiwa Sakaya ni mzoefu katika Bunge hili, lakini kauli ya Mheshimiwa Waziri ameitoa hapa kwa uchungu mkubwa sana, sijawahi kumwona Mheshimiwa Profesa Mbawala akizungumza kwa staili ya namna hiyo. Inaonesha kwamba ana *commitment* kubwa sana katika Wizara hii, hebu tumpe nafasi, nimwombe sana dada yangu Mheshimiwa Sakaya tumrudishie shilingi yake ili akatimize majukumu yake haya. Ametoa *commitment* tutaiona, kama kuna haja ya kurekebisha mwaka ujao tutaona inakuwaje, lakini nina imani kabisa kwamba alichokisema hiki atakitekeleza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN MOHAMED BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza linalonisikitisha upande wa Serikali na wengi wetu tuko tumeshikwa na *historical fact*, watu waliiba zamani, waliiba zamani. Kuna polisi, kuna TAKUKURU, kuna nani, *this is administrative job*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, jambo la maji ni jambo la msingi, hoja hii kama inawezekana Bunge hili, irudishe Kamati ya Bajeti tukajadili namna ya kuusaidia Mfuko wa Maji kupata fedha. Katika fedha ambazo Serikali inataja, *the best performing source* ni Mfuko wa Maji, kwa sababu ni *ring fenced*. Kwa hiyo hoja ya maji isiathirike na *administrative reasons* na *facts* ambazo zimetokana na wezi, waliofanya wameharibu, ni sawasawa uendeshe gari unaangalia *site mirror* badala ya kuangalia mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani kwamba kuna umuhimu sana ..... (Makofi)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe. Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa michango yote ya Waheshimiwa Wabunge, lakini kama nilivyosema kuna mambo mawili ya msingi hapo. La kwanza ni usimamizi, la pili hatulipi fedha tu kwa sababu tunalipa, tunalipa fedha kutokana na *certificates* zinazoletwa na wakandarasi. Kama wakandarasi hawajaleta *certificates*, hiyo ni shida na wakandarasi wetu wengine uwezo wao ni mdogo, mtu anafika karibuni asilimia 95 maji hayatoki. Sasa tumejipanga vizuri wakandarasi hao wajanja wajanja wenye historia tunawafukuza, naamini tukijipanga hivyo na tukisimamia vizuri, tutaenda vizuri. Naomba Mheshimiwa Sakaya, bado nasema hatuhitaji kuongeza fedha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia kwenye hili. Lengo hapa ni kupanua mtandao wa maji kwa watu ambao hawajawahi kufikiwa hata na miradi. Ninapooonga sasa hivi, Kaliua hawajawahi kupata

mradi wowote wa maji kwa miaka yote na maeneo mengine pia, ndiyo maana tunasema kuwa fedha ikiwa ya kutosha, achana na miradi ambayo ipo sasa hivi ambayo ina ubadhirifu watapanua mtandao watu wengine tupate maji kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri hapa wa Fedha amesema tumetoa fedha asilimia 59 mpaka sasa hivi. Leo ni Mei, imebaki miezi miwili bajeti imeisha. Tulitegemea angalau iwe imetolewa angalau kwa asilimia 90, kwa hiyo bado utoaji wa fedha hauendi sawasawa nan i kutokana na kwamba fedha hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe *realistic*, lengo ni kusaidia Watanzania na kiukweli hata ukiangalia takwimu na *data* ambazo zimetolewa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, siyo kwamba kwenye Wilaya tuna maji kwa asilimia 64, siyo kweli. Kwa hiyo, lengo letu ni kwamba tuwe na fedha ya kutosha, tusambaze maji kwa wakati, tusimamie miradi ndiyo Mheshimiwa Waziri ambayo ameiweka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, kwa kweli Watanzania...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Sakaya muda wako umekwisha. Ile hoja yako sasa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti Bunge liamue.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa Waheshimiwa Wabunge nitawahoji kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya ya kuongeza fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maji

(Hoja iliitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit.....	Sh.1, 215,000,000/=
Kif. 1003 - Policy And Planning Unit.....	Sh. 750,000,000/=
Kif. 1004 - Government Communication Unit.....	Sh. 290,000,000/=
Kif. 1005 - Legal Services Unit.....	Sh. 383,825,000/=
Kif. 1006 - Procurement Management Unit...Sh.	733,624,000/=
Kif. 1007 - Management Information System Unit.....	Sh. 363,337,000/=
Kif. 1008 - Internal Audit Unit.....	Sh. 367,901,000/=
Kif. 1009 - Project Preparation, Coord. and Delivery Unit.....	Sh. 200,000,000/=
Kif. 2001 - Water Resources.....	Sh. 6,218,400,000/=
Kif. 2002 - Central Stores.....	Sh. 0
Kif. 2003 - Water Laboratory.....	Sh.2,100,000,000/=
Kif. 3001 - Urban Water Supply and Sanitation Division.....	Sh. 4,683,962,000/=
Kif. 4001 - Rural Water Supply.....	Sh. 0
Kif. 4002 - Water Sector Program Coordination Unit.....	Sh. 0
Kif. 5001 - Water Development and Mangmnt Institute.....	Sh. 3,003,035,000/=
Kif. 6001 - Drilling and Dam Construction Agency.....	Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 49 – Wizara ya Maji

Kif. 1001 - Administration and Human Resource Management.....	Sh. 9,000,000,000/=
Kif. 1003 - Policy and Planning Unit.....	Sh.11,800,000,000/=

Kif. 2001 - <i>Water Resources</i> .....	Sh.35,000,000,000/=
Kif. 2003 - <i>Water Laboratory</i> .....	Sh.5,000,000,000/=
<i>Kif. 3001 - Water Supply and Sanitation Division</i> .....	Sh. 549,669,888,530/=
Kif. 4001 - <i>Rural Water Supply</i> .....	Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuweke rekodi sawa, hoja ya Mheshimiwa Sakaya, haikuwa kuongeza fedha kwenye Fungu la Wizara ya Maji, ilikuwa ni kuongeza shilingi hamsini. Kwa hiyo nataka ili tukae vizuri, tuelewane vizuri kabisa, maana ukiacha hivi inapotosha na kiti chenu, Mwenyekiti wenu asingependa alipotoshe Bunge kwa hoja ya Mheshimiwa Sakaya. Kwa hiyo narudia tena wanaoafikiana na hoja ya Mheshimiwa Sakaya...

**WABUNGE FULANI:** Hapana tumeshaamua.

**MWENYEKITI:** Mnasemaje?

**WABUNGE FULANI:** Tumeshaamua.

**MWENYEKITI:** Ndiyo kuamua tumeshaamua, lakini hoja inakaa vizuri tu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, mtoa hoja, Taarifa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Januari, 2016, Kanuni ya 104(3)(a) na (b) kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge,

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa na iamulie)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa hiyo natamka rasmi kwamba Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2019/2020 sasa yamepitishwa rasmi na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii niwashukuruni sana ninyi kwanza kwa kuichangia vizuri hoja hii na hatimaye kuipitisha, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Naibu wake Mheshimiwa Aweso lakini na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri waliyofanya kutufikisha katika hatua hii. Changamoto ya maji kama mnavyoona wote na mmezisema vizuri, bado ni kubwa, lakini pia tunaangalia hali ya tabianchi inazidi kutuathiri sana katika maeneo hasa kwenye vyanzo vya maji upatikanaji wake unazidi kupungua, lakini mahitaji yanaongezeka, idadi ya watu inaongezeka, mahitaji ya kiuchumi yanazidi kuongezeka, lakini mmefanya uamuzi wa busara rasilimali fedha hii ambayo mmeidhinisha.

Naamini wote tungependa tuone *value for money* na kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri aliyoyatoa, nadhani



tumpe nafasi hiyo, wakadhibitishwe hayo ambayo wanayo katika kuboresha utoaji wa huduma ya maji nchini.

Waheshimiwa Wabunge, baada kusema hayo, sina matangazo, kwa hiyo nawashukuruni tena na naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa Tatu Asubuhi siku ya Jumanne, tarehe saba mwezi wa Tano.

*(Saa 1.07 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 7 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*